

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Saba – Tarehe 11 DESEMBA, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati ifuatavyo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU
NA BUNGE:**

Taarifa ya Hali ya Madawa ya Kulevywa Nchini ya
Mwaka 2012.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 67

Utekelezaji wa Ahadi za Rais

MHE. OMARI R. NUNDU aliuliza:-

Utekelezaji wa ahadi za Rais ni jambo la kutiliwa mkazo sana kwani ahadi hizo hutolewa kwa nia njema ya kutatua matatizo katika jamii na kuchangia maendeleo ya nchi yetu:-

(a) Je, ni ahadi ngapi za Rais zimetolewa tangu tupate uhuru na zimekasimiwa kugharimu kiasi gani cha fedha?

(b) Je, ni asilimia gani ya miradi inayotokana na ahadi huwa inatekelezwa kwa kila awamu ya Urais tangu tupate Uhuru?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuko katika Awamu ya Nne ya Uongozi wa Nchi tangu Uhuru toka kwa wakoloni miaka 52 iliyopita. Serikali kwa sasa haina takwimu sahihi za ahadi mbalimbali zilizowahi kutolewa na Marais wote waliotangulia zinazoweza kuonyesha na kuainisha mchanganuo wa gharama za utekelezaji. Ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa kwa awamu mbalimbali za uongozi zimekuwa zikitekelezwa kwa kujumuishwa katika Makadirio ya Bajeti ya Serikali kila Mwaka wa Fedha kuendana na mipango ya muda mfupi, wa kati na muda mrefu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UR. NA BUNGE]

Kwa mfano, katika miaka hii mitano ya ahadi za Mheshimiwa Rais, Serikali ilichapisha Kitabu cha ahadi zote na hizi zimesambazwa katika Wizara mbali mbali na Halmashauri ili zitekelezwe kulingana na Bajeti za Wizara na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya ahadi hutekelezwa kwa awamu kulingana na uwezo wa Serikali. Hivyo, ahadi zinazotolewa kwa awamu moja zinaweza kuendelea kutekelezwa katika awamu zinazofuata. Kwa mfano, Rais wa Awamu ya kwanza aliahidi kujenga daraja la Mto Rufiji; kutokana na ufinyu wa Bajeti daraja hilo lilijengwa kipindi cha Awamu ya Tatu.

Aidha, ahadi ya ujenzi wa daraja la Kigamboni ilitolewa na Rais wa Awamu ya Pili, lakini ujenzi wake unafanyika sasa na Awamu ya Nne. Naomba kusisitiza kwamba utekelezaji wa ahadi, zinazoibuliwa, zinazotolewa na Mheshimiwa Rais ni sehemu ya utekelezaji wa mipango yote ya Serikali katika kuwaleta amaendeleo wananchi. Hivyo, ahadi hizo zinapotolewa hutafsiriwa katika mipango na Bajeti za kila mwaka za sekta zote za Mikoa na Wilaya.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini kitu ambacho kimedhihiri hapa ni kwamba kuwa takwimu hazipo. Sasa Serikali haioni kuwa kuna wajibu wa kuweka takwimu hizo na tathmini ya ufanisi wake kuzuia mnyenyo wa ahadi hizo kufuatia muda?

Tunawashukuru Marais wa CCM wa Awamu Nne kwa ahadi zinazo-*supplement*, yaani zinazojazia Ilani na kuleta maendeleo makubwa. Lakini hivi sasa kuna dalili ya kuweza kuja kutolewa ahadi za kushinikiza kura zaidi badala ya maendeleo. Hata pengine kutolewa ahadi za misaada ya majengo ya imani za kidini na udhaifu wa maskini wetu. Jambo ambalo ni hatari sana. Serikali na Taasisi zake kama vile Tume ya Uchaguzi mnaliona hili na mnalishughulikiaje? Ahsante sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Umelielewa hilo swali. Mimi hapana sikulielewa. Kama umelielewa jibu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kinachokosekana hapa kwangu ni takwimu. Lakini taarifa za ahadi tunazo na miradi iliyotekelezwa tunayo.

Lakini kwa sababu yeye alitaka takwimu za fedha hizo ndiyo nimesema ni ngumu kuzijua. Lakini tunazo, tunajua ahadi ndiyo maana nimetoa mfano ahadi ya Rais ya Awamu ya Kwanza daraja la Rufiji ambayo limejengwa na Rais wa Awamu ya Tatu na ahadi ya Rais wa Awamu ya Pili iliyotekelezwa sasa ya Kigamboni na Rais wa Awamu ya Nne. Ahadi na miradi iliyotekelezwa tunayo ila hizo takwimu za shilingi ngapi ndiyo imekuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nadhani unataka kuhusisha mambo ya siasa na ahadi zinazotolewa sasa za kidini sijui kama nimekuelewa. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba ahadi zinatolewa na wanasiasa wengi, hata sisi Waheshimiwa Wabunge tumetoa. Baadhi yetu hata sisi tumetoa hatujatekeleza zote.

Mheshimiwa Rais ametoa sasa hii ni aina fulani ya kuibuaji haiwezekani kiongozi amefika mahali, Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Rais amefika mahali watu wanakullilia nyumba imezulilwa, Mheshimiwa Mbunge hapa jana, halafu ukatoka bila kuahidi lolote. Haya ndiyo mazingira yanayomkuta kiongozi yeyote katika kuahidi, kuunga mkono katika kuibuwa miradi ambayo inatekelezwa.

Sasa utekelezaji ni suala lingine inatekelezwa namna gani? Lakini kwa Waheshimiwa Marais haya niseme utekelezaji wake unakwenda kwa Bajeti. Sasa inawezekana mtu akaenda kwenye sherehe maana Serikali haina dini ndiyo. Lakini inawezekana kiongozi mmoja akaenda kwenye madhehebu yake akaahidi kujenga msikiti au kusaidia Kanisa siwezi kujua. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UR. NA BUNGE]

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu kama ulivyoanza kusema swali la Mheshimiwa Nundu sikulielewa vizuri. Labda angelifafanua lakini kama na yeye amenielewa. Inatosha kusema tu kwamba kila mwenye kutoa ahadi analo jukumu la kusimamia utekelezaji wake.

Na. 68

Mahusiano ya Vyama vya Siasa Nchini

MHE. ALLY M. KEISSY (K.n.y. MHE. MWIGULU L. N. MADELU) aliuliza:-

Msingi wa mahusiano ya Vyama vya Siasa huwa ni malengo ya pamoja na imani moja:-

(a) Je, Serikali ilishawahi kufanya uchunguzi kujua ni nini mahusiano yaliyopo kati ya baadhi ya Vyama vya Siasa Tanzania?

(b) Je, mahusiano hayo yana manufaa/nia njema kwa Tanzania?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawahi kufanya uchunguzi kuhusu uhusiano uliyopo kati ya baadhi ya Vyama vya Siasa nchini kwa vile vyama vilivyopo vimesajiliwa na vinaratibiwa kwa Mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya Mwaka 1992. Kwa mujibu wa Sheria hivyo, vifungu vya 11(a)(b) vinaruhusu Vyama vya Siasa kuingia makubaliano ya kuungana na kuunda chama kipya cha siasa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UR. NA BUNGE]

Katika mazingira hayo, vyama vya awali vinavyokuwa vimepoteza sifa za kuwepo kwake yaani vinakufa. Hata hivyo, tangu kutungwa kwa Sheria hii, hakuna Vyama vya Siasa vilivyowahi kuungana kwa malengo ya kisiasa na kuwa na imani moja.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Vyama vya Siasa vimewahi kuwa na makubaliano yasiyo rasmi kisheria kama mkakati wa kutafuta kuungwa mkono na wapiga kura nyakati za uchaguzi.

Serikali haiwezi kutamka kwa hakika ni kwa kiasi gani uhusiano na makubaliano ya aina hiyo yameweza kuwa na manufaa kwa Tanzania. Hata hivyo, mfumo wa vyama vingi nchini umekuwa chachu katika kukuza demokrasia na uhuru wa mawazo na kujieleza licha ya kasoro zilizopo.

MHE. ALLY M. KEISSY: Mheshimiwa Spika, swali dogo tu la nyongeza. Hivi Vyama vya Siasa Tanzania vimekuwa vingi sana kuliko nchi zote ulimwenguni labda *DRC* ndiyo inazidi.

Je, kuna mpango gani wa Serikali kuviangalia upya vyama siyo kusajili sajili tu kila mtu anakuja na chama chake inakuwa kama Vyama vya ukoo? (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Kwamba tumezidi, hapana mimi nimetoka nchi moja Namibia watu chini ya milioni moja na kitu wana Vyama zaidi ya 50. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama ulivyotangulia kusema sisi tuna Vyama 21, lakini kwa takwimu tulizonazo si vingi ukilinganisha vilivyopo katika nchi mbalimbali. Zipo nchi nyingi tu kama India zina vyama vingi sana vya Majimbo, vya Kitaifa na zipo nchi nyingi ambazo zinazidi maradufu kwa vyama vyetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UR. NA BUNGE]

Lakini hicho alichokisema kama vipo vyama ambavyo vinaandikishwa kiukoo, hivi tungevijua. Kwa kweli hakuna sifa ya kiukoo inayoruhusu kusajili. Sifa zinazoruhusu chama kusajiliwa zimeainishwa kwa mujibu wa Sheria na bila shaka Msajili anatekeleza Usajili wake kwa Mujibu wa Sheria hiyo.

SPIKA: Ahsante sana tunaendelea na swali linalofuata, mmeliogopa swali hilo?

Na. 69

Mji Wa Katoro Kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo

MHE. LOLESIA JEREMIA BUKWIMBA aliluliza:-

Taratibu zote za uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Katoro ulioko Wilaya ya Geita zimekamilika katika Ngazi za Halmashauri na Mkoa:-

Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katoro utanzishwa rasmi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI imepokea taarifa ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katoro tarehe 27 Agosti, 2013 kupitia barua yake yenye Kumb. Na. *GDC/L/20/18/5*. Taarifa hiyo inaonyesha kuwa mapendekezo hayo yamepitishwa katika kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kamati (*WDC*), Baraza la Madiwani na Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*).

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi uliofanyika, mapendekezo hayo yameonekana kuwa hayajapitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji pamoja na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC). Hivyo, taratibu hizi zote ambazo ziko kisheria zikikamilika, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itayafanyia kazi maombi haya pamoja na maombi mengi yatakayokuwa yamewasilishwa kutoka maeneo mengine.

Aidha kabla ya kuanzisha mamlaka hiyo, Ofisi hii itatuma wataalam kwa ajili ya kuhakiki vigezo vinavyozingatiwa katika uazishaji wa Mamlaka za Miji Mdogo.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri katika jibu lake ameonyesha kwamba kuna baadhi ya vitu muhimu Mihutasari haipo. Lakini mimi kwa vile natoka kule ninajua kabisa kwamba vikao vyote vilifanyika na mihutasari yote ipo. Sasa ningependa kujua kwamba je, mihutasari hii ikiletwa ni lini sasa uanzishwaji wa Mji Mdogo wa Katoro utaanzishwa?

Lakini vilevile kuanzishwa kwa Mji Mdogo kunaambatana na huduma mbalimbali muhimu kama huduma za maji, barabara na kadhalika. Sasa ningependa kujua kipindi hiki ambacho Serikali inashughulikia taratibu za kuanzisha Mji huu.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi katika kuwapa huduma muhimu kama maji, barabara katika Mji wa Katoro? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza kama ananihakikishia mikutano yote ilikaa na mihutasari ipo, ningemwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ni Mbunge wa kule aniletee na mimi nitamhakikishia kwamba tutalifanyia kazi ili Mamlaka ya Mji Mdogo iweze kuanza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la barabara na maji kwa kuwa huu mji upo katika Halmashauri ya Geita. Ninachoomba tu kwamba waweke katika bajeti yao ya mwaka 2014/2015 na ile miradi ambayo ipo basi itekelezwe kwa ajili ya maandalizi ya kuwa na Mji Mdogo wa Katoro.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ilishapitisha kwamba Kibiti kunafaa kabisa kuwa Mji Mdogo na taratibu zote zilifuatwa kuanzia ngazi ya vijiji, kata, Wilaya, Mkoa na tulishaleta maombi yetu kwa muda mrefu Serikali.

Je, Serikali itatangaza lini sasa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibiti?

SPIKA: Kwani hili swali lilikuwa la Kibiti hili! *Anyway* Mheshimiwa Waziri unajua kujibu jibu maswali ambayo siyo yenyewe.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kama ananihakikishia kwamba taratibu zote zimefanyika na zimefika Ofisi kwangu.

Napenda nimhakikishie kwamba tutakavyomaliza kupitia na kujiridhisha kwamba taratibu na vigezo vyote vimefuatwa Mji huo utatangazwa.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi naomba nimwulize Waziri Mji wa Mombo Mkoani Tanga ni Mji Mdogo kwa muda mrefu na hatua za kuomba kuwa Halmashauri ya Mji zilishapelekwa muda mrefu na vikao vyote vilishafanyika na Mkoa ulishapeleka Wizarani.

Je, ni lini mtatupa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji wa Mombo?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Swali jipya, lakini kwa sababu Waziri atasema, hata mimi ningeweza kujibu sasa hivi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mary Mheshimiwa Chatanda na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameleta maombi ya kuwa na Miji Mdogo katika maeneo yao. Ni kwamba maombi yafika Ofisini kwetu tunayafanyia kazi, vigezo vikifikiwa basi tutangaza kuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo.

SPIKA: Ninaomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

Na. 70

Zoezi la Upandaji Miti Jimbo la Manyovu

MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA aliuliza:-

Jimbo la Manyovu lina eneo kubwa ambalo linahitaji kupandwa miti aina mbalimbali:-

Je, Serikali ina mpango gani unaotekelezeka kwa zoezi la upandaji miti Jimboni humo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI]

Mheshimiwa Spika, Upandaji wa miti katika kila Halmashauri unazingatia Mpango wa Kitaifa unaozitaka Halmashauri zote nchini kupanda miti isiyopungua 2,000,000 kila mwaka. Kuanzia mwaka 2008 hadi 2013, jumla ya miti ya aina mbalimbali 2,137,860 lipandwa katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Manyovu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe katika Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 imepanga kutenga shilingi milioni 12 kwa ajili ya upandaji wa miti isiyopungua milioni 2. Uoteshaji na upandaji wa miti hiyo unafanyika kwa kushirikisha vikundi watu binafsi Taasisi mbalimbali kama wakala wa huduma za misitu na asasi zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuzikumbusha Halmashauri zote kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mpango wa upandaji miti ili kuleta ufanisi.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru Mheshimiwa Waziri umesema vizuri kabisa kwamba ni sera ya Halmashauri kwamba zipande miti milioni mbili kila mwaka.

Lakini imeonyesha kwamba kuanzia 2008, mpaka 2013 miaka saba iliyopita Jimbo langu limepandwa miti milioni mbili (2), Milioni mbili mara 7 ni milioni kumi na nne. Tunao upungufu wa miti zaidi ya milioni kumi na mbili na Halmashauri yako unayo simamia wewe, imekuwa wazembe kupanda miti kwenye Jimbo langu.

Je ni hatua gani utawachukulia na adhabu gani utawapa watendaji wako kwa kutotimiza mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, la pili, milioni mbili ambayo imepandwa kuanzia miaka hiyo, ya 2014/2015. Je, inatosha kuziba pengo hilo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo, Halmashauri yetu mimi na yeye imeshindwa kutekeleza malengo yale ambayo ofisi yangu iliagiza sasa cha kufanya naomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu sisi tunaagiza wao wanatekeleza. Alirejeshe kwenye Baraza la Madiwani na wale wote waliohusika kuzembea kupanda miti inayohusika wawachukulie hatua. Wale ambao watahitaji sisi tuwachukulie hatua basi Baraza lipendekeze nini cha kuwafanyia.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la uharibifu wa mazingira sasa hivi ni janga la Kitaifa na ukizingatia kwamba sasa hivi kuna mabadiliko tabia Nchi. Kwa hiyo ubandaji unakuwa ni jambo la lazima hakuna jinsi ya kulikwepa vinginevyo itakuwa tatizo.

Sasa alichokisema Mheshimiwa Waziri, kwamba kuna agizo la kupanda miti milioni mbili kila Halmashauri ambapo kwa kweli uharibifu ni mkubwa kuliko hiyo kasi ya marekebisho. Sasa Serikali inachukua hatua gani madhubuti kuhakikisha agizo hilo linatekelezwa lakini tunaongeza kasi ya upandaji miti kwenye maeneo yaliyoharibika ahsante sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kabisa mabadiliko ya tabia Nchi sasa ni janga la Dunia na kama mmeshaona kwenye vyombo vya habari, Dunia inahangaika na sasa tumetoka Paris kulikuwa na Mkutano wa Rais wote wa Afrika, pamoja na nchi ya Ufaransa ambayo inaandaa mkutano wa 21 wa mabadiliko ya tabia Nchi. Tumeshona jinsi ambavyo nchi mbalimbali sasa hivi zinapata majanga makubwa ya mafuriko, kama China, Tonga, na kadhalika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA]

Mimi niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, ili suala tusilifanyie mzaha Serikali imeshachukua hatua na imeshaagiza miti milioni moja bado haitoshi. Tunaomba tupande miti mingi zaidi, kwa sababu wenzetu wa *Mozambique* wameshapigwa na mafuriko makubwa sana. Kenya pia imeshapa adhari hizo. Tanzania tumerukwa siyo kama sisi tunamwomba sana Mungu, ila ni kwa sababu tuna miti inayopunguza joto la Bahari.

Kwa hiyo yale mawimbi makubwa yanapokuja kuelekea kwetu yanakuta ufukwe wetu unakuwa na hali ya ubaridi kidogo. Kwa hiyo mawimbi yanahama.

Lakini, tutakapoendelea kukata miti mingi tutegee kabisa madhara waliopata Philippines, New York, na Mozambique tutayapata hivi karibuni. Kwahiyo naomba nitumie muda huu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika Halmashauri tuhakikishe hiyo miti milioni mbili inapandwa, na zaidi ikiwezekana hata milioni nne. Ahsante sana.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, amekuwa akijitahidi sana kuhimiza wananchi kupanda miti na kuzuia wakata miti haramu, kwa ajili ya kupunguza adhari za mabadiliko ya tabia Nchi, lakini pia na kulinda Rasilimali mlima Kilimanjaro.

Je, Serikali haioni kazi nzuri hii inayofanywa na huyu Mkuu wa Mkoa na ikampa msaada wa Rasilimali fedha?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, noamba kujibu swali la nyongeza kama ifuavyo. Mkoa wa Kilimanjaro, kwa sababu ya Mlima ule kuna miradi kadhaa na kuna mradi wa Kitaifa *Compact* uko chini ya Mkuu wa Mkoa. Kwa hiyo, mimi nawaomba watu wa Kilimanjaro wanaoweza kuandika miradi, waandike miradi kwa sababu tuna pesa pale za kuhifadhi Mkoa ule na Mlima Kilimanjaro.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA]

Lakini vile vile tunafanya jitihada kuomba pesa zaidi kutoka *Global Environmental Facilities* ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya kuhifadhi Mlima ule. Lakini sio mlima ule, tuhifadhi Nchi yetu kwa kupanda miti mingi zaidi. Lakini kabla hatujapata hiyo misaada sisi wenyewe pia tuna uwezo na tusimamie kwa juhudi zetu zote, tupande hiyo miti, kwa pesa chache tulizo nazo. *(Makofi)*

SPIKA: Mazingira yakiwa ni ya Serikali basi tumekwisha. Kama tutangoja Serikali na fedha zake, basi Mazingira hayatakuwepo. Naomba tuendelee na swali linalofuata. *(Makofi)*

Na. 71

Walimu Kupewa Wizara Maalum

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA (K.n.y. MHE. ESTER AMOS BULAYA) aliluliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka Wizara Maalum ambayo itashughulikia masuala ya Walimu kuliko ilivyo sasa ambapo Wallimu hawana Wizara Maalum?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niamba ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Esta Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala la walimu yanashughulikiwa na Taasisi mabambali kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambayo inashughulikia pamoja na mambo mengine Sera, Sheria, Miongozo, Taratibu, Viwango vya Elimu na Elimu ya Ualimu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI]

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, inashughulikia masuala ya kiutumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiwemo Walimu. TAMISEMI pamoja na mambo mengine huratibu uendeshaji wa elimu ya Msingi na Sekondari; Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na mambo mengine ni Waajiri wa Walimu na Idara ya Ualimu katika Tume ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kuwathibitisha walimu kazini, kuwapandisha vyeo na kuwachukulia hatua kwa utendaji usioridhisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977 Ibara 36 (1), Mheshimiwa Rais ndiye mwenye Mamlaka ya kuunda au kuvunja Taasisi na kuzipangilia majukumu kwa kadiri atakavyoona inafaa, kwa nyakati na mazingira mbalimbali na kulingana na agenda muhimu za Kitaifa zilizopo. Mheshimiwa Rais huunda Taasisi kupita Hati mbalimbali za mgawanyo wa Majukumu, Sheria, Tamko la Rais na Hati ya Rais ya Mwongozo wa Majukumu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vigezo vikuu vinavyozingatwa katika kuunda Taasisi ni pamoja na kuzingatia Katiba, mikakati ya kitaia ya muda mrefu na muda wa kati (Dira ya Taifa, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, MKUKUTA na kadhalika) Sera na Sheria mbalimbali, ilani ya Chama Tawala, jukumu linaloundiwa Taasisi kutokuingiliana na Mamlaka ya Taasisi yoyote nchini; na kuhakikisha *Checks and Balance* katika utendaji wa Taasisi mbalimbali. Kila Taasisi inayounda hulenga kuchangia katika kutekeleza malengo ya Taifa letu.

Kwa hiyo, suala la kuwa na Wizara Maalum ya kushughulikia kada moja Walimu peke yake kama inavyopendekezwa siyo moja ya kigezo katika kuunda Wizara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ALPHAXARD K.N LUGOLA: Mheshimiwa Spika, kwanza nasikitika kabisa kwamba swali la Mheshimiwa Bulaya halijaguswa na halijajibiwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, sentensi ya majibu ya mwisho anasema, kwa hiyo suala la kuwa na Wizara Maalum ya kushughulikia kada moja ya Walimu peke yake kama inavyopendekewa siyo moja ya kigezo katika kuunda Wizara. Swali linahusu Wizara maalum, swali halihusu Wizara.

Je, kwanini Mheshimiwa Waziri amechambua vigezo vya kuuunda Wizara, badala ya kuchambua vigezo vya kuanzisha Wizara Maalum.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, walimu hawa wamekuwa wakihangaika hasa kwa kutojua ni Wizara gani inayoshughulika na walimu katika Nchi yetu. Kwa kuwa TAMISEMI imejazwa Sekta nyingi za mtambuka Elimu, Maji, Mifugo, Uvuvi, Barabara, Afya inasababisha walimu hawa wasiwe na tija katika kutoa ya Elimu bora hapa Nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Wizara Maalum kwa ajili ya Walimu peke yao? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri kujibu amejibu, isipokuwa wewe hukuridhika, basi ndiyo hicho tu. Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lugola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunisaidia kujibu sehemu ya majibu ambayo nilistahili kujibu. Lakini kitu ambacho hakunisaidia Mheshimiwa Lugola hakutoa vigezo vya kuanzisha Wizara Maalum mimi nimetoa vigezo vya kuanzisha Wizara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI]

Sasa kwa nafasi yangu nimekuwa Wizara ya Utumishi ambayo inashughulikia uundaji wa miundo ya Wizara mbalimbali. Ninavifahamu vigezo vya kuanzisha Wizara. Lakini kwa bahati mbaya sifahamu vigezo vya kuanzisha Wizara Maalum na Wizara Maalum sijui inakuwaje. Kwa hiyo Mheshimiwa hakunisaidia ili niweze kumjibu. Kwahiyo kwa maana ya suala la Mheshimiwa Ester Bulaya tumelijibu. Lakini suala la Walimu kuwapeleka TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, naomba aende akazungumze na Chama cha Wafanyakazi cha Walimu, ajaribu kuzungumza na baadhi ya Walimu, yakiwemo Matatizo ya Walimu. Baada ya kuwa wamepelekwa TAMISEMI yamepungua kwa kiasi kikubwa sana. Akitaka ushahidi sasa akalinganishe walimu walioko katika Vyuo vya Ualimu na walimu ambao wapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mfano wa matatizo ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, walimu wa Shule za Msingi, ndiyo wana matatizo lakini si mengi kama wa Sekondari. Sekondari wakati tunawaridhi wakitokea Wizara ya Elimu, wengi walikuwa hawajapandishwa vyeo tangu waajiriwe, wengine walikuwa hawajathibitishwa kazini. TAMISEMI wamejitahidi kwa kiasi kikubwa wengine hata mafaili wakati wanapelekwa TAMISEMI walikuwa hawana.

Kwa hiyo naomba kabla hatujazungumza kuwasemea walimu hebu tukawaulize wenyewe, mnaridhika huko mliko? Mnaonaje mkilinganisha na kwa zamani? Msije mkawaamulia mambo ambayo wenyewe mtawakuta kwamba hamuwaridhishi. *(Makofi)*

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii niweze kumwuliza Waziri swali la nyongeza kwa niamba ya Walimu wa Tanzania. Napenda kuuliza swali. Je, Serikali inawasaidiaje Chama cha Walimu kuwatetea majukumu yake na kuweza kuwawezesha walimu kudai stahili za madai yao kama ilivyo inavyodaiwa kuyumba yumba mpaka sasa hivi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, kama ifuatavyo. Kwanza tunao utaratibu Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi wa Umma, TAMISIMI na Wizara ya Elimu ya kukutana mara kwa mara na walimu. Tuko katika mchakato wa kupanga kikao na Chama cha Walimu katika kujadili matatizo yao.

Kwa hiyo tunakutanana nao, tunawasiliana nao, na hata karibuni Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi alipanga kikao ambacho tulikuwa tunakutana na Chama cha Walimu kwa bahati mabaya mimi sikuhudhuria lakini waziri wa Elimu alikutana nao. Tunakutana nao na mimi mwenyewe katika ziara za Mikoa, mara nyingi huwa moja ya mambo yangu ninayofanya katika Ziara zangu ni kufanya kikao na watumishi ambapo ninawaacha kuwa huru, kuuliza maswali, kusema kero zao. Kwa hiyo, tunawahamasisha. Huwa tunawaambia kuwa huru sema lolote usiogope wote walioko hapa. Kwa hiyo, tunawaamasisha. Wenye kero wapeleke kwenye vyama vyao vya Walimu na Vyama vinatuletea lakini pia na wenyewe mmoja mmoja tunawasikiliza. *(Makofi)*

Na. 72

Ukaguzi wa Mazingira kwa Miradi ya Maendeleo

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Miradi yote mikubwa ya ujenzi na ya maendeleo hufanyiwa tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza kutekelezwa kwa mujibu wa sheria husika.

(a) Je, ni miradi mingapi mikubwa ya maendeleo imefanyiwa ukaguzi wa mazingira wakati wa utekelezaji wake?

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa na kurekebishwa kwa miradi isiyotekeleza Ripoti ya Tathmini ya Athari za Mazingira?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kuanzia mwaka 2008 Oktoba, mpaka 2013 miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ilikuwa imesajiliwa kwa ajili ya kuifanyia Tathimini ya athari kwa Mazingira ni 2,595 ikiwa ni pamoja na miradi ya Sekta, Majengo, Barabara, Madini, Nishati na Mengineyo. Kati ya hiyo miradi 1065 tu ndiyo iliweza kupatiwa vyeti.

Aidha, miradi 53 ilikuwa inatekelezwa bila kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira au maelekezo ya Tathimini ya Athari kwa Mazingira (*TAM*). Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutozwa faini na kuamriwa kufanya ukaguzi wa athari kwa Mazingira kwa miradi iliyoanzishwa bila kufanywa *TAM*.

(ii) Kwa miradi ambayo ilifanyiwa *TAM* na kugundulika kuwa haikuzingatia Sheria ya usimamizi wa Mazingira au maelekezo yaliyotolewa katika taarifa ya *TAM*, wamiliki walipigwa faini na kupewa amri ya kurekebisha uharibifu wa Mazingira uliotokana na shughuli zao (*Restoration Order*) kwa mujibu wa Sheria.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fulsa hii kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa katika Wilaya yetu ya Namtumbo kulikuwa na mradi, au upo mradi wa ujenzi wa Barabara na sasa hivi hauko kwenye *Restoration Stage*. Hatua ya kurekebisha uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli zao na sasa hivi tunaridhika pembeni mwa Barabara wanavyorekebisha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA]

Lakini kulikuwa na malalamiko katika maeneo ambayo walikuwa wanapasua miamba ya mawe kwa ajili ya kupata kokoto, mawe yalikuwa yanaruka kwenye mashamba ya wana vijiji na kwenye vyanzo vya maji.

Je Serikali inaweza ikambia *NEMC* kwa hatua hii wakaenda wakatizama wanavyorekebisha maeneo hayo ya miamba ya mawe ili werekebishe kama ilivyokuwa zamani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, napenda kujibu swali la nyongeza la Vita Kawawa, kama ifuatavyo ni kweli utaratibu katika kuanya *Restoration* baada ya mradi kukamilika ni kwamba wajenzi katika maeneo hayo wanapashwa warudishe hali ilivyokuwepo mwanzoni.

Kama alivyosema, tutakubaliananae kwamba tutaomba wenzetu wa *NEMC* kuona namna gani ambavyo wanaweza kuhakikisha kwamba *Restoration* inakuwa kama ambavyo inapashwa kufanyika na kama ilivyokuwa imeelezwa kwenye *Environment Impact Assessment* waliyopata. *(Makofi)*

MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, kwakuwa suala la mazingira ni suala tete na lina adhari kubwa katika Taifa letu tusipolitilia maanani na kwakuwa pamoja na kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, na Mazingira ndiyo inayoshughulikia masuala haya, lakini mwisho wa siku watendaji wakuu

MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA: Mheshimiwa Spika, Nakushukuru sana. Kwa kuwa suala la mazingira ni suala tete na lina athari kubwa kwa Taifa letu tusipolitilia maanani. Pamoja na kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais na Mazingira ndio inayoshughulikia masuala haya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA]

Lakini mwisho wa siku Watendaji Wakuu wako chini ya TAMISEMI. Ni mipango gani mikubwa ya makusudi inayo *link* pamoja na Wizara hii ambayo ndo ina watu kimsingi kuhakikisha haya mazingira yanaboresha katika maeneo mbalimbali?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa uliza swali vizuri *broad*.

NAIBU WAZIRI. OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:
Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msigwa kama ifuatavyo:-

Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004 iko wazi kabisa imezipa mamlaka za vijiji za Kata za Wilaya na Mikoa kuhakikisha kwamba zinashughulikia Mazingira. Ofisi ya Makamu wa Rais, inabaki kuwa *coordinator* na kuhakikisha kwamba Sheria zinafuatwa kwa kutumia *NEMC*.

Kwa hivyo, nimhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Vikao vya Halmashauri agenda ya Mazingira iwe kama ni agenda ya kudumu ili kuhakikisha kwamba miradi yote inayotekelezwa inahakikisha na kuhakikisha kwamba Mazingira yetu hayaharibiwi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Moses Machali, swali la nyongeza.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimwulize swali moja dogo la nyongeza. Wananchi wa Jimbo la Kasuli Mjini katika vijiji kama vya Msambala, wanamlalamikia aliyekuwa Mkurugenzi wa Bonde la Ziwa Tanganyika ambao waliokuwa waratibu suala zima la Uhifadhi wa Mazingira. Wananchi hawa walipewa kazi waandae vitalu vya miti ili kusudi waweze kuviuza, lakini walichukuliwa miti yao halafu hawajalipwa fedha zao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOSES J. MACHALI]

Je, Wizara yako iko tayari kuweza kushughulikia tatizo hili na pengine wale waliohusika kuwatapeli wananchi hawa wanachukuliwa hatua za kinidhamu?

SPIKA: Mheshimiwa Moses Machali umetenda haki kwa swali hili? Haujatenda haki, yaani yeye aanze kujua nani alichukuwa hela? Mheshimiwa Waziri labda alipita huko alikutana na hilo suala la vitalu. *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli Ziwa Tanganyika linahifadhiwa na *Lake Tanganyika Authority* ambapo ni mradi kati ya nchi nne: Burundi, Kongo *DRC*, Zambia pamoja na Tanzania na kuna pesa zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi pamoja na Wananchi wanaozunguka Ziwa hilo.

Hatua tumeisha chukuwa tulikuwa na Meneja wa Mradi upande wa Tanzania ambaye hakufanya vizuri tumemfukuza kazi, na tumemuweka mwingine. Lakini niseme tu kwamba Halmashauri ndizo zinatakiwa kusimamia.

Kwa hiyo, kama kuna matatizo tunaomba hizo Halmashauri zenye hao watu, kwa sababu miradi hiyo inasimamiwa na Maafisa walio chini ya Halmashauri. Kwa hiyo, tunaomba mchukue hatua mathubuti sisi kwa upande wetu tumeisha chukua hatua na Meneja wa Mradi huo tumeshamfukuza kazi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Mifungo na Uvuvi, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, atauliza swali linalofuata.

Na. 73

Uonevu na Unyanyasaji kwa Wafugaji Kwimba

MHE. LETICIA M. NYERERE aliuliza:-

Matukio ya uonevu na unyanyasaji wa wafugaji katika Jimbo la Kwimba na nchini kote yamezidi kuongezeka:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na tatizo hili?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa pole kwa wafugaji ambao waliathirika na vitendo vya uonevu na unyanyasaji kutokana na operesheni mbalimbali za kuhamisha wafugaji kutoka eneo moja kwenda eneo jingine ili kupisha shughuli zingine za kiuchumi na uhifadhi. Malalamiko mengi hapa nchini yanayojitokeza juu ya uonevu na unyanyasaji wa wafugaji yamekuwa ya kiripotiwa wakati wa zoezi la kuhamisha mifugo hiyo.

Serikali imekuwa ikichukuwa hatua mbalimbali kupunguza uwezekano wa kutokea uonevu wa aina yeyote na unyanyasaji wa wafugaji wa kudhibiti vitendo vya watendaji wa Serikali ambao wanajihusisha na unyanyasaji wa wafugaji na kuwachukulia hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, Katika kuendeleza Sekta ya Mifugo wilaya ya Kwimba, Halmashauri ya Kwimba kupitia programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2012/2013 imeboresha huduma za mifugo kwa kutekeleza miradi ifuatayo: Ukarabati wa malambo 1, ujenzi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]

wa malambo viwili 2.Ujenzi wa Visima virefu vya maji vinane na ujenzi wa visima virefu viwili.

Mheshimiwa Spika, aidha miradi mingine iliyotekelezwa katika kipindi hicho ni ukarabati wa majosho sita, ujenzi wa majosho matatu, chanjo ya ng'ombe dhidi ya homa ya mapafu, ambapo jumla ya ng'ombe 63,587 walichanjwa na mbwa 855 walichanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa. Serikali kwa upande wake itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya nchini, kuwajengea uwezo wafugaji ili kuongeza tija katika wafugaji na kuleta hali ya utengamano. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Leticia majibu swali la nyongeza.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ungwana wake wa kukiri uharibifu na uonevu uliofanywa kwa wafugaji wa Kwimba.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda Kwimba kufanya tathmini ya uharibifu huo, ili Serikali iwalipe fidia Wafugaji wa Kwimba?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kutokana na ukosefu wa dawa za majosho, ng'ombe na mifugo ya Kwimba imekuwa ikioshwa bila kutumia dawa. Kwa kuwa kuwaosha ng'ombe hao bila matumizi ya dawa ni sawasawa kabisa na kama Mheshimiwa Waziri ataoga bila sabuni, madhara ni yale yale yanayojitokeza kwa ng'ombe pia na Mheshimiwa Waziri anaweza akapata madhara hayo hayo. Je, Serikali inatoa kauli gani?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]

Kwanza pole niliyoitoa sio kwa Wilaya ya Kwimba peke yake, ni kwamba hatujapokea Taarifa rasmi za Wilaya ya Kwimba kuhusiana na uonevu wowote.

Lakini pole niliyoitoa ni opereshini kwa ujumla ambazo zimefanyika katika maeneo mbali mbali hapa nchini. Kwa hiyo, lakini kwenda kutembelea wananchi wafugaji katika kuangalia yaliyokuwa ya naendelea niko tayari kwenda huko kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Swali lake la pili linahusu dawa za majosho. Nidhahiri kwamba Serikali haiwezi ikatoa dawa za majosho kwa mifugo yote nchi nzima. Kwa hiyo, ni muhimu Halmashauri zielewe kwamba inapotokea kwamba kuna aina ya kupe ambao wanaathiri mifugo ya Halmashauri hiyo, kwa sababu kupe hizi zina tofautiana eneo moja kwenda eneo jingine. Basi wafanye bidii na kuelimisha wananchi. Wafugaji wenyewe wagharamikie.

Lakini sisi kama Serikali tuna ruzuku ambayo tunaitoa kila mwaka ya dawa za kuogeshea mifugo haitoshi, lakini angalau hicho kidogo ambacho kipo kutokana na upatikanaji wa fedha kitaendelea kupelekwa Wilayani ikiwemo Wilaya ya Kwimba.

SPIKA: Mheshimiwa Ndassa, swali la nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naomba niipongeze sana Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini nilikuwa naomba niulize. Hivi uonevu, unyanyasaji unao tamkwa na majibu ya Serikali, kwamba Serikali imetoa chanjo kwa ng'ombe zilizotajwa lakini majosho na kadhaalika. Je, huo ni unyanyasaji au ni uonevu?

SPIKA: Umelielewa swali? Tunaomba urudie hilo swali mimi sikuelewa pia.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, kwenye majibu ya Msingi ya Mheshimiwa Waziri. Serikali imesema kwamba imetoa chanjo kwa mifugo kutoka Wilaya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

ya Kwimba, ng'ombe, mbwa na kadhalika. Mwenye swali anasema kuna uonevu na unyanyasaji wa Wakulima katika Jimbo la Kwimba.

Je, mimi nauliza hivi kuogesha mifugo kujenga mabwawa, chanjo huo ni uonevu? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI::

Mheshimiwa Spika, kimsingi Mheshimiwa Ndassa alikuwa ananisaidia kujibu swali kwa mwuliza swali la msingi, kwamba Serikali imekuwa inajali sana wafugaji pamoja na wafugaji wa Kwimba, kwamba tumeweka miundombinu mbalimbali kwa maana hiyo hayo yote tuliyoyafanya ni kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji.

Ingekuwa inania ya kuwanyanyasa hata majosho, malambo, na chanjo zote zisingepelekwa katika Wilaya hiyo ya Kwimba.

SPIKA: Aah! hayo si mnaelewa wenyewe tuendelee. Tuendelee na swali lingine Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Maryamu Salum Msabaha.

Na. 74

Kujenga VETA Kwenye Vikosi vya JKT

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA aliuliza:-

Vikosi vya JKT huchukua vijana kwa ajili ya mafunzo mbalimbali.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni vema kujenga vyuo vya VETA kwenye Kambi hizo ili kijana wanaohitimu waweze kujajiri wenyewe?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Maryam Msabaha, anapolitaja neno *VETA* ana maanisha vyyo vinavyoendesha mafunzo ya ufundi, basi Jeshi la kujenga Taifa lina Vyyo sita vya aina hiyo. Vyyo ni 831 KJ Mgulani, 834 KJ Makutopora, 843 KJ Nachingwea, 842 KJ Mlale, 835 KJ Mgambo na 838 KJ Maramba. Hata hivyo Wizara yangu inakiri kuwa vyyo hivi ni vichache sana na havina vifaa vya kutosha vya kufanyia mazoezi ya vitendo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kutafuta fedha ili tuweze kununua vifaa vipya. Vile vile Wizara yangu ina mpango wa kujenga Vyyo vinne vya ufundi katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Mbeya Arusha ili kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi kwa vijana. Kwa kuwa Wizara yangu inakabiliwa na ufinyu wa Bajeti, Wizara ya Ulinzi ina mpango wa kutumia fedha zinazotokana kwa mapato yanayokusanywa na Shirika la Uzalishaji Mali SUMA ili kutekeleza azma hii kadiri inavyowezekana.

Kwa msingi huo basi Wizara yangu inaiona hoja ya kujenga vyyo vingi zaidi vya ufundi katika makambi ya Jeshi la kujenga Taifa kama ni suala muhimu.

SPIKA: Mheshimiwa Maryamu Msabaha Maswali ya nyongeza.

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Spika, Ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watendaji wote, wamekuwa mstari wa mbele kupigania maslahi ya Jeshi. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARYAMU S. MSABAHA]

Kwa kuwa Mafunzo ya JKT ni mafunzo ya silaha nzito na silaha nyepesi.

Je, Serikali hamwoni sasa kuna haja ya kuwafuatilia vijana wote waliopitia mafunzo ya JKT ili muwape vipaumbele kwa kuwapa ajira ili waepukane na vitimbi vya kwenda kuingizwa kwenye dibwi la ujambazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa JKT ni pamoja na mafunzo ya useremala hii nchi ina misitu ya kutosha. Je, hamwoni sasa kuna umuhimu wakuwapa vijana hawa wa JKT vibali vya kupasua mbao ili ujenge madawati ili wanafunzi wetu waepukane kukaa chini?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryamu Salum Msabaha, kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli vijana wetu wa Jeshi la kujenga Taifa wanafundishwa silaha na kwa maana hiyo basi kama Serikali haikuwa na mipango madhubuti, vijana hao wanaweza kutumia ujuzi huo katika kufanya vitendo vya uhalifu, tunalijua hilo. Pia akashauri basi Serikali iwafuatilie vijana hawa na mimi nakubali Serikali inalo jukumu la kuwafuatilia vijana hawa na Wizara yangu itatekeleza jambo hilo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia akasema: Je, Serikali haioni haja ya kuwapatia vijana hawa ajira. Kwanza Jeshi la Ulinzi la Kujenga Taifa sisi tumeweka mipango maalum kwamba vijana wanaojiriwa katika Jeshi la Kujenga Taifa wasiajiriwe uraiani. Vijana ambao tunaowaajiri tunawaajiri moja kwa moja kwa kupitia vijana hawa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA]

Kwa lengo hilo la kuwapatia ajira lakini hata hivyo hatuwezi kutosheleza vijana wote. Nimezungumza na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri tukakubaliana kwamba Jeshi la Polisi nalo lifanye hivyo, Magereza wafanye hivyo na Zima Moto wafanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hata tukifanya hivyo bado hatuwezi kutosheleza haja ya kuajiri vijana wote. Lakini jambo la msingi ambalo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tunalifanya, nikuwapatia vijana hawa stadi za maisha. Tunawafundisha masuala ya ufundi, kilimo na ufugaji. Ili watokapotoka katika Jeshi la kujenga Taifa waweze kujitegemea. Hili la kuwapa vibali vijana waliopitia Jeshi la kujenga Taifa wakate Misitu.

Mheshimiwa Spika, mimi hii nafikiri itakuwa Sera ya Serikali zinagongana. Maana upande mmoja tunataka kutoa ajira, lakini upande mmoja lakini tunahujumu sera ya kulinda mazingira.

Sasa sijui tu kati ya mambo mawili haya. Lakini kama jambo la msingi ni kutoa ajira. Mimi nafikiri tusitoe vibali vya kukata misitu ovyo tutakuwa tunaleta madhara makubwa sana kwa nchi yetu.

Sasa mimi nafikiri jambo la msingi Serikali inayo dhima kama nilivyosema nikuanzisha vyuo vya *VETA* ndani ya Jeshi la kujenga Taifa ndani ya Wizara ya elimu. Ili vijana wengi zaidi wapatiwe maarifa na mafunzo ya ufundi ili hatimaye waweze kujajiri.

SPIKA: Mheshimiwa Muhammad Sanya, swali la nyongeza.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba vyuo hivi ni viidogo na hawana vifaa vya kufanyia kazi kivitendo na kwa kuwa SUMA JKT walipewa kupitia Wizara hii mkopo wa zaidi ya dola milioni 20 wa matrekta kutoka India na kwa vile matrekta haya asilimia 80 yameishauzwa na mkopo wenyewe ni wa nafuu na wa uda mrefu.

Je, haioni Wizara kwa wakati huu kwa vile walishauza sehemu ya matrekta kutumia asilimia fulani ya fedha hizo zilizokwisha rudi katika Wizara kununulia vifaa na kuongeza vyuo hivi, ili kuleta tija wakati wao wanalipa kidogo kidogo kwa Serikali ya India mkopo wa zaidi ya dola milioni 20?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, kama ifuatavyo:-

Mimi sina tatizo na ushauri wake. Ni kweli kama anavyosema lakini naomba nisahihishe sio matrekta yenye thamani ya dola milioni 20, ilikuwa ni milioni 40. Ni kweli tumeuza matrekta na fedha zinaendelea kukusanywa kutoka kwa wakopaji, sasa sina tatizo na wazo la kutumia fedha hizo lakini tatizo langu tu ni kwamba, iko dhana imejengeka miongoni mwa Watanzania kwamba mkopo ni nusu ya bure. Mimi nataka watu wetu wajenge utamaduni wanapokopa walipe sasa tukianza utaratibu huo kwamba tunakopa tunakusanya fedha halafu tuzitumie. Mimi nafikiri ushauri wako ni mzuri, lakini pia tutumie busara mimi nafikiri Wizara yangu itakaa na kulifikiria jambo hili tukiona kwamba busara ipo tutafanya hivyo.

Tukidhani kwamba tufanye tofauti basi tutafanya hivyo. Lakini dhamira na nia bado tunayo ya kuhakikisha kwamba tunatafuta vifaa kwa kadiri inavyowezekana ili vijana wetu wapate uwezo na fursa ya kufanya mazoezi ya vitendo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante sana, tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Captain John Komba.

Na. 75

Fidia kwa Tanzania Kusaidia Kumwondoa Idd Amini

MHE. CAPT. JOHN DAMIANO KOMBA aliluliza:-

Tanzania ilisaidia sana Uganda katika vita vya kumwondoa Idd Amini Dada wa Uganda na hivyo kumfanya Rais Museven kutawala kwa amani nchi hiyo na kwa sasa Rais Museven anashirikiana na Rwanda kuihama bandari ya Dar es salaam na kuanza kutumia Bandari ya Mombasa, Kenya:-

Je, kwa nini Tanzania isidai fidia Serikali ya Uganda kulipa madai ya vita vya Uganda?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Captain John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilipigana vita na Uganda kuanzia mwaka 1978 hadi 1979 kufuatia uvamizi uliofanywa na Nduli Iddi Amin Dada wa Uganda aliyevamia na kuikalia sehemu ya ardhi yetu katika Mkoa wa Kagera.

Kwa kuwa vita hivyo vilitokana na uvamizi wa Nduli Iddi Amin Dada, baada ya vita kumalizika mwaka 1979 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliitaka Serikali ya Uganda kuilipa fidia Tanzania. Serikali ilikubali wazo hilo ya kuilipa Tanzania fidia hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA]

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Serikali ya Uganda haikutekeleza makubaliano ya mwaka 1979 ya kuilipa Tanzania fidia. Kwa hivyo, Serikali ya tatu ya Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ilifanya tena majadiliano na Uganda. Kufuatia majadiliano hayo Serikali ilitakiwa kuilipa Tanzania dola za Kimarekani dola milioni 18,441,029.91.

Mpaka sasa Uganda imeshalipa dola za Kimarekani milioni 9,656,065.35. Fedha hizi ziliwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Deni lililobaki ni dola za Kimarekani milioni 8,824,964.56.

Mheshimiwa Spika, majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda yanaendelea ili sehemu iliyobaki ya deni iweze kulipwa haraka iwezekanavyo. Wizara ya Fedha ya Tanzania inaendelea kufuatia madeni hayo kwa sababu Wizara ya Fedha ndiyo yenye jukumu hilo. *(Makofi)*

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa deni hili ni la muda mrefu na fidia ni ya muda mrefu na Serikali ya Uganda inalipa kidogo kidogo, imebaki kama nusu deni hivi na kwa kuwa Serikali ya Rwanda kuihama Bandari yetu ni kwa sababu ya Uganda, kwa nini Serikali ya Tanzania isililazimishe Uganda kutumia Bandari yetu mpaka deni hili liishe? *(Kicheko/Makofi)*

Swali la pili, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kumkumbusha Rais Museveni kwamba ilimpa hifadhi ya kisiasa, ilimpa elimu, pia amempata mke huku huku, kapata Urais huku huku, kwa nini anaendelea kutuhujumu sisi Watanzania?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA: Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya pekee na Tanzania ina bahati sana ya kuwa na viongozi wa aina ya Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mtakumbuka mwalimu aliwahi kusema Waafrika wote ni ndugu zangu na Bara la Afrika ni moja.

Kwa hiyo, halingii maanani kwa mtu kumsaidia ndugu yake jana. Lakini wanapotofautiana mawazo leo anamdai yale mambo ambayo aliyafanya nyuma. *(Makofi)*

Watanzania tunasahau haraka sana. Juzi hapa katika Bunge hili tulitoa tamko la kumuenzi Marehemu Mzee wetu Mandela, tukasema Mandela ni mtu wa ajabu sana, anastahama ya juu sana, anasamehe.

Sasa sisi Watanzania leo, jana tumemsifu mtu kwa kusamehe, leo Watanzania hao hao wanataka kulipiza kisasi. Mimi aah mimi nasema tu tuwalazimishe Uganda kutumia Bandari ya Dar es Salaam, kweli tumewasaidia, lakini tuliwasaidia kwa kuamini kwa misingi ya utu na ubindamu na kujenga umoja wa Bara la Afrika. *(Makofi)*

Tanzania ina historia katika dunia ya kuheshimika sana popote ambapo dunia inakabiliwa na matatizo, basi busara ya kidiplomasia Tanzania imekuwa ikitafutwa miaka yote na uongozi wa Tanzania umekuwa ukitafutwa miaka yote.

Mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Watanzania tuendeleo kulinda rekodi katika medani ya kidiplomasia, katika medani ya uongozi. Kweli kuna tatizo. Lakini nadhani tatizo hili litamalizwa kwa mazungumzo na litamalizwa kwa Tanzania kutoa uongozi unaostahiki na tutakumbuka wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipolihutubia Bunge aliyaeleza haya. Mimi nafikiri ni vizuri tufuate ushauri wa viongozi wetu. *(Makofi)*

Na. 76

Kiwanda cha Kusindika Chai Korogwe

MHE. ANNE K. MALECELA (K.n.y. MHE. STEPHEN H. NGONYANI) aliuliza:-

Katika Tarafa ya Bungu Kata ya Mpale, Dindira na Bungu zina wakulima wengi wa Chai na mara zote huhangaika kutafuta soko la Chai wanayolima na pia wananchi walitoa eneo la Saikare ili kujenga kiwanda cha Chai ili kupata soko la chai.

Je, Serikali itawajengea lini kiwanda hicho ili Wakulima hao wapate mahali pa kuuza mazao yao?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Tarafa ya Bungu Kata za Mpale, Dindira na Bungu yenyewe zina wakulima wengi wanaolima chai. Tatizo kubwa waliionalo ni kukosa mahali pa kuuza chai, soko la chai pamoja na kutaka kujengewa kiwanda cha chai ili wakulima wapate mahali pa kuuza chai yao inayozalishwa katika Tarafa yao ya Bungu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wanakijiji walishatoa eneo la Sakale lenye zaidi ya hekta 1,500 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha wakulima wadogo wa chai kupitia chama chao cha *Tea Growers Cooperative Society*. Juhudi za ujenzi wa kiwanda katika eneo hilo lilishindikana kwa sababu ya kukosa Hatimiliki ya eneo hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

Hivi sasa Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe inaendelea na utaratibu wa kupata Hatimiliki ya eneo hilo. Hatimiliki hiyo itakapopatikana itakuwa chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe tayari kuwavutia wawekezaji wa ujenzi wa kiwanda cha Chai.

Mheshimiwa Spika, nashauri wakulima hao hivi sasa wauze chai yao katika kiwanda cha chai cha Dindira ambacho kina uwezo wa kusindika tani 30 za majani mabichi ya chai kwa siku. Kiwanda hiki kipo katika hatua ya mwisho za kukamilisha mtandao wa pili wa uzalisha yaani *second line of production* utakaokiwezesha kiwanda kusindika wastani wa tani 60 za chai kwa siku.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, naridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Lakini naomba nimwulizie Mheshimiwa Ngonyani maswali mawili. Kwa kuwa Serikali ilichatwaa eneo la msitu wa Sakare kuwa chini ya Halmashauri ya Korogwe.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kujenga kile mahala hapa badala ya kusumbuka na kungoja Hatimiliki ili kuwaondolea wananchi adha ya kuwa maskini bila ya sababu?

Swali la pili Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa kiwanda cha Mponde ambacho kipo kwenye Jimbo la Bumbuli, Jimbo la Mheshimiwa January, kilifungwa kwa sababu ya migogoro ya wakulima wa chai.

Je, Serikali haioni kwamba ni vyema sasa ikasaidia kwenda kuangalia mgogoro ule na kuutatua mgogoro ule ili kiwanda kile kifunguliwe kiweze kuwasaidia wananchi wa sehemu ile pamoja na wananchi wa Tarafa ya Bungu kuuza chai yao pale kuliko ambavyo kiwanda kile kinaendelea kufungwa na wananchi wanateseka? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya kuwatetea wananchi wake ili waweze kupata maeneo ya kuuza Chai yao na ili waweze kupa kiwanda.

Mheshimiwa Spika, nikianza na swali hili la kwanza au la pili ambalo anasema kwamba kuna kiwanda cha Mponde ambacho kingeweza kuwasaidia wakulima wa Tarafa ya Bungu.

Naomba tu nieleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kiwanda hiki kipya cha Mponde hivi sasa kina mgogoro mkubwa sana ambao upo kati ya wakulima wanachama wa chai kule Korogwe pamoja na wale wa Lushoto ambao mgogoro huu sasa umefikia sehemu kubwa sana na Waziri mwenye dhamana ya zao hili la chai ambaye ni Waziri wa Kilimo na Ushirika hivi sasa alishaingilia mgogoro huu na amechukua hatua ya kuandika barua kwa Waziri Mkuu ili kupata suluhu ya mgogoro huu.

Sasa ningependa tu nishauri kwamba baada ya mgogoro huu kusuluhishwa na Waziri Mkuu itakuwa vyema wananchi wa Tarafa ya Bungu na Kata zake zote waweze kupata fursa ya kuweza kutumia kiwanda hiki cha Mponde kwa shughuli ya kuuza chai yao.

Na lile pili kusema kwamba kuna eneo ambalo limeshapatikana kule eneo la Sakare waweze kujenga kiwanda. Ningemshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu ambazo zinatumiwa sasa hivi ni kushirikiana na Halmashauri pamoja na Wizara yangu tuweze kuangalia kama eneo hilo litafaa na itakidhi katika kuendeleza kujenga kiwanda cha Chai kwa kule kwenye Tarafa ya Bungu na kama itakidhi basi Halmashauri pamoja na mimi tushirikiane kuhamasisha tupate wawekezaji ambao wataweza kusaidia kupata kiwanda cha Chai hapo Bungu. *(Makofi)*

Na. 77

**Tatizo la Ukatikaji wa Umeme Mara kwa
Mara Dar es Salaam**

MHE. MARIAM KISANGI (K.n.y. ABBAS Z. MTEMVU)
aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Jimboni Temeke na maeneo yote ya Jiji la Dar es Salaam kumekuwa na ukatikaji wa mara kwa mara wa umeme tena bila taarifa maalum kutolewa mapema:-

Je, Serikali inaweza kuwaambia wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kuna tatizo gani linaloendelea?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa zinazosababisha kukatika kwa mara kwa mara umeme katika Jiji la Dar es Salaam ni zifuatazo:-

- (i) Uchakavu wa miundombinu ya kusambaza umeme;
- (ii) Uwezo mdogo wa vituo vya kusambaza umeme vya Kurasini, Mbagala, Ilala na Kigamboni; na
- (iii) Kuongezeka kwa kasi kwa mahitaji ya umeme ikilinganishwa na uwezo wa kimiundombinu uliyopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la umeme la *TANESCO* imechukua hatua zifuatazo ili kuondoa kero hiyo. Kwanza, tumekarabati na kupanua vituo vya kupozea umeme kwa kufunga transfoma kubwa ili kuongeza uwezo katika vituo vifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

Mbagala, *Oysterbay, City Centre, Kariakoo, Bunguruni, Gongolamboto, Kigamboni na Mbezi Beach*. Kukamilika kwa kazi hii kumepunguza sana tatizo la kukatikakatika umeme Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa uko mradi mkubwa unaoendelea kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam, wa *Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)* ambao utakapokamilika utaboresha huduma ya umeme Dar es Salaam. Mradi huu unahusisha ujenzi wa kilomita 51.7 za njia ya msongo wa kilovoti 135 kuanzia Ubungo kwenda Kurasini, Mbagala, Kipawa hadi Gongo la Mboto. Aidha, vituo vya kupozea umeme vyenye uwezo wa *MVA 50,132* kwa *33 KV* vitajengwa katika maeneo ya Gongo la Mboto, Mbagala na Kurasini. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* pia inajenga kituo kipya cha kusambaza umeme eneo la Kisutu chini ya ufadhili wa Serikali ya Finland. Kituo hiki kitakapokea umeme kutoka Ilala na Makumbusho kupitia *under ground cable* na kuusambaza.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mbunge kwamba tatizo la kukatika katika umeme katika Jiji la Dar es Salaam linaendelea kupungua na kwamba miradi niliyoitaja hapo juu ikikamilika tatizo hilo litakwisha kabisa.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri pamoja na mikakati ya Serikali ambayo inajitahidi sana katika kulitatua suala la umeme Jijini Dar es Salaam, ninayo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la kukatikakatika umeme katika Jimbo la Temeke na Mkoa mzima wa Dar es Salaam linaendelea kuwa kubwa na linaleta athari kubwa kwa wananchi kuunguziwa vifaa vyao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARIAM N. KISANGI]

Je, Serikali inasema nini maana umeme huu unakatika sekunde unarudi, unakatika hali ambayo kweli ni uharibifu wa miundombinu au kuna tatizo lingine?

La pili, kwa kuwa tatizo la umeme Dar es Salaam kama ilivyoainisha Serikali ni pamoja na uongezeko wa mahitaji na ni kweli Jiji la Dar es Salaam linajengwa majumba makubwa kila kunapokucha, viwanda vingi.

Je, Serikali iko tayari kupanga mikakati hii na Halmashauri husika ambazo zinatoa vibali vya ujenzi huo, ili kujua mipango au uwezekano wa kubatikana umeme na uendelezwaji wa mji huu kuhakikisha vinakwenda sambamba?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, lakini kwanza lazima tuelewe kwamba *TANESCO* ya leo ilianza mwaka 1964 na toka wakati huo miundombuni mingi hatukufanya maboresho na zaidi ya hapo *TANESCO* ya mwaka 1964 ilirithi miundombinu za ukoloni *TANESCO* iliyokuwepo wakati huo ilianzishwa mwaka 1934.

Kwa hiyo ndugu Watanzania na Waheshimiwa Wabunge mnaonikiliza suala la kuboresha miundombinu ni la lazima. Sasa kwa upande wa Dar es Salaam hatuhitaji kukakaa na Halmashauri. Sisi wenyewe tuna uwezo na kuna miradi, siyo mipango, kuna miradi. Ni kwamba toka uhuru mpaka wakati huu Dar es Salaam ilikuwa na *sub-station 5* peke yake za kupozea yaani uhuru tulikuwa watu milioni 9.

Sasa hivi watu milioni 9 na umeme ulikuwa unatoka Dar es Salaam ndiyo ulikuwa unaenda sehemu zingine za Tanzania. Dar es Salaam ina watu karibu milioni nne au milioni tano. Tunachokifanya ni kwamba *sub-station* zile tano, tunajenga zingine kubwa tano na hizi kubwa tano zinazojengwa zitakamilika Septemba mwakani. (*Makofi*)

Kingine ambacho tunachokifanya tunajenga *sub-station* zingine ndogo ndogo kumi na tano kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam na kingine ambacho tunakifanya tunaachana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

na mtindo ule ambao hitilafu ikitokea magari ya *TANESCO* yanazunguka karibu yanagongana na magari ya watu wengine. Tunaweka taratibu za kutumia *system* ambayo hitilafu ikitokea hapo hapo inajulikana kwamba hii ni hitilafu ya Mbagala.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tukubali kwamba miundombinu ya mwaka 1964 ni lazima iboreshwe na katika kuboreshwa ni lazima matatizo yakatokea. (*Makofi*)

SPIKA: Haya ahsante. Tuendeleo na Wizara ya Maji, angalieni na saa pia nina maswali matano kwa dakika 10, haiwezekani. Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo.

Na. 78

Tatizo Kubwa la Maji Tarafa ya Chole na Maneromango

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Tarafa ya Chole na Maneromango zinakabiliwa na tatizo kubwa la maji, licha ya mradi wa Benki ya Dunia kuchimba visima kijiji cha Chole, Kwala, Vikumburu na Boga, bila mafanikio:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Tarafa za Chole na Maneromango zinapatiwa maji ama kutoka Bwawa la Zumbi au kutoka Mto Rufiji ili kutatua kabisa matatizo ya maji kwenye maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bwawa la Zumbi na Mto Rufiji ni kati ya vyanzo vya maji vinavyoweza kutumika katika Tarafa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

za Chole na Maneromango zilizopo katika Halmashauri ya Kisarawe. Serikali itaangalia uwezekano wa kutumia vyanzo hivi endapo itaonekana vyanzo vya maji vilivyopo havitoshelezi mahitaji.

Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa vijiji 10 katika vijiji vya Boga, Vikumburu, Kwala, Msanga, Kihare na Chole vilivyopo Tarafa za Chole na Maneromango katika Halmashauri ya Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa ujenzi wa miundombinu ya maji unaendelea katika Vijiji vya Msanga na Kihale na utakamilika mwezi Januari 2014. Utafiti wa kina umekamilika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Chole ambalo litatumika kuvipatia maji vijiji vya Chole na Kwala Kijiji cha Vikumburu kitapata maji kupitia bwawa lililopo la Vikumburu. Katika kijiji cha Boga utafiti unaendelea kwa kutafuta change kipya cha maji.

Aidha, Serikali kupitia DAWASA imechimba visima vinne katika vijiji vya Chole, Kwala, Kurui na Mtunani. Visima vya Chole, Kwala na Kurui vimepata maji na hivyo vitaendelezwa kwa kufungiwa pampuza nguvu ya jua. Pia, Serikali kupitia ufadhili wa Serikali ya China inachimba visima 30 katika Wilaya ya Kisarawe. Kati ya visima hivyo, visima 18 vinachimbwa katika vijiji vya Maneromango, Kitongamango na Mafumbi vilivyopo katika Tarafa za Chole na Maneromango.

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza nilipenda sana kuishuru Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wilaya ya Kisarawe na kusikia kilio changu cha muda mrefu katika janga la maji katika Wilaya ya Kisarawe. Lakini mie napenda kuwashukuru Shirika la *Plan International* wametusaidia Mradi mkubwa wa Shilingi Milioni mia tatu na sabini, kwa hiyo napenda kutoa shukuruni hizo za dhati.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SELEMANI S. JAFU]

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri unaona juhudi imefanyika na mimi naipongeza sana. Lakini tukiangalia hali halisi ya *Water table* ya Wilaya ya Kisarawe inachangamoto kubwa sana.

Kwa hiyo, nilitaka nipate hasa kauli ya Serikali, kwa vile chanzo cha Zumbi Bwawa la Zumbi ni chanzo muhimu sana kwa muhimu sana kwa mustakabali wa Wilaya yetu ya Kisarawe na kwa vile tuko katika *Big results now*. Je, Serikali inafanya *Commitment* gani kuamua hata ikiwezekana mwaka huu kuanza michakato wa *feasibility study* kwa ajili Bwawa la Zumbi kuipatia maji Wilaya ya Kisarawe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina Shirika la *Planning International* imefanya kazi kubwa sana ya kuipatia maji wa Kisarawe maji kwa kutumia Shilingi milioni mia tano na arobaini (540,000,000/=).

Lakini kiwango cha madini ya chuma katika maji yale ni kikubwa sana na ni wazi kwamba tumepeleka maombi haya Wizarani ione ni jinsi gani itarekebisha maji yale. Hata hivyo tuliamu

Je, Wizaru inasemaje kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kisarawe pale mjini utibu wa yale maji ili mradi wa wana Kisarawe waje kunywa maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafo kama ifuatavyo. Lakini kwa niaba ya Wizaru nichukue pongezi zake tunashukuru, na mimi niungane nae kuwashukuru *Planning International* kwa kutusaidia maji pale Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kuhusu kuiomba Serikali kuanza kufanya tathimini au *feasibility study* kwa ajili ya matumizi ya Bwawa la Zumbi ni wazo zuri lakini nilitaka Mheshimiwa Mbunge kwa sasa hivi tunaweza tusilifanye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

kwasababu tumeshafanya mpango mkubwa wa maji pale Kisarawe katika visima 55 vilivyotolewa na Serikali ya China, visima 30 tumevipeleka Kisarawe na visima karibu 18 vinachimbwa kwenye tarafa hizi mbili ambazo zina matatizo ya maji kwa hiyo tunadhani kwamba maji ni rasiliamli yetu, tuendele tuendele kutunza kile chanzo cha ziwa zumbi itakapofika wakati wake tutafanya tathmni lakini kwa sasa hivi tupate fedha tuelekeze kwenye maeneo mengine ambayo wanaitaji maji. Lakini wazo lake zuri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu madini ya chuma ni kweli yale maji pale mjini yana madini ya chuma, ambayo wananchi wanayatumia pale, na nikweli Halmashauri walileta maombi Wizarani.

Wizara yangu ilituma wataalm kwenda kufuatilia na kuangalia kama ni sahihi na baada ya kupima kwamba inerudhika kwamba ni kweli kuna madini ya chuma, sasa kazi ambayo tumeifanya ni kwamba ili kuondoa yale madini ya chuma inatakiwa yale maji ambayo yanazalishwa yapitishwe kwenye mtambo ambao yataunganishwa na hewa ya *Oxygen*.

Hewa ikiungana na yale maji iweze kuchukua yale madini ya chuma ambayo yanaweza yakawa kama kutu, kwayo hiyo kazi tumeshaanza kuifanyia kazi. Lakini la msingi ambalo tumelifanya ndiyo maana tulipeleka Shirika letu la Dawasa ili wachimbe visima na katika vile visima vinne (4) vilivyochimbwa vitatu (3) vilipata maji, yale maji ambayo yanachuma.

Kwa hiyo, wananchi waendele kutumia yale maji sasa hivi wakati tunaendelea kuangalia utaratibu wa kuwa na mtambo utakaowezesha yale maji kupitishwa pale ili yaweze kuondolewa hiyo *iron* iliyoko kwenye hayo maji. *(Makofi)*

Na. 79

Walimu Walioajiriwa Tangu Mwaka 2011-2012

MHE. DAFTARI MAUA (K.n.y. MHE. MAIDA H. ABDALLAH)
aliuliza:-

Tangu kupitishwa kwa Bajeti ya mwaka 2011/2012 ni walimu wangapi wameajiriwa hadi sasa.

Kwa mujibu wa Shule zilizopo nchini, Serikali inaweza kulieleza Bunge kiwango cha upungufu wa walimu mashuleni na kwamba upungufu huo umesababishwa na nini?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu kupitishwa Bajeti ya mwaka 2011/2012 jumla ya walimu 54,142 walijajiriwa hadi hivi sasa. Mwaka 2011/2012 jumla ya walimu 26,492 walijajiriwa wakiwemo wa Cheti 13,246 Stashahada 6,003 na Shahada 7,243. Aidha, mwaka 2012/2013 jumla ya walimu 27,650 walijajiliwa wakiwemo wa cheti 13,633, Stashahada 4,176 na Shahada 9,841.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012/2013, mahitaji ya walimu wa shule za Msingi yalikuwa 204,131. Kwa sasa, walimu waliopo ni 167,508 kwa hivyo upugufu ni walimu 36,623 sawa na asilimia 17.9 Aidha, mahitaji ya walimu shule za Sekondari ni 103,950, waliopo ni 66,820 kwa hivyo upungufu ni walimu 37,130 sawa na asilimia 35.7.

Mheshimiwa Spika, upungufu huo umesababishwa na ongezeko kubwa la shule za Msingi na Sekondari na uandikishwaji wa wanafunzi lililotokana na mafanikio ya utekelezaji wa mipango ya Elimu ya Msingi na Sekondari (MEM) na (MMES). *(Makofi)*

Na. 80

**Shule ya Sekondari ya Binga
kuwa Chuo cha Ualimu**

MHE. GAUNDENCE C. KAYOMBO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuifanya Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Mbinga (*Mbinga Day*) kuwa Chuo cha Ualimu kama ilivyokuwa awali?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1994, Serikali iliamua kuvibadilisha baadhi ya Vyuo vya Ualimu kuwa Shule za Sekondari za Kutwa, Mbinga kikiwa kimojawapo. Uamuzi huo ulifikiwa baada ya utafiti uliofanyika kubaini kuwa Vyuo hivi vilikuwa na uwezo mdogo wa kudahili wanachuo kiasi cha kutokuwa na tija.

Ili Chuo cha Ualimu kiweze kuendeshwa kwa ufanisi na tija, kinapaswa kuwa na wanachuo wasiopungua 600. Vyuo hivi vilikuwa vinadahili wanachuo chini ya 250 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Mbinga Day, ni miongoni mwa Vituo vya kutolea Mafunzo kazini, kwa walimu wa Sekondari wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Mafunzo haya yanendeshwa na Serikali kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*).

Kwa kuzingatia uwekezaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vikiwemo vifaa vya maabara na kemikali, ni vyema shule hii, iendelee kutoa huduma hii ya mafunzo kazini katika maeneo ya Mbinga.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Mheshimiwa Spika, ieleweke kwamba vyuo vya Ualimu ni vya Kitaifa. Kwa hiyo, waombaji wa mafunzo ya Ualimu kutoka Jimbo la Mbinga na Majimbo mengine wanaweza kupangwa kwenda kusoma chuo chochote cha Ualimu kutegemeana na michepuo ya masomo na nafasi zilizopo.

MHE. GAUNDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante, mara nyingi katika Bunge lako hili, Serikali imekuwa ikisema ahadi za Rais, ni amri na zitatekelezwa sasa kwa majibu haya, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kusema ahadi hizo za Rais zilikuwa za uongo? Na haziwezi kutekelezwa?

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi ya Serikali kurejea maamuzi yake. Ushirika ulivunjwa, ukarudishwa, Mamlaka za Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa zilivunjwa, baadaye zikarudishwa, hivi majuzi tu Wizara ya Elimu pia, iliweka muundo mpya wa kusahihisha mitihani yake pamoja na madaraja na mazingira ambayo yameeleweka na Mheshimiwa Waziri hapa kuhusu Sekondari ya *Mbinga Day*, wananchi wa Mbinga walikuwa wanayafahamu na ndiyo maana walimwomba Rais.

Je, yuko tayari sasa kufanya marajeo na kukubali maombi ya wananchi wa Mbinga ambayo Rais ameishayakubali?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa, rafiki yangu, Kayombo kama ifuatavyo. Moja nikiri kwamba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake wana kiu sana na Chuo cha Ualimu pale Mbinga.

Suala hili Mheshimiwa Mbunge alilihoji wakati akichangia Bajeti yangu Mwezi wa sita (6) mwaka huu, na majibu yake tuliyaweka katika kitabu ukarasa namba mia moja na mbili (132), lakini kwakutambua haja hiyo, naweza kusema kwamba mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge tutashirikiana kuangalia namna ambavyo Serikali inaweza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

ikakidhi mahitaji ya wana Mbinga. Ama ahadi ya Mheshimiwa Rais, kwa kujua kiu cha Mheshimiwa Mbunge, nilifanya mawasiliano na Ofisi ya Rais, kwa juhudi zote na kupewa uhakika kwamba hakuna rekodi ya Mheshimiwa Rais kutoa ahadi hiyo.

Nimefanya hivyo kwa juhudi kwa maelekezo yale yale ya kawaida kwamba pale ambapo Mheshimiwa Rais ameelekeza sisi kama Mawaziri hatuna jambo jingine la kufanya bali ni kutekeleza hilo. Lakini hakuna rekodi ya ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais.

Kwa hiyo, hatukuichukulia kwa hali hiyo. Lakini nisisitize tena kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameomba tufanye mabadiliko, tutajitahidi kufanya mabadiliko hayo kwa kushirikiane naye pale ambapo itakuwa imewezekana.

Na. 81

Ujenzi wa Barabara ya Nyamwage Hadi Utete kwa Kiwango cha Lami

MHE. RAJAB A MOHAMMEND (K.n.y. KURUTHUM J. MCHUCHULI) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ya Nyamwage hadi Utete (Rufiji) kwa Kiwango cha Lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthumu Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyamwage – Utete yenye urefu wa kilometa 33 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Barabara hii ni ya changarawe na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

inapitika majira yote ya mwaka. Kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, barabara hii haipo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mpango wa Serikali ni kuzijenga barabara kuu zinazounganisha Mikoa (*trunk Roads*) pamoja na kukamilisha miradi inayoendelea. Barabara zingine tutazijenga kwa awamu jinsi upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu. Aidha, Serikali itaendela kuifanyia matengenezo barabara hii ili iendelee kuptika majira yote ya mwaka.

MHE. RAJAB A. MOHAMMEND: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo hayana afya kwa wananchi wa Rufiji. Mheshimiwa Waziri huoni majibu haya ni ya kibaguzi na ya kuwavunja moyo wananchi wa Rufiji. Hasa ukizingatia kwamba barabara hii ina umuhimu kwao lakini wewe unasema kwamba haiko katika mpango wa kuiwekea lami. Wao wanajua kwamba barabara hii ndiyo inayoenda katika Makao Makuu ya Wilaya na ndiyo inaenda katika Hospitali Kuu ya Wilaya.

(c)Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri unasema kwamba ni ufinyu wa Bajeti. Wananchi wa Rufiji wanaenlewa kwamba katika muda wa miaka mitatu, Serikali imetoa misamaha ya kodi ya *one point eight trillion* lakini vilevile imeshindwa kukusanya maduhuli ya *one point four trillion* kwa miaka mitatu na wananchi wa Rufiji wanalijua hilo. Serikali leo inakuaje inasema kwamba hakuna fedha, Bajeti finyu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo. Kwanza kabisa sijasema kwamba Barabara ile siyo muhimu. Barabara zote ambazo tume – *transfer* kwenye Nchi, kuna barabara kuu na barabara za Mikoa. Barabara hii nimesema ni barabara ya Mkoa, iko chini ya Wizara yangu na ninaposema kwamba haipo mpango na maana kwa sasa kuna barabara ambazo tayari tunaendela kuzijenga lazima kwanza tuzimalize hizo, halafu tutaendelea na zingine.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Haiwezekani kwamba barabara zote kilomieta 86 elfu za Nchi hii, mnaweza kuzianza kujenga kwa kiwango cha lami kwa mara moja. Lazima twende kwa mpango na kama tunavyosema kwamba tuna upungufu wa fedha, ni kwamba inategemeana na Bajeti.

Bajeti ambayo tumepewa kwa mwaka huu hairuhusu kuanza kujenga barabara hiyo. Lakini miaka inayokuja kwa kuzingatia namna mtakavyoruhusu Bajeti tutaendelea kuzijenga barabara hizi Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya kwenda Makao Makuu ya Wilaya pale Utete ziko ziko mbili. Iko barabara kutoka Nyamwage kwenda Utete na barabara ya kutoka Kibiti kwenda Utete. Kwa wanaotoka Kibiti kwenda Utete kwa kupitia barabara ya Kibiti, Mkongo - Utete ni kilomita kama 40, lakini ukizunguuka Namage ni zaidi ya kilometa 100 na kwakuwa barabara hii ni kama *alternative Track Road* kwa barabara kubwa ya Kibiti Lindi.

Endapo Daraja la Mkapa likiwa na matatizo matatizo barabara hii ndiyo inayotumika kama *Alternative Track Road*. Je, kwa kuwa barabara hii ina umuhimu sana Serikali haioni kwamba sasa hivi kuna haja ya kuiweka kwenye mpango ili nayo iweze ili nayo iweze kujenga kwa lami kuanzia Kibiti, Mkongo, Utete mpaka Nyamwage?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa wa Kibiti kama ifuatavyo. Ni kweli kama anavyosema barabara ya Kibiti, Utete, ni barabara muhimu na ndiyo maana kwa sasa tunatumia kivuko kwenda kwenye Makao Makuu ya Wilaya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Kuhusu kuijenga kwa kiwango cha lami kama anavyotaka jibu lake linafafana kama lile jibu la kwanza kwamba barabara hizi zote, ambazo ni za Mikoa tutazifanya kwa baadae baada ya kumaliza hizi barabara ambanzo ni Kuu *Track Road* kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa kwa Tanzania nzima.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimeshahau kuwatambua wageni. Kwanza kabisa nina wageni ambao wamefika kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 35 kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tawi la Mtwara. Karibuni sana. Tuna wageni wengine Waheshimiwa Wabunge, ni Mwinjilisti Elisha Samson, kutoka Bukombe. Ni Mgeni wa Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Godbless Lema wa Ndugu Allbless Lema na Ndugu Brillian Lema, lazima wako na mama yao, haiwezani kuwa peke yao. Hao ni watoto wa Bwana Godbless Lema.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze shughuli za kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Anna Abdallah, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 11 Desemba, 2013 saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 231.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*).

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba tuko Bungeni, wengine wanazungumza kama vile wako nje. Siku nyingine mtatajwa na wananchi wenu wawasikie mnavyopiga domo humu ndani.

Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed – Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Bunge ya Serikali za Mitaa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 watakuwa na kikao chao kwenye Ukumbi wa *Basement*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Kaimu Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Huduma za Jamii, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 227.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Mary Chatanda, ameomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa (C). Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yao kwamba watakuwa na kikao saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa (B).

Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya PAC, kuwa watakuwa na kikao saa 7.15 mchana katika Ukumbi wa *Basement*. Kwa hiyo, hizi ni shughuli za kazi.

HOJA ZA KAMATI

Taarifa za

Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Bunge ya Bajeti na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Pamoja na Mapendekezo na Maoni Yaliyomo Katika Taarifa hizo

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. APHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7). Lakini pia iende pamoja na Kanuni 39(1)(3). Ambayo moja inasema Waziri anaweza kuulizwa maswali kuhusu masuala yoyote ya umma au jambo lingine lolote ambalo linasimamiwa na ofisi yake na fasili ya (3) inasema:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. APHAXARD K.N. LUGOLA]

Madhumuni halali ya swali lolote yatakuwa ni kutekeleza Ibara ya 63(2) na 63(3)(a) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako, Wabunge tufahamu kama katika kipindi cha maswali ni fursa kwa Mbunge kuuliza swali ama ni fursa kwa Mbunge kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimeomba mwongozo huo kwa sababu, kumezoeleka tabia kwa baadhi ya Mawaziri wanataka kutumia fursa ya kipindi cha Maswali, kuwafanya Wabunge wasiwaulize maswali lakini wawashauri wapendekeze. Nimesema hivyo kwa sababu muda mfupi uliopita wakati wa Kipindi cha Maswali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Hawa Ghasia, wakati nilipomwuliza Swali la Nyongeza la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, aliniambia mimi kwamba sikumtendea haki kwa nini nisiishauri Serikali igezo vya kuanzisha Wizara Maalum.

Pia wakati anamjibu Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, aliyemwuliza anachukua hatua gani kwa watendaji wa Halmashauri ya Manyovu, kutopanda miti. Akasema nakushauri Mheshimiwa Albert Ntabaliba uende kule wewe ndiye uchukue hatua, ukishindwa ndiyo uje uniambie.

Mheshimiwa Spika, tabia hii ya baadhi ya Mawaziri, kutuambia sisi Wabunge tuwashauri, na wao ndiyo wanaolipwa mishahara kwa kazi hiyo, wana wataalam ambao wanalipwa mishara mizuri sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, mwongozo ni nini. Hayo ya mishahara yamekujaje?

MHE. APHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako je, ni sahihi baadhi ya Mawaziri kututaka sisi wakati wa Maswali, tusiwaulize Maswali, lakini tuwashauri ni sahihi? (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, katika kifungu cha Katiba kile, kile kinasema kuwashauri na kuisimamia Serikali, ni sahihi tu. Isipokuwa mnakosa uvumilivu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi ya leo hii, tutakuwa na wachangiaji na kwa hesabu zangu tena tumeishakula muda mwingine, hawatazidi wachangiaji wanane (8) tumekwisha tumia hizi dakika, maana yake hapo palikuwa na mtu mmoja zaidi.

Kwa hiyo watakuwa wanane (8). Kipindi cha jioni tukirudi tutakuwa na wachangiaji kidogo upande wa Serikali, halafu watatoa watoa hoja kila mmoja atakuwa na dakika 30 ku-*react* katika mijadala tuliyokuwa nayo katika siku hizi tatu. Kwa hiyo, wachangiaji nilionao kwa sasa ni Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Deusderius J. Mipata, Mheshimiwa Dustan Mkapa, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah na sana sana tukiweza tunaweza kumfikia Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi. *(Makofi)*

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kutokana na hotuba ambazo zimetolewa. Kwanza niwapongeze watoa hotuba zote.

Kamati ya Bajeti, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, kwa umahiri wao mzuri pamoja na Wanakamati wao na mimi nikiwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa kuweza kupangilia vizuri na hatimaye kuweza kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba katika Halmashauri zetu kuna matatizo makubwa sana. Wengi wamezungumza, na yamezungumzwa miaka mingi iliyopita lakini kumeonekana kwamba hakuna mabadiliko

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

yoyote na sijui tunalitakia nini taifa hili. Lakini kwa kweli Halmashauri zetu zina matatizo makubwa sana. Ambayo yanahitaji ...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, jaribu kunyanyua *microphone* hiyo unayoitumia juu kidogo, kwa sababu tunakusikia kwa mbali.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa sana katika Halmashauri zetu. Matatizo haya yamezungumzwa sana muda mrefu hata miaka iliyopita. Nimeingia hapa Bungeni nimekuta watu wakilalamika wakizungumzia kuhusu matatizo yaliyoko katika Halmashauri zetu lakini pia hata katika kipindi hiki ambacho nimekaa Bungeni, yamekuwa yakizungumzwa hayo hayo bila kuwepo marekebisho.

Mheshimiwa Spika, tukianza na Mfuko wa Jimbo, tunafahamu kabisa kwamba Mfuko wa Jimbo, Mwenyekiti ni Mbunge mwenyewe, pamoja na wengine wanaohusika. Lakini kuna baadhi ya Halmashauri ambazo zimehodhi madaraka ya Mbunge, na kujifanya kwamba wao ndiyo wakubwa wa Mfuko huu, katika kupanga mikakati ama shughuli za kufanyia Mfuko huu. Mambo hayo tumeyaona katika Halmashauri ya Korogwe Vijijini, ambapo Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini, hajui ni namna gani Mfuko wake wa Jimbo unavyotumika na wala hahusishwi kwa lolote.

Mfuko huu ameushikilia Mwenyekiti wa Halmashauri ndiye ambaye anapanga mipango yote. Hili linasikitisha sana, kwa sababu wananchi hawapati nafasi ya kuibua Miradi ambayo wanaitaka wao ili Mbunge aweze kufanya kazi yake ikiwa ni pamoja na kusaidia yale ambayo yeye alikuwa ameyaahidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna baadhi ya Halmashauri ambazo zimefikia hatua ya kutumia Mfuko huu, kwa Miradi ambayo pia haikuibuliwa na Wananchi kwa wao wenyewe kupanga wanavyotaka na kisha kusingizia kwamba Mbunge wa Jimbo hilo analifahamu. Hii imetokea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

katika Halmashauri ya Muheza na pia inarudisha nyuma juhudi za Halmashauri na juhudi za Mbunge.

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo kwa sababu gani. Kama kutakuwa hakuna uelewano katika ya Mbunge na Halmashauri katika Mfuko huu. Huu unakuwa ni udhoofishaji wa shughuli za Mbunge kwenye Jimbo, lakini pia inamfanya hata Mbunge mwenyewe asiweze kusimamia ipasavyo maendeleo katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo limeonekana ni katika usimamizi wa Miradi. Kuna udhaifu mkubwa sana tena wa makusudi katika usimamizi wa Miradi, kwa maana ya kwamba watu wanapeana Zabuni kwa kujuana bila kujali uwezo wa mtu kufanya kazi.

Kwa mfano katika Jimbo la Korogwe Vijijini, tulishuhudia Mwenyekiti wa Halmashauri anaweka saini kwenye Karatasi inayoitwa eti ni ya Mkataba, binafsi siwezi kukubali kwamba ni ya Mkataba, kwa sababu mimi ni Mwanasheria, ninafahamu zilivyo karatasi za kisheria. Eti ni ya Mkataba yeye peke yake na kuruhusu Wakala kukusanya ushuru yeye peke yake bila Mkurugenzi kusaini, wala watu wengine kusaini. Mkataba unasema kwamba asaini mbele ya watu wawili.

Hakuna mtu yeyote aliye saini pale ni yeye mwenyewe peke yake, na fedha inayoletwa kwenye Halmashauri ni kidogo sana. Tulijaribu kumwuliza kwa sababu tulikuwepo, ni kwa nini imekuwa hivi. Alisema yeye anachojua ni kwamba ameweka saini na wala yeye hayuko kwenye Bodi ya Wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyo ni Mwenyekiti wa Halmashauri. Tunasema kwamba Halmashauri zetu zinadhoofika. Mwenyekiti wa Halmashauri ni Diwani, ndiye mwakilishi wa wananchi. Anashirikiana na watendaji wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

Halmashauri kudhoofisha Halmashauri. Kitu kingine ambacho tulikiona na ambacho kimedhoofisha pia, ni kutokuelewana kati ya viongozi wa Serikali na baadhi ya viongozi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Korogwe Mjini, alisimama Mwenyekiti wa Halmashauri, walisimama Madiwani, wakalalamikiwa kwamba wanashindwa kufanya kazi zao kwa sababu wanaingiliwa na Mkuu wa Wilaya. Mkuu wa Wilaya anapanga mipango yake analeta. Na wao wakipanga mipango yao haiendi. Kwa hiyo mipango imesimama haiendi vizuri. Halmashauri ya Korogwe Mjini ina hayo matatizo. Ninaiomba Mamlaka inayohusika iingilie kati suala hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), alikuwepo hili analijua. Pia Waziri Mkuu tumepata taarifa pia analijua. Lakini tunashangaa mpaka sasa amekaa kimya, Halmashauri ya Korogwe inaendelea kudidimia. Wamezungumza wao wenyewe mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pia linarudisha nyuma maendeleo na Halmashauri zetu, katika kupeana Zabuni kwa kujuana. Katika Kata ya Mazinde kuna Sekondari moja ambapo katika Kata hiyo, mtu na mkwewe ndiyo wahusika.

Mheshimiwa Spika, Baba Mkwe, ndiye Diwani wa Kata, aliyepo mwanaye ndiye Afisa Mtendaji. Wameshindwa kupeleka katika Baraza la Madiwani, kuelezea matatizo ambayo yanaikabili shule ile kupitia kwa Diwani wao. Kwa sababu inaonekana kwamba Diwani ameshindwa kusimamia Kata yake. Sasa Afisa Mtendaji hawezi kumchongea Diwani kwenye Baraza au mahali popote kwenye Mamlaka inayohusika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

Matokeo yake shule ile haina vyoo, wala haina chochote, tuliwaambia kama haiwezekani basi ifungwe, kwa sababu shule imezunguukwa na kinyesi watu hawana sehemu ya kujisaidia.

Mheshimiwa Spika, vitu hivyo vinarudisha nyuma maendeleo. Vitu kama hivyo ndivyo vinavyofanya Halmashauri zetu zinaonekana kwamba hazifanyi kazi. TAMISEMI inaonekana kwamba haifanyi kazi. Hivyo ndivyo vinavyofanya hali inakuwa hivyo. Lakini kama vitarekebishwa, mimi naamini kabisa mambo yatakwenenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, Morogoro tunaye mama mmoja ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri anafanya kazi vizuri sana. Huyu mama anahujumiwa sana. Sasa tunashindwa kuelewa ni TAMISEMI ama ni Mkoa. Kuna hii fedha ya barabara ambayo inatoka Wizarani. Wanasema inapitia mkoani. Huyu mama kila anapojaribu kuifuatilia anapata vikwazo.

Matokeo yake barabara zinakuwa hazijengwi, zinaendelea kuchakaa. Kila akizungumza anapewa vitisho. Aliongea mbele ya Kamati mpaka anataka kulia, kwamba ninaomba mnisaidie. Mkoani wanani katisha tamaa. Na kule mkoani wana-*coordinate* na kule Wizarani. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) (Mheshimiwa Hawa Ghasi), una watendaji ambao ninafikiri ama kwa kufahamu ama kwa kutokufahamu wanakuhujumu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kuzungumzia ni uwezo mdogo wa watendaji. Wakati mwingine Halmashauri zinakwamishwa na uwezo mdogo wa Watendaji. Sasa sijui hawa watendaji huwa wanachaguliwa na TAMISEMI ama ni wao wenye ndio wanaowachagua. Tunashindwa kuelewa ndiyo maana tunaendelea kumtwisha mzigo Waziri atatueleza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

Mheshimiwa Spika, Mbozi kuna mgogoro mkubwa sana wa ardhi, Halmashauri yao karibu inabinafsishwa. Kesi ziko nyingi za ardhi Mahakamani, tuliuliza pale tukaambiwa hakuna Afisa Ardhi, ambaye anakidhi viwango. Halmashauri inazidi kupoteza mapato. Halmashauri inazidi kuadhirika sijui TAMISEMI hili kama mnalijua na mmechukua hatua gani, lakini taarifa tumeishazileta ofisini kwenu lakini kama kawaida mmekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa ya Wanasheria katika Halmashauri zetu. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza hakuna Mwanasheria. Wakiwa na shida wanaazima Mwanasheria kutoka Pangani. Huyu wa Pangani naye alikuja Muheza akaharibu, alivyoharibu amekwenda kuadhibiwa Pangani. Kwa hiyo Muheza mpaka sasa hakuna Mwanasheria.

Sasa zile kesi zilizopo pale. Wakati mwingine Halmashauri ina kesi ambayo inaweza ikashinda na ikaongeza mapato pengine kuna kitu inagombea, nani atazisimamia? Tena katika hili ninaomba niulize na Waziri mimi ninaomba ujibu vizuri tu. Kwamba hata katika kipindi kilichopita wakati niko kwenye Kamati nyingine hili la Wanasheria tullilizungumzia sana ya kwamba Halmashauri zetu hazina Wanasheria na kumekuwa kuna mvutano kwenye uajiri.

Tuliwahi kutoa ushauri kwamba Halmashauri zenyewe ziajiri. Sasa leo utatujibu ni nani ambaye anatakiwa apeleke Wanasheria katika Halmashauri, ni Wizara ama ni Halmashauri zenyewe ndizo ziajiri? Kwa sababu Mwanasheria ndiye roho ya Halmashauri. Kama hakuna Mwanasheria kwenye Halmashauri kuna kuwa kuna matatizo makubwa sana. Samahani ni Muheza na siyo Handeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo lilijitokeza katika Mkoa wa Tanga ni katika Wilaya ya Handeni ambako kuna udhaifu mkubwa katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Nimeitoa Handeni hii kama kielelezo, lakini imeonyesha kabisa katika Halmashauri zetu nyingi. Asilimia (80%) ya Halmashauri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

zetu nyingi zina matatizo katika kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (*Internal Auditor*). Sasa mimi sijui, kama hawana taaluma. Hawakidhi viwango mimi sifahamu. Lakini ni kwa nini hili litokee kwa sababu hapa ndipo pesa za Halmashauri zinafujwa, zinaibiwa. Watu wanachota wanavyotoka, *business as usual*. Tumekwenda Handeni pale tena wale *Internal Auditors* wako watatu tena vijana. Lakini hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, awasilize sana Wabunge kuhusu kilio hiki cha TAMISEMI, hali ni mbaya sana. Mimi binafsi nilikuwa ninasikia tu zamani. Lakini sasa hivi nimejionea kwa macho hali ni mbaya. Ninashangaa ambapo kunatakiwa kuongezwa miji mingine ili hali hii iliyopo tu tayari iliishakuwa ni tatizo. Mimi ninaomba kwanza tufanye maboresho.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya WAZiri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) tuboreshe kwanza hizi Halmashari zetu zilizopo, tuondoe haya matatizo mengi yaliyopo, ndipo tuanzishe miji mingine. Kwa kufanya kinyume na hali hiyo ni kuongeza mizigo mingine mikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), hilo alione alifanyie kazi, Halmashauri zilizopo ziboreshwe, tuondoe uozo uliopo huu, maana yake matatizo yote unatwishwa wewe Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Wenyeviti wa Halmashauri zetu, ambao ni wanasiasa wenzetu wanashirikiana na Watendaji kuhujumu Halmashauri zetu. Hili tumeligundua wakati tunapo wahoji. Tunahoji ubadhilifu wa pesa zilizopo kwenye Halmashauri, katika Miradi mbali mbali. Kandarasi mbali mbali zimetolewa, ambapo zile Kandarasi zinapotolewa ni lazima Mwenyekiti wa Halmashauri anajua. Lazima Mkurugenzi kama kawaida anajua. Lakini Mwenyekiti wa Halmashauri anapoulizwa anacheka tu, yaani anacheka. Kucheka tu, hasemi chochote anabakia anatabasamu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

Hili lilitokea mbele yetu tukiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbulu, kweli alitusikitisha sana. Alitusikitisha sana Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbulu. Maana mimi nilisema labda Mbunge wa kule kwa kuwa labda ni CHADEMA, lakini mbona Madiwani pale wengi ni wa CCM na Mwenyekiti wa Halmashauri mbona ni CCM. Tunamwuliza kwa nini fedha inachezewa namna hii inapotea yeye anacheka tu. Halafu ndiye Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, hii ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema Mheshimiwa Kinana kama unanisia huko uliko ninaomba utusaidie. Hao Mawaziri wewe waache tu wakae ofisini. Lakini ninaomba utusaidie Hawa Wenyeviti wa Halmashauri hawa wanaoshirikiana na Watendaji kuiba fedha za wananchi watimuliwe mara moja. Haiwezekani Mwenyekiti wa Halmashauri unaitwa mbele ya Kamati, unaulizwa kitu kiko wazi halafu unanza kucheka tu pale. Unamchekea nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaonyesha ni kwa jinsi gani hawa watu ni Miungu watu na hawaguswi. Pengine maskini ya Muungu hata Waziri akisema kitu hawamsikilizi. Kuna vitisho, na hivi ni mwanamke basi ndiyo imeishakuwa ni balaa.

Lakini mimi ninasema Mheshimiwa Waziri simama imara kitaeleweka kama utaamua. Kwa sababu unafanya kazi kwa kufuata sheria na taratibu. Hufanyi kazi kufuata unayoyataka wewe. Kama utasimamia sheria yanawezekana. Wametokea Wakurugenzi wanaofanya vitu vya ajabu, ni wezi, wanajulinana wamehamishwa na wengine wamepandishwa vyeo.

Mheshimiwa Waziri vitu kama hivi ndiyo kero, shughulika nao. Ukimtoa mmoja ama wawili heshima itakuja na hawata kuchezea tena. Kama ni Mamlaka ya juu ndiyo ambao wanafanya vitu kama hivyo, wasiliana nao. Baraza la Mawaziri Mwenyekiti ni Mheshimiwa Rais, mshaurini mwambieni huyu mtu yuko hivi, hivi na hivi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PHILIPA G. MTURANO]

Mbona Wakurugenzi wengine akisikika tu hisia kwamba anapelekwa Halmashauri fulani au Jiji fulani, kama ni mwizi watu wanamkataa na ushahidi tunaujua siyo lazima niwataje hapa. Kwa nini tuendeleo kuwakumbatia watu ambao wako hivyo? Nasi tunaomba mtupe meno LAAC na tumeshaanza hiyo kazi pamoja na kwamba, hamtupi meno, lakini wale ambao wamesababisha wizi kwenye Halmashauri tunapokuwa tunahoji Halmashauri ...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, muda umekwisha.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Kwa hiyo, ile kaulimbiu ni *Better Resign Now siyo Now Better Results Now!*

SPIKA: Mheshimiwa Alhaji Missanga!

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi katika kipindi hiki cha mwisho mwisho nilishakata tamaa.

Baada ya maelezo mazuri sana ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kuhusiana na Taarifa za Kamati hizi tatu, unajikuta mtu umefilisika kwa sababu yale yote ambayo ulitaka kusema jamesemwa na Kanuni zetu haziruhusu kurudiarudia.

Nianze kwa kuzipongeza Kamati hizi tatu na hasa Wenyeviti wao, kwa taarifa nzuri na bayana ambapo wamebainisha upungufu kadhaa uliopo. Nawapongeza sana na niwatakie kila la kheri katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiamua kuacha mambo ambayo jamesemwa sana na wenzangu, niseme kwa ujumla; moja, Kamati hizi tatu zimetuletea tatizo, yaani zimewasilisha kwetu tatizo ambalo lipo na si lingine isipokuwa ni nidhamu mbovu ya matumizi ya fedha za Serikali. Hilo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

ndiyo tatizo ambalo tumeletewa na wameleta kwenye Bunge hili ili Bunge lisaidie kulitatua tatizo hilo la nidhamu mbovu katika matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Taarifa ya Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali za Mitaa, ukurasa wa saba, naomba kumnukuu, anasema; "Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, bado kuna ubadhirifu, ufiisadi na utovu wa nidhamu wa hali ya juu wa matumizi ya fedha za umma na hii inatokana na Wizara husika (TAMISEMI), kutosimamia kwa karibu au yenyewe kuhusika moja kwa moja na ufiisadi huu."

Mheshimiwa Spika, haya maneno ni makali mno, hii *statement* ni kali mno, mimi ninavyoiona sijui wenzangu kama wanaipuuza au wanaonaje. Hii ni *record*, haya maelezo yameingia kwenye *Hansard* na yatasomwa na vizazi vijavyo. Wananchi watasoma kwamba, Bunge lilipelekewa tatizo kwamba, kuna nidhamu mbaya sana ya matumizi ya Serikali ndani ya Serikali. Sasa Bunge linafanyaje? Huyu ni Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa.

Ukichukua Taarifa ya Mheshimiwa Zitto, kwenye ukurasa wa saba vilevile, kifungu namba 24, amekwenda mpaka karibu kurasa sita, saba, akiainisha upungufu juu ya matumizi mabovu ya fedha za Serikali. Hiyo nayo ni *record*, ipo, imeingia kwenye *Hansard*. Watu watajuliza hivi Bunge baada ya kupelekewa tatizo hili limechukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, sitaki kuingia katika *details* ambazo wenzangu wameingia, lakini mimi nazungumza hili la ujumla, tumeletewa tatizo kwamba Serikali ina matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, Naibu Waziri wa Fedha alipokuwa anajibu swali Siku ya Jumatano au Alhamisi alikiri, nadhani swali lilikuwa la Mheshimiwa Hamad. Naomba nim-*quote* kwenye jarida lako ambalo nadhani ni *official*, linaitwa *Bunge Daily News*. Mheshimiwa Janet Mbene anasema: "Ni kweli kuwa, nidhamu ya matumizi ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

moja ya matatizo makubwa Serikalini." Waziri anakiri kwamba na Serikali wanajua kuwa hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema limeletwa kwetu hapa na kama limeletwa kwetu maana yake ni lazima tutoke na kauli ya kusaidia. Vinginevyo, hii *Hansard* atakayekuja kusoma baadaye asione baada ya hapo Bunge lilisema nini, tutakuwa hatujatimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze, Serikali ilipoleta kilio cha kwamba mapato ya Serikali ni madogo kwa muda mrefu, ulitumia busara yako, ukashawishi Bunge likaboresha Kanuni zake na ikaundwa Kamati ya Bajeti ili iisaidie Serikali katika kupata mapato zaidi hasa kwa kubuni vyanzo vingine vya matumizi. Kamati ya Mheshimiwa Chenge inafanya kazi nzuri na ndiyo kwanza wameanza na nina hakika wakipewa nafasi na ushirikiano, wanaweza wakafanya kazi nzuri zaidi.

Wakati Bunge lako likijihusisha na upataji wa mapato kwa wingi ili kukidhi mahitaji makubwa ya Serikali, sasa linakuja hili bomu, kwamba jamani hicho mnachokusanya wenzenu huku tunatafuna, Waziri anakiri! (*Makofi*)

Sasa mimi napata tatizo, tufanyeje? Tumwambie Mheshimiwa Chenge asimamishe kazi ili abuni vyanzo vipya vya mapato au tunafanyaje? Kwa hiyo, nasema tunalo tatizo kubwa ambalo tumeletewa na wenzetu, Kamati zetu zote tatu kuna ubadhirifu mkubwa na kuna nidhamu mbovu kama ilivyoandikwa ya matumizi ya fedha Serikalini na sisi tunategemewa kutoa jibu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika hili lazima tuseme kitu, lazima tuiielekeze Serikali kitu ili tuonekane tumetenda haki, lakini pia tumewatendea haki Wanakamati wa Kamati zote tatu kwa tatizo ambalo wametuletea. Hilo ndiyo la ujumla ambalo nilitaka kusema. Sasa sina hakika Waheshimiwa Wenyeviti hawa watatu wamejipanga namna gani, sina hakika watakapokuwa wanakuja kujibu kama ulivyoeleza hapa. Mimi ningepata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

mapema ningewaambia walau wakutane wao wenyewe wote watatu, kama siyo Kamati zote tatu walau Wenyeviti, waje na azimio hapa wanataka Bunge hili lifanye nini juu ya tatizo kubwa ambalo wamelieleza kwamba jamani eeh, hata mkipata fedha kiasi gani nidhamu ya matumizi ni mbovu. (*Makofi*)

Mimi niwashauri sana Mheshimiwa Chenge na wenzake kuwa kule watusaidie Bunge hili waje na azimio litakalotoa dawa. Vinginevyo, watoto wetu na vizazi vyetu vijavyo watakaposoma *Hansard* hizi, wataona kweli hatukutenda haki na tutakuwa hatukuzitendea haki Kamati zetu tatu ambazo zimetuletea tatizo. (*Makofi*)

Hilo ni la ujumla nimesema sitaki kuingia kwenye yale ya moja moja ambayo yalisemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Sasa niende Jimboni kwangu, naendelea kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Sisi watu wa Singida tumepata Wilaya ya Ikungi, nashukuru sana na mimi nilihangaika sana na wenzangu. Hizi Wilaya mpya sijui maelekezo hayajatoka sawasawa, yapo malumbano makubwa sana kati ya Halmashauri mpya na Halmashauri Mama.

Pale Singida, kwanza, yalianza malumbano ya namna ya kugawana watumishi. Nampongeza na kumshukuru Mkuu wa Mkoa, amejitahidi sana akatatua tatizo hili. Sasa hivi lipo tatizo la pesa. Mimi nilidhani kwa busara ya kawaida, hizi Halmashauri mpya ndiyo ambazo hazijajiweka sawasawa walau wangepewa *priority* ya fedha za utawala na nyingine ili ziweze kukaa sawasawa. Matokeo yake fedha zinakwenda kwenye Halmashauri Mama na Halmashauri Mama hazitaki ku-*release* zile fedha hasa za utawala.

Mwezi Julai, Halmashauri Mama ilipelekewa shilingi milioni 51 kwa maana ya Halmashauri Mama pamoja na Halmashauri ya Ikungi, zimekamatwa hazikugawiwa. Mwezi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

wa Agosti hakuna fedha zilizopatikana, mwezi wa Septemba zilipelekwa tena shilingi milioni 51, Halmashauri Mama imezibana haitaki kutoa. Mwezi Oktoba zimepelekwa nusu, milioni 28, Halmashauri Mama imebana haitaki kugawa kwa mwenzake. Sasa hizi Halmashauri mpya zitafanya kazi namna gani?

Halmashauri hii kuna Vikao vya Kisheria vya Madiwani. Halmashauri hii mpya ina Watumishi ambao wameletwa kutoka maeneo mbalimbali, yapo maeneo karibu sita, posho zao zinatakiwa zilipwe na Halmashauri ya Ikungi, italipa na fedha gani wakati fedha zimekaliwa na Halmashauri Mama? Sasa sioni ni kwa nini Serikali inashindwa kuamua tatizo kama hili?

Halmashauri ya Ikungi ina akaunti zake, kuna tatizo gani la kutokutoa fedha ambazo zipo kwenye bajeti zikapelekwa kwenye Halmashauri hiyo mpya zipelekwe kwanza kwenye Halmashauri Mama halafu baadaye tena ndiyo zipelekwe kwenye Halmashauri mpya? Hiyo ni *duplication* ya kazi ambayo haina sababu, ni kupoteza fedha za Serikali tu. Naomba sana, hili itafika Madiwani wa Halmashauri mbili hizi wabadilishane maneno mabovu na wanaweza hata wakafikia hatua ambayo siyo nzuri kama Serikali haitachukua hatua za haraka katika jambo hili.

Mheshimiwa Waziri Ghasia, nakuomba sana hili lichukuliwe kwa sababu limefika mahali pabaya. Maneno yanayosemwa na Madiwani hasa wa Wilaya ya Ikungi dhidi ya Madiwani wa Halmashauri Mama ni mabovu na wana haki ya kufanya hivyo. Naomba sana uchukue hatua.

Tatu, Taarifa ya Kamati ya Mheshimiwa Rajab inasema kwamba, zipo fedha za Mfuko wa Jimbo hazitumiki. Mimi nashangaa, lakini ukweli ni kwamba, sawa, kama fedha zinakuja mwezi wa nne au wa tano zitatumika saa ngapi? Kwa nini fedha hizi zinachelewa na zipo *budgeted* na mwaka huu tumesema bajeti imeisha mwezi wa sita, kuanzia mwezi wa saba na kuendelea Serikali itekeleze; sasa hazijafika unategemea zitatumika namna gani?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED H. MISSANGA]

Mheshimiwa Spika, naomba sana fedha za Mfuko wa Jimbo, hivi ninavyozungumza na watu siku hizi wanazijua, Mheshimiwa Mbunge, tunaomba msaada kwenye Mfuko wa Jimbo. Ukimwambia fedha hakuna haamini ni ugomvi kati ya Wabunge na Wananchi kwa sababu wanategemea kupata msaada kutokana na fedha hizo. Naomba sana fedha hizi ziwahi. (*Makofi*)

Pili, gharama za maisha zimepanda, viwango ambavyo vililekwa huko nyuma sasa vimebadilika. Naomba Serikali ihusishe viwango hivi. Halmashauri au Jimbo kama la kwangu kupata shilingi milioni thelathini hazikidhi haja na kwa sababu Wananchi sasa walio wengi wanaomba msaada kutoka kwenye Mfuko huo. Kwa hiyo, hilo nalo naomba sana lichukuliwe hatua.

Jambo la mwisho ni habari ya Watendaji. Mimi naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba, mwisho wa mwezi huu lazima *circular* ya kukasimu madaraka ya ajira ya Watumishi iwe imetoka; vinginevyo ni hatari. Hakuna Watumishi kwetu kule; maendeleo yatapatikana wapi? Mtendaji wa Kijiji hakuna, Mtendaji wa Kata hakuna, watu wanakaimu. Mtu anakaimu hajui leo yupo kesho hayupo, matokeo yake usimamizi wa Miradi ya Maendeleo na usimamizi wa maendeleo ya Wananchi hauwezi kuwepo mahali panapohusika kwenye vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kugongewa kengele ya pili, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja, lakini hoja zangu hizi na hasa lile la Wilaya ya Ikungi, ningeoomba sana na nimwombe Mheshimiwa Chenge na wenzake watuletee azimio juu ya utovu wa nidhamu ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Mwambu yupo? Anayefuata ni Mheshimiwa Desderius Mipata!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie Taarifa za Kamati hizi tatu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati wa *PAC*, nawapongeza Wenyeviti kwa utaratibu mzuri walioutumia kuwasilisha Taarifa hizi. Pia nampongeza *CAG* kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kubainisha yote haya ambayo yanatufanya tuchangie katika Taarifa hii.

Kwanza, ni katika mapato. Katika mapato tumeona *trend* ya mapato ilivyo na inatupa fursa kwamba, tukitegemea vyanzo vya nje tutakwama. Kwenye Taarifa ya Bajeti inaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa tumeweza kufanikiwa kwa asilimia 85.7 kwa vyanzo vya ndani na kwa vyanzo vya nje tumefanikiwa kukusanya asilimia 32 tu; maana yake ni nini?

Maana yake ni kwamba, lazima tuhakikishe tunatilia mkazo katika kutafuta vyanzo vyetu sisi wenyewe. Nchi yetu imekaa mahali ambapo ni *strategic* kwa suala la mapato. Ukanda wa bahari ambao tunapakana nao ni faida kwa Tanzania, hali ya mvua ni faida kwa Tanzania. Madini na maliasili vikitumika vizuri na watu tulionao, bado vingeweza kuchangia sana katika mapato. Kwa hiyo, kama Taifa ni lazima tuanze kutafuta njia ya kujitegemea zaidi, tuachane na njia za kutegemea wafadhili na athari zake zinaonekana kutokana na Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, pili ni juu ya utoaji wa fedha. Katika robo ya kwanza tumeona utoaji wa fedha *trend* iliyopo siyo nzuri sana na kama tukienda hivi maana yake mpaka mwisho wa mwaka tutakuwa tumetekeleza Miradi bila kufikia malengo. Sasa siyo utamaduni mzuri, kwa robo ya kwanza fedha iliyotolewa ni asilimia 11 tu badala ya asilimia 25, imeanguka kwa asilimia 14. Kama *trend* ni hiyo maana yake tutafika mwisho wa mwaka hatujafanya vizuri. Fedha za mikoa vilevile zimefikia asilimia 17 badala ya asilimia 25, maana yake ni kwamba, tumeanguka kwa asilimia nane, siyo utamaduni mzuri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DESDERIUS J. MIPATA]

Katika Halmashauri zetu pia tumeziona changamoto nyingi na nyingi zimezungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Mimi ni Mjumbe wa ALAT, ninayewakilisha Mkoa wa Rukwa. Nataka niseme Halmashauri zina changamoto nyingi na nyingi zinasababishwa na Serikali. Mojawapo; kuchelewa kupeleka fedha kwenye Halmashauri kunasababisha udhaifu mwingi. Moja, ndiyo hiyo Halmashauri ambayo tumeipa mambo mengi isimamie, Wizara nyingi sasa zinaangukia kwenye Halmashauri kule chini, lakini unawapa pesa kwa kuchelewa unategemea nini? Lazima utegeme kutapatikana changamoto.

Pesa tunazowapa ni kidogo kuliko walichokadiria wao na ruzuku za fidia zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka. Ni wazi huwezi kupata matarajio ya ajabu bila kuwekeza vizuri na takwimu zipo hapa jinsi Halmashauri zinavyopata fedha, tunakwama kupeleka fedha. Wakurugenzi wanafanya kazi katika mazingira magumu mno, ndiyo maana watu wengi wanakimbilia hata kwenye Ubunge hapa.

Mimi nimefanya kazi kama Mwenyekiti wa Halmashauri kwa vipindi viwili, hakuna kazi mbaya kama Ukurugenzi, utasemwa na kila mtu atakuvuta Diwani, atakuvuta Mwananchi, Waziri akija na presha zake, Mkuu wa Wilaya na presha zake, Mkuu wa Mkoa na presha zake, mwisho unashindwa hata kutumia taaluma vizuri.

Kwa hiyo, tuangalie kwa makini haya yanayofikiwa badala ya kulaumu na sisi ndiyo watengeneza utaratibu, tuweke utaratibu mzuri wa kuziwezesha Halmashauri kufanya kazi na siyo kulaumu tu. Ni chombo ambacho tumekidhamini kuyapa majukumu mengi watufanyie, sasa watatufanyia bila kuwasaidia, ni lazima tujenge misingi mizuri, mojawapo ni haya yafuatayo:-

Kwanza, mapato; Halmashauri tumesema imekuwa tegemezi kwa asilimia 90. Sasa kama wewe ni tegemezi kwa asilimia 90 na huyo bwana anayekupatia pesa anakupa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DESDERIUS J. MIPATA]

anapotaka yeye ni vipi utafikia malengo ni ngumu. Ifike wakati Serikali iamini kwamba, Halmashauri inaweza, tutafute mbinu za ukusanyaji wa mapato. Mapato ambayo tunafikiri Halmashauri inaweza ikakusanya, wakusanye wao wajitegemee. Tuwawekee utaratibu, tutafute Taasisi kama ilivyo *TRA*, tutafute Taasisi ambayo inaweza ikakusanya Halmashauri zikapata pesa za kutosha na siyo kuwa tegemezi. Ikiwa tegemezi tusifikirie mafanikio hayawezi kupatikana yatapatikana wapi wala tusiyatarajie.

Pili, ni kuchelewa kuwapelekea hizo pesa ambazo tumewaahidi kwamba tutawapa. Huwezi kufanya vizuri kama unachelewa. Wana vyanzo vichache na wengi wao hawana uwezo wa kuvikusanya; watakusanyaje? Ni ngumu kufikia malengo. Mimi ningependa niwashauri, Serikali iangalie kwa makini haya mambo badala ya kutupia lawama tu kwenye Halmashauri. Nakubaliana zipo changamoto katika Miradi hatuwezi kuivumilia lazima tuchukue hatua.

Hatua zimekuwa zikichukuliwa, nakumbuka kwenye *ALAT* ya mwaka jana tulikuwa Arusha, Mheshimiwa Waziri, alitoa taarifa na kuwaasa Wakurugenzi, tena kwa ujasiri na ukali, lakini akija hapa anashambuliwa kana kwamba hafanyi kazi. Lazima muiangalie Historia ya Wizara hii, Wizara hii imekuwa ikilaumiwa Mawaziri wake karibu wote isipokuwa Waziri huyu ambaye tunaye hapa, ndipo alipokuwa anaongoza Halmashauri sikusikia kelele. (*Makofi*)

Mimi ni Mwenyekiti wa Halmashauri, niwekuwa Diwani kwa miaka 17, kwa hiyo, nilikuwa nafuatilia kwa makini. Wizara ngumu kubwa ni hii hapa. Amepewa mama wa watu badala ya kumtia moyo sasa tunamdhoofisha! Mimi sijapendezwa na michango iliyotolewa hapa, mingine haijengi, ina nia ya kunyanyasana au kama siyo kunyanyasa ni kudunisha kitu kizuri kionekane kuwa ni cha hovyoo.

Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Mama Hawa Ghasia, anafanya kazi nzuri mno na ni jasiri, tumtie moyo. Makosa yatakuwepo kwenye chombo kikubwa kama hiki,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DESDERIUS J. MIPATA]

tuyazungumze tutafute mwafaka ni namna gani tunaweza tukayasuluhisha siyo kuponda tu, mimi sijakubali. Kazi ni nzuri na nasema michango hii tunayoitoa Wabunge mingi inatokana na malezi yetu huko tunakotoka. (*Makofi*)

Sisi wengine ili upate Ubunge hapa lazima utoke huko umekuwa Balozi na vijana wale wadogowadogo wanafunzwa maadili, wanafunzwa uzalendo, wanafunzwa utii na uchapa kazi, lakini maeneo mengine wanafunzwa ubishi, kukataa, kugoma, sasa tukija humu tunakutana wote. Kwa hiyo, tunapotoa michango ya namna hii, Wananchi lazima wawe makini, huyu amelelewa wapi na huyu amelelewa wapi; ni Tanzania hii hii inayoongozwa na Jakaya Kikwete yenye sifa katika Afika Mashariki na Kati. Juzi tulikuwa Ulaya wanaisifu, tulikuwa Uingereza wanaisifu, kwa utulivu wa amani, *stable political situation* ya hapa ambayo ina-*encourage* maendeleo zaidi na imedumu kwa muda mrefu kuliko nchi nyingine. (*Kicheko/Makofi*)

Leo mtu iwe ni rahisi kusema tu kwamba CCM haijafanya vizuri, imechakaa, imechakaa namna gani? Wakati mwingine umri mkubwa ni kustahili kuwepo kwamba, unakwepa mishale mingi kwamba wewe umejiandaa vizuri, lakini siyo kuzuka na kufa, kuzuka na kufa kama vyama vingine tunavyoviona. Tuna misingi ambayo inaleta mafanikio na matarajio ya Watanzania ndiyo maana CCM inadumu leo na siyo wanavyodhani wengine kwamba, uwepo wa CCM muda mrefu haifai imechakaa, hapana ni ubora wake, ukongwe ni ubora vilevile.

Kwa hiyo, nataka niseme kuwa, Wananchi wanaosikia hotuba za Kamati hizi mbili wasifikiri mambo ni mabaya kuliko. Mimi nipo kwenye Kamati ya PAC, imeeleza hapa kwamba, ndiyo wakati ambapo Serikali na Taasisi zake zimekuwa watiifu na kurejesha hesabu vizuri na kwamba, *percentage* iliyofikiwa hakuna hati mbaya iliyofikiwa kwenye Wizara na Serikali kuu.

Taarifa hii hapa ya Bwana Zitto na mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo, sasa ubaya tunaupata wapi? Katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DESDERIUS J. MIPATA]

Uongozi ni lazima mambo yapatikane, haya mambo ni lazima tukae chini tuone yanavyokuwa na tuyachukulie hatua.

Naishauri Serikali, tusiache kuwachukulia hatua watu wabovu, tutaleta malezi mabaya, tutakaribisha maneno mengi ya kusemwasemwa bila sababu, yale yanayobainika tuyachukulie hatua, kama mama alivyokwisha kuwachukulia hatua baadhi ya Watumishi wengi tu, zaidi ya 52 wamekwisha chukuliwa hatua, Wakurugenzi tu peke yake.

Zaidi ya Watumishi 814 wa kada mbalimbali walishachukuliwa hatua kwenye Halmashauri zetu hizi. Sasa siyo lazima kila siku anasimama na kusema halafu leo ndiyo tumeipokea Taarifa, ulitegemea ayaseme haya leo! Taarifa ameipokea leo, kuna watu walikuwa kwenye matarajio mbalimbali, hatua atazichukua tu kama kawaida. Sasa ulitarajia kabla ya taarifa uwe umepata amefukuza wangapi, amechukulia hatua wangapi, ni kitu ambacho hakiwezekani katika utendaji.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba, Wizara ya TAMISEMI inafanya kazi vizuri na Wizara hii isaidiwe tu na kuivunja moyo itatupelekea turudi tulikotoka. Miaka mingi tuliivunja tukaanza kuikarabati upya, sasa tumefikia mahala pazuri leo tunashindwa kuisaidia.

Mimi nadhani tusaidiane, tuangalie changamoto zilizoko mbele yetu hizo ndiyo tushughulike nazo, badala ya kuangalia *individuals*, maana naanza kuona kuna kusonta watu vidole, unaenda naye, unataka uamke naye. Hatuwezi kwenda kama Taifa, ni lazima tuyakabili matatizo yetu na siyo mtu mmoja mmoja, hii haiwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dunstan Mkapa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia katika Kamati hizi tatu zilizopo mbele yetu. Awali ya yote, naomba niseme kwamba, mimi nipo kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa pongezi kwa Kamati hizi zote tatu, kwa kazi nzuri waliyofanya na kwa mawasilisho waliyoyotoa hapa Bungeni. Pia naomba nitoe pongezi kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukagua mahesabu yetu na kutoa taarifa. Wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini mwisho wa siku wanatuletea taarifa ambazo sisi Wabunge tunazifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze kuchangia Taarifa ya Kamati ya Bajeti. Mimi ninavyoona kwa maono yangu, mlolongo mzima wa maandalizi ya Bajeti unakuwa na gharama kubwa sana, lakini mwisho wake tunajikuta Wizara, Idara na maeneo mbalimbali pamoja na kwamba wamekisia makisio yao, lakini mwisho wa siku wanapewa pesa ambazo hawakuzikadiria.

Mfano: Utakuta makadirio haya yanaanzia vijijini mpaka ngazi ya Halmashauri, Halmashauri wanaondoka wanaenda kwa mfano Dar es Salaam, wanakaa wanajifungia huko, wanapata posho, karatasi nyingi zinatumika na mambo mengine mengi. Kama waliomba milioni 100, utakuta wanaambiwa *ceiling* yenu ni milioni 60. Sasa sioni mantiki yoyote kwa nini basi wasiambiwe *ceiling* yenu ni milioni 60, tunaomba mfanye mchanganuo kutokana na hizo milioni 60. Kwa kweli gharama kubwa zinatumika katika kuandaa bajeti, lakini mwisho wa siku pesa wanayopangiwa inakuwa ndogo.

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa katika Kamati hii tulitembelea Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Lindi kuna Miradi miwili ya Maji ya Umwagiliaji; kuna Mradi wa Ngongowele na Mradi wa Ngongo. Miradi hii imegharimu pesa nyingi sana. Ule wa Ngongowele pamoja na kwamba haujaisha,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DUNSTAN D. MKAPA]

umeshagharimu kiasi cha shilingi milioni 800 na mpaka sasa haujafanya kazi na sitegemei kama utafanya kazi. Kwa sababu Mradi ule kumbe ni kwa ajili ya wakati wa masika tu, hakuna chanzo chochote cha maji, wanasubiri mvua zinyeshe ndiyo Mradi ule uanze kufanya kazi. Kwa kweli hii ni hasara kubwa sana kwa Taifa letu, tulikwenda pale ingawa tulimkuta bundi pale anatugomea gomea na kutuchachia lakini tulikwenda tukafanya ile kazi, mwisho wa siku tukagundua ule Mradi unamaliza fedha za Serikali bure.

Tunaomba Ofisi za Kanda za Idara hii ya Umwagiliaji hazifai ziondolewe kwa sababu zinaffiisha na zinaua Miradi mingi ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara hewa, inasikitisha sana kuona idadi nyingi ya pesa zinapotea kwa ajili ya mishahara hewa. Cha kujiuliza ni kwamba, kwa mfano; mtu amekufa, Halmashauri hiyo hiyo ndiyo inaandaa mazishi ya marehemu, Halmashauri hiyo hiyo ndiyo inayoandaa kusafirisha maiti ya yule marehemu, mwisho wa siku itapita miezi mitatu, minne hadi mwaka, mshahara wa marehemu unaendelea kwenda benki tu; ni kitu cha ajabu sana!

Hata hao waliostaafu, Halmashauri au Serikali inaandaa malipo tena inamwandikia barua kwamba, kuanzia tarehe fulani utakuwa haupo kazini. Anapewa kama ni mshahara wake wa mwisho na mafao mengine ya likizo, lakini mwisho wa siku mshahara wa yule mstaafu unaendelea kwenda benki tu bila kusimamishwa. Mishahara hii inaishia mifukoni mwa watu, ukienda benki unakuta inatolewa kila mara. Kwa hiyo, naomba sana Idara ya TAMISEMI, wajitahidi kuona jambo hili na kama mtu amefariki basi mshahara wake usitishwe na kama mtu amestaafu basi mshahara wake usitishwe.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi Halmashauri nyingi zimewaweka Mawakala kukusanya mapato yake. Utakuta wale wanaokusanya mapato ndiyo wanaonufaika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DUNSTAN D. MKAPA]

zaidi kuliko hata Halmashauri, kwa sababu mikataba ile inakuwa mibovu sana. Sasa tunashauri kwamba, Wanasheria wa Halmashauri kabla hawajaingia mkataba na mhusika, wafanye utafiti kwanza waone ni kiasi gani wanachoweza kuingia mkataba na huyo mkusanyaji mapato.

Vilevile kwenye mapato, kwa mfano kwenye Ripoti ya Mwenyekiti wa LAAC, ameelezea kabisa, aya ya 219(a) kwamba, idadi ya vitabu vya kukusanyia mapato ambavyo mawakala wa ukusanyaji wa mapato hawakuvirejesha katika Halmashauri husika. Hii ina maana kwamba, hapa wizi umefanyika wameshakusanya mapato sasa wanasingizia kutopeleka vitabu kwa ajili ya mrejesho kwenye Halmashauri husika.

Kukaimu ndiyo ugonjwa mkubwa sana ndani ya TAMISEMI. Idara nyingi zinakaimiwa, Idara nyingi hazina Watendaji Wakuu wa Idara, kwa hiyo, zinawafanya wale wanaokaimu kuvunjika moyo. Wengine wanakaimu hata kwa miaka minne au mitano, wanavunjika moyo, wanafanya kazi *business as usual* kwa sababu hawajui hatima yao ni nini. (*Makofi*)

Wizi wa kimtandao ndani ya TAMISEMI upo, mfano mkubwa ni kule Mbarari ambako zilipelekwa shilingi milioni 800 na siku ya pili yake zote zikatoka kwa hundi mbalimbali. Kwa hiyo, nafikiri huo ni mtandao wa wizi ambao upo kati ya Hazina, Halmashauri pamoja na TAMISEMI.

Fedha kupelekwa mwishoni mwa mwaka wa fedha ni tatizo sugu katika Halmashauri na hasa katika Idara ya Maji. Idara ya Maji fedha zake zinapelekwa mwishoni, sijui kwa nini lakini ukikuta kwenye mahesabu yao, Halmahauri nyingi zinapata pesa za maji mwishoni mwa mwaka.

Vilevile Halmashauri hazipati *Other Charges (OC)*. Miezi kadhaa inapita bila kupelekewa *OC*. Kwa mfano, Wilayani kwangu Nanyumbu fedha za mwezi Oktoba hazikupelekwa kabisa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DUNSTAN D. MKAPA]

Sasa unajuliza Halmashauri kama haikupata fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida tutafanyaje kazi. Naomba kujua kwa nini fedha hizi hazikupelekwa wakati majibu yanatolewa na kama hazikupelekwa zitapelekwa lini kwa sababu tunazihitaji hizo fedha ili kuweza kuendeshea Halmashauri yetu ya Wilaya ya Nanyumbu?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Jimbo zinachanganywa na pesa nyingine za Halmashauri. Sasa unaweza kwenda ukataka kutumia pesa zako unaambiwa pesa hakuna, Sheria haitaki hivyo. Tumeshona hiyo ilichanganywa, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, walishatumia hizo pesa za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya matumizi mengine ambayo ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nalitolea ushauri kwa Wenyeviti na Mameya kusaini mikataba. Mimi naona hapa turudishe Bungeni kama ni Kanuni, kama ni Sheria, Wenyeviti hawa wasisaini mikataba, kwa sababu wengine hawana uelewa wa sheria. Nimesoma juzi kwenye gazeti, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Korogwe, ameingizwa matatani kwa sababu amesaini mkataba peke yake. Ninadhani siyo utaratibu mzuri; utawezaje wewe mwenyewe uwe mwendesha mashitaka, wewe wewe hakimu na wewe wewe polisi; haiwezekani. Kwa hiyo, hoja hiyo Wenyeviti na Mameya kusaini mikataba ya Halmashauri naona siyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, penye kukosoa lazima tusifie. Sisi tumetembea kama Kamati, tumekwenda Halmashauri ya Wilaya ya Newala, tumezungukia Miradi yake yote ni mizuri. Mkurugenzi wa Wilaya ya Newala anastahili pongezi na tulimpa pongezi, kwa sababu anafanya kazi kwa viwango. Tumetembelea Miradi mingi, tumekuta kweli thamani ya fedha ipo. Sasa siyo wote ambao wanafanya mambo ndivyo sivyo, penye kusifia lazima tusifie na tunapotaka kukosoa basi Serikali ichukue hatua haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, baadhi ya Miradi haianzii kwa Wananchi au haiwahusishi Wananchi. Tumekwenda Wilaya ya Ruangwa, katika Kijiji

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DUNSTAN D. MKAPA]

cha Mkowe, tumekuta kuna Mradi wa Umwagiliaji Maji pale, Wananchi hawakushirikishwa tangu mwanzo wameugomea, lakini tayari shilingi milioni 41 zimeshatumika. Sasa hii ni hasara kwa Serikali. Ushauri wangu ni kwamba, Miradi hii iwashirikishe Wananchi tangu mwanzo waikubali ndipo ianze kufanyika.

Mwisho kabisa, niseme kwamba, jamani, tumethubutu, tumeweza na tunasonga mbele. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mengi kwa Taifa hili na ninyi mnaobeza labda hamwelewi historia ya nchi hii. Ninawaambieni kwamba, Serikali yetu imejitahidi sana katika maendeleo ya nchi hii. Halmashauri zetu zimeboresha mambo mengi sana, lakini kuna watu wachache na kuna Viongozi wachache ambao wanaharibu na hao wamekuwa wakichukuliwa hatua mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Paul Lwanji na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, ajiandae.

MHE. JOHN P. LWANJI: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Awali ya yote, nawashukuru Wenyevitwa wa Kamati hizi tatu, kwa Taarifa zao ambazo wameziwasilisha humu ndani. Ninasema kwamba, ni Taarifa nzuri na imetupa nafasi ya kuweza kuzijadili kwa mapana na marefu. Mengi yamesemwa, lakini na mimi nitachangia kwa jumla tu.

Mheshimiwa Spika, mijadala iliyopita ilipaswa kutujenga tuishauri Serikali namna ya kuweza kurekebisha matatizo yaliyooneshwa katika Ripoti hizo. Badala yake ilikuwa imeonekana kama inataka ku-*paralyze* Serikali. Hatuwezi kukubali tufikie hapo, kwa sababu matatizo ndiyo sehemu ya shughuli zetu. Hizi Kamati ziliundwa kwa ajili ya kwenda kuchunguza, kuona kama shughuli zinakwenda vizuri au vipi. Sasa zinapoleta Ripoti zake, basi tuchangie katika utaratibu wa kujenga.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI]

Mheshimiwa Spika, historia ya Halmashauri au Serikali za Mitaa, ni vyema tufahamu; wakati wa Uhuru tulikuta Serikali za Mitaa. Mwaka 1961 tukavunja Utemi. Ule Utemi ulikuwa ni kwa sababu tulitaka tujenge Umoja wa Kitaifa, lakini baadaye lilikuwa jambo zuri tu na mimi ukoo wangu ulikuwa wa Mtemi, labda ningeweza kuwa Mtemi leo, lakini ili tuweze kujenga Umoja wa Kitaifa tulikubali na lilikuwa jambo zuri tu. Ilipofika mwaka 1972, ni lazima tukiri kwamba, tulikosea kuvunja Serikali za Mitaa pamoja na Vyama vya Ushirika.

Kwa wale waliokuwepo wakati huo, hawapigi makelele sana kwa sababu wanaelewa historia yao. Kwa wale ambao walikuwa hawajazaliwa ndiyo wanaopiga makelele sana humu ndani. Mwaka 1972 ilitangazwa kwamba zinavunjwa na sisi wengine tulikuwa vyuoni tumeandaliwa kwa ajili ya kwenda kuendesha hizo Halmashauri, lakini zikavunjwa baadaye tukawa Mabwana Shauri (*Administrative Officers*). Kwa hiyo, tulikosea hapo.

Mheshimiwa Spika, jengo kama hili unapolivunja au likiungua moto, Mungu aepushie mbali, halichukui muda na magari ya zimamoto yasipowahi kufika hapa, jengo hili kwa muda wa saa mbili au hata saa moja, litakuwa limeteketea lote, lakini kujenga sasa, hapo ndiyo tatizo. Kuja kuliinua jengo hili mpaka lifikie hali ilivyo sasa hivi ni kazi kubwa na ndivyo ilivyotokea kwenye hili suala la Halmashauri zetu. Mwaka 1972 tulizivunja, tulipoona tumekosea tukarudi 1983 tukaanza kujenga upya. Sasa si kazi ndogo ndugu zangu, ni kazi kubwa. Lazima mlielewe hili, siyo kazi ndogo na kumbukeni kabisa kwamba, Halmashauri zetu hizi bado zina tatizo la kupokea fedha za kutosha.

Bajeti nzima ya Serikali ni asilimia 25 tu ndiyo inayokwenda kwenye Halmashauri zetu. Mnapaswa kulielewa hili na mazingira magumu ambayo wenzetu wanafanyia kazi. Sikusimama hapa kutetea uozo, hapana, mabaya lazima yaainishwe na yachukuliwe hatua. Lazima tukubali kwamba, kuna mazuri pia, sasa mabaya yasifunike mazuri. Kwa hiyo, ningeomba ndugu zangu tulielewe hili na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI]

muelewe kabisa kwamba, tumetoka katika mazingira magumu ya dunia tofauti kabisa, kuliko dunia iliyopita ya Madikteta na nini. Sasa hivi tunapaswa kujenga Utawala Bora, Utawala wa Sheria.

Watu wamepelekwa Mahakamani na Mhimili ule mwingine mnauachia kwa sababu aidha wananunua haki au pengine taratibu zetu katika kutoa haki hiyo hazifuatwi sawasawa wanarudi, tena kibaya zaidi wanarudi makazini. Sasa hii lawama ichukue Wizara ya TAMISEMI, haiwezekani, ni lazima tuangalie mfumo mzima, sheria zetu hizi tuzirekebishe. Tunaposema tuwafukuze, ni dhahiri kabisa kwamba, tutawafukuza na hakuna tutakachopata. Mimi nilidhani hizi sheria zingerekebishwa ili pale wanapobainika, basi sheria ziseme wazi kwamba, wafilisiwe wafidie kile ambacho wamechukua.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, nimetembelea Miradi kadhaa katika Halmashauri zetu. Zamani tulikuwa tunahofu kwamba tutakuta Miradi hewa na ndivyo ilivyokuwa, unakuta Miradi imeandikwa kwenye vitabu na imepitishwa, lakini mkienda kwenye *site* hakuna Mradi. Iliwezi kutokea mara kadhaa, lakini sasa hivi tume-*shift* hapo kuna *development*. Huwezi kutegemea kwamba utakwenda kukuta Mradi, sijui itakuwa ni kwa nadra sana, lakini unaikuta Miradi.

Sisi tumetembelea Arusha, tumetembelea Kilimanjaro hivi karibuni na tukafanya *random check* tu ya Miradi hiyo. Tukasema jamani hebu tunataka tuone Miradi yenu. Tunakuta wametupangia kwamba tutakwenda kuona Mradi huu na huu. Sisi pale pale kwenye kikao kabla hatujatoka, tunageuza tunasema hatuwezi kwenda kuona Miradi ambayo mmetupangia ninyi. Ninyi mmetupa taarifa, sasa katika taarifa yenu tutachagua hiyo Miradi tutakayokwenda kuiona.

Kwa hiyo, kama kulikuwa kuna miradi 20, sisi tunachukua Miradi saba au nane kulingana muda tulionao katika Halmashauri hiyo, tunakwenda tunaangalia, maana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI]

tunapokuwa kwenye Kamati tuko wa vyama vyote. Kweli tumeshuhudia Miradi ipo na kwa asilimia kubwa. Kwa mfano, tulipokwenda kwenye Manispaa ya Moshi, Miradi yao ilikuwa imekamilika vizuri tu. Sasa sisi tuna *function* nyingine na wenzetu wa LAAC mahesabu huko ni kivyao vyao jinsi walivyoandika vitabu vyao, lakini sisi tunataka kuona *value for money on site* na tumeona. Ndugu zangu tumeona na malalamiko makubwa ni kwamba, kama Serikali ingetoa fedha kwa wakati, Miradi hiyo ingekuwa inakamilika yote kwa wakati. (*Makofi*)

Tatizo letu ndugu zangu ninyi mnaopiga kelele, mnauchukia Mwenge, lakini kipindi cha Mwenge huwa ndiyo kipindi kizuri sana cha kuweza kutathmini Halmashauri zote zimefanya nini. Kipindi hicho Miradi mingi iliyotekelezwa huoneshwa. Kwa wakati huu pamoja na Wananchi kuchangishwa, ni wakati ambao Halmashauri imetekeleza Miradi mingapi na Miradi ipi, tunaiona. Kwa hiyo, ndugu zangu ninaomba tujenge, hatua hii tuliyofikia siyo haba. Mwaka 1983, leo ni mwaka 2013, ni takriban miaka 30. Historia ya Halmashauri za Serikali za Mitaa imeanza miaka mingi sana toka Mkoloni aanze kutawala nchi hii. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri tu. Wenzetu wanaofanya kazi katika maeneo hayo, wanafanya katika mazingira mazuri sana. Mkurugenzi analipwa shilingi ngapi ndugu zangu? Ninafahamu mshahara wa Mkurugenzi, lakini nitataja kwa kifupi, ni milioni mbili na ushee kidogo, mpaka anapokuja kukatwakatwa mwisho anabaki na milioni moja. Sasa Serikali itazame eneo hili, hawa watu wanasimamia mapesa mengi.

Ndugu zangu, mimi ningeliomba sana, sijui kuna Tume ya Mishahara na nini, lakini hawa watu wapewe mshahara ambao hata kama ana tamaa, basi iwe ni tamaa zake mwenyewe, lakini asishawishike kwa sababu ya mshahara. Maana *status* aliyonayo katika Wizara anayohudumia ni kubwa, yeye ni mtu wa pili kwa DC na unampa nyumba *Grade A*, gari na kila kitu, lakini mshahara hamna. Mshahara wa ajabu sana katika kipindi hiki. Kwa hiyo, matatizo kama hayo yaangaliwe na kama nilivyosema, hizo sheria zetu tuzihuishe ili wale watakaokuwa na tamaa,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN P. LWANJI]

basi tuwashughulikia ipasavyo, tuwafilisi ili waogope, badala ya kusema tuwapeleke mitaani, tuwafukuze au tuwaweke sehemu nyingine, wapewe adhabu inayostahili.

Mheshimiwa Spika, kuna wazuri na wabaya katika Halmashauri zetu. Toka wiki iliyopita tumewatangazia hali ya hatari. Sasa watu wale wanafanya kazi kwa wasiwasi kwamba ukikosea kidogo, hata ukihisiwa kama Mke wa Mfalme, basi wewe ufukuzwe tu. Sasa yule mtu hawezi kupanga mipango yake ya kuiba kweli! Lazima kauli zetu zingine tuziangalie, kwa sababu tunaweza tukawachochea watumishi wakafanya mambo ambayo pengine wasingefanya kama tusingewazungumzia.

Mheshimiwa Spika, juzi tulikwenda Uingereza tukakutana na hiyo Kamati ya upande huo ya TAMISEMI kama ya kwetu hapa, wana matatizo kama haya haya. Uingereza nako ni matatizo kabisa. Wale watu waliotutawala wakaweka mambo hayo ya *Local Government* na nini, wana matatizo mpaka leo, mpaka *Her Majesty the Queen* ameunda Tume watu wanaenda pale kueleza matatizo ya Halmashauri zao. Kwa hiyo, sidhani kama tuko pabaya, nadhani tuko pazuri tu. Siku zote tunalalamika hapa kwamba, Serikali haina meno. Sasa Serikali inapochukua hatua, tayari tena tunageuza, Serikali ya Kidikteta, Serikali haina huruma! Juzi tu Operesheni Tokomezwa imeleta kizaazaa hapa, lakini nia ilikuwa nzuri kabisa ya kuhakikisha wanyama wetu wanalindwa na nini. Serikali haiwezi kufanya kazi katika mazingira ya namna hiyo; mkifanya hivi, kibaya. *Architect* wa Serikali ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, huyu huyu Mheshimiwa Pinda, ndiye Waziri aliyekaa sana katika Wizara hii na amefanya mengi. Leo uje useme kwamba, aondoke kwa sababu ya Taarifa hizi, *we are not serious at all!*

Mheshimiwa Spika, nadhani tupo pazuri tu. Ushauri ni kama nilivyosema, ni sisi kuhuisha Sheria zetu ziweze kuwabana hao watu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, atafuatia Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, atafuatia Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha leo hii kusimama hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa heshima ya pekee kabisa, kuzishukuru Kamati zetu zote; Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma na Kamati yetu ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati hizi zinafanya kazi kwa niaba ya Bunge letu na Taarifa ambazo zimeletwa ni za Bunge. Nina imani kwamba, Taarifa hizi ni sahihi na cha kufanya sasa ni kuboresha na kupeleka miongozo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hizi zilijadiliwa toka tarehe 6 Desemba, 2013. Nimeangalia kwa makini michango ya Wabunge mbalimbali, lakini tathmini niliyoifanya ya michango yote ya Wabunge, wamethibitisha kwamba, Serikali kupitia Wizara zake zote, imeshindwa kusimamia matumizi mabaya ya fedha za umma. Hii imethibitishwa zaidi na Taarifa za Msimamizi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika Vitabu vyake vyote viwili vya LAAC na vya Hesabu za Serikali Kuu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hawakusema hapa kwa ku-*provoke*, walikuwa wanasema wakiwa na *data* ambazo zimeandikwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, wale wote ambao wanasema labda walikuwa wanazungumza tu, walikuwa wananukuu mambo ambayo yamefanyiwa kazi na hiyo ndiyo kazi yetu, kuikosoa Serikali na kuhakikisha inarejea nyuma kuleta maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaiasa Serikali kwamba, tunapozungumza hasa upande huu wa Upinzani, tunakuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RASHID ALI ABDALLAH]

na mambo muhimu sana, msiyabeze mambo haya, myachukue na myafanyie kazi. Hatuwezi kupata maendeleo yaliyo kamili katika Taifa hili bila ya kuwa na fedha. Tegemeo la Watanzania walio wengi ni Halmashauri zetu. Halmashauri nyingi zimelalamikiwa kwa ubadhirifu wa Fedha na Kamati hii ya LAAC imesema kwamba, kuna ufisadi wa hali ya juu. Mimi hii hali ya juu imenipa mashaka kweli. Hali ya juu *to what extent?* Ipo juu vipi? Kuna ubadhirifu wa hali ya juu. Imeendelea kusema kwamba, kuna utovu wa nidhamu wa matumizi ya fedha za umma wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, Idara hii ipo chini ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu na Msimamizi Mkuu wa Shughuli zote za Serikali. Hii ndiyo picha. Wizara zingine zilizopo nyuma zitafanya nini kama Waziri Mkuu amekalia uchafu huu? Mimi simlaumu Waziri Mkuu, ninachokilaumu ni Utawala Bora. Wizara ya Utawala Bora imeshindwa kufanya kazi zake. Hatuendi hata siku moja Mfanyakazi wa Halmashauri akaambiwa na Mkguzi Mkuu wa Fedha za Serikali apeleke vitabu vya ukaguzi na akashindwa kuleta vitabu vya ukaguzi. Huu ni Utawala Bora haufanyi kazi zake. (*Makofi*)

Hatuwezi kabisa Halmashauri zilizokaguliwa 14 na Mkguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kukawa na *shortage* ya bilioni 15 na zaidi kwa mambo mbalimbali. Huu ni upungufu wa Utawala Bora. Huwezi hata kidogo ukaambiwa fedha yako uliyopangiwa na bajeti ni kiasi fulani, Halmashauri zimetumia zaidi ya bilioni moja nje ya bajeti. Wameambiwa na nani hawa watumie hizi fedha? Hizi fedha si za kwao. Fedha Bunge linakaa linapanga bajeti kwa mujibu wa mahitaji tuliyonayo. Leo wanatokea Wafanyakazi wa Halmashauri wanatumia zaidi ya bilioni moja bila ya idhini!

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu katika Taarifa ya CAG, ilihamisha shilingi 113, 150,141 na shilingi 2,482,366,765 kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa matumizi ya ofisi. Hadi kufikia mwisho wa mwaka, Taarifa za Fedha zinaonesha hakuna bakaa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RASHID ALI ABDALLAH]

yoyote ya fedha. Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma ilionesha kwamba, kuna bakaa ya shilingi milioni 660 na katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kulioneshwa kuna shilingi milioni 844. Hizi fedha mwisho wa mwaka hakuna ripoti katika Ofisi Kuu ya Waziri Mkuu. Hizi fedha zilikuwa na malengo gani? *Inference* inatuonesha kwamba, fedha hizi zilikuwa *target* ya kuweza kutumiwa vibaya. Hii tunarejea kulekule kwamba Wizara ya Utawala Bora haifanyi kazi hata kidogo. Kuna haja kabisa ya kufanya *big reformation* Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hebu niangalie vitabu ambavyo havikuwasilishwa kwa ukaguzi, tena huu ni mchezo toka mwaka 2007/2008, kuna vitabu 860 havikwenda kwenye ukaguzi; mwaka 2008/2009 kuna vitabu 1,341 havikwenda kwenye ukaguzi; mwaka 2009/2010 kuna vitabu 944 havikwenda kwenye ukaguzi; mwaka 2011/2012 kuna vitabu 2,990 havikwenda kwenye ukaguzi. Hivi vitabu una uhakika vilikuwa na kiasi gani cha fedha za umma; ni hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa ya kuangalia utaratibu mpya wa kuweza kuzilinda fedha za umma na kutumika kwa utaratibu ambao umewekwa. Mimi nashauri, kitu cha kwanza, tuboreshe Ofisi za Utawala Bora. Aliyetufikisha hapa, wizi wote wa fedha, ubadhirifu na utovu wa nidhamu ni Wizara ya Utawala Bora, kabisa, hana uwezo wowote wa kujing'amua na suala hili. Wewe kama mtumishi unakwenda kuiba kwa misingi ipi?

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo napenda kuishauri Serikali, ufanywe ukaguzi wa haraka haraka, tusikae sana. Wizara ya Utawala Bora ikiwa vizuri, nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali itakuwa nzuri. Matumizi ya fedha za Serikali yatakwenda mahali panapohusika na kwa maana hiyo tutarejesha matumaini ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matumaini ya Watanzania katika kauli zilizotolewa na Wabunge, yamepotea njia na hayana mwelekeo. Kuna haja Serikali hasa Waziri Mkuu, kusimama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RASHID ALI ABDALLAH]

makini na kumshauri Rais kwamba, Wizara ya Utawala Bora bado haijafanya kazi zake. Mimi ninaendelea pale pale, Utawala Bora kwa tafsiri ina kazi nzito katika Taifa hili. Kwa hiyo, yafanywe marekebisho ya hili halafu kuwe na kaguzi za haraka haraka katika maeneo mbalimbali ili kuweza kudhibiti wizi wa fedha hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya ajiandae.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia na kitu ambacho kinanipa nafasi ya kufanya kazi hii ya Ubunge, ambayo kwa sisi Wanaharakati wa Usalama Kazini, naweza kusema sasa hivi imeshaingia kwenye kundi la ajira hatarishi. Kwa sababu toka nimekuwa Mbunge katika kipindi cha miaka mitatu, nimekamatwa mara nyingi na Polisi kuliko nilivyokamata miaka 20 ambayo nilikuwa mtaani ninapiga muziki. Inabidi tufanye hivyo na tutaendelea kukomaa na ndiyo maana huwa tunakuwa wakali sana tunapoonu mtu yeyote analeta mchezo katika *movement* yetu, awe kiongozi, awe mwanachama wa kawaida. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nami niongelee kidogo juu ya masuala ya Halmashauri. Halmashauri zetu matatizo siyo Wakurugenzi na Watumishi, kuna tatizo kubwa sana la Wenyeviti wa Halmashauri na Mameya, ambao ni *cruel* wakubwa, wezi wakubwa, wana *mentality* za ki-*cruel*, wana ubabe, wanaendesha Halmashauri kibabe, hawaitishi vikao kwa wakati unaotakiwa. Madiwani wakijaribu kufuatilia, wanaendesha kibabe kama alivyo Meya wa Mbeya Mjini; hataki vikao na ubabe wake ndiyo uliochangia kwa kiasi kikubwa, vurugu za Wamachinga mwaka 2011. Mpaka leo tunataka Tume ije ifanye uchunguzi ili tujue tatizo, lakini hakuna kinachotokea kitu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPH O. MBILINYI]

ambacho kinampa kichwa Meya huyu na kuzidi kufanya vitendo vya ubabe na hili nina uhakika Serikali mnalijua hata Waziri Mkuu analijua kwamba, tatizo la maendeleo ya Mbeya ni Meya wa Mbeya Mjini.

Mheshimiwa Spika, Meya analeta ubabe kwenye Vikao vya Halmashauri, anafikia hatua ya kutamka Madiwani wa CCM kwanza hawa wa CHADEMA wapo kidogo wachapeni wapigane na ngumi zinapigwa, wanaiga ya Bungeni. Meya kwenye Halmashauri ya Jiji kama Mbeya na sababu ya kufanya hivyo ni kwamba, Madiwani wanahoji mamilioni ya fedha ambayo Meya na Mkurugenzi wametumia kwenda safari ya China kinyume cha utaratibu. Watu wanataka kujua umetumiaje zaidi ya milioni 70 kwa safari ya China wakati tunahitaji milioni 16 tu ili kumwaga lami nyepesi kwenye eneo la soko ili Wamachinga ambao wamekubaliana na sisi Viongozi kwamba pale mkituwekea lami nyepesi tutakubali kuhamia pale na kufanya shughuli zetu. Leo hii mnasema hakuna milioni 16 za kwenda kufanya hiyo kazi, halafu ghafla *from nowhere* mnachukua zaidi ya milioni 70, Meya na Mkurugenzi. Kama Mheshimiwa Msigwa alivyosema jana ukiona Meya na Mkurugenzi wapo sambamba hawagombani, hawana mgogoro, ujue kuna jambo nyuma linaloendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena, ukiona Meya kama yule wa Mbeya alimshambulia sana yule Meya, maana mpaka nikawa ninauliza Viongozi yule Mkurugenzi wa mwanzo mmempeleka wapi, mmemwondoa ghafla bila tamko, wanasema usijali yule kapandishwa cheo. Hata kama amepandishwa cheo mtu-*consult* sisi, tulikuwa tunamhitaji bado afanye kazi za Mbeya pale. *Regardless* mnasikiliza majungu ya kisiasa na mnaangalia namna ya kuondoa watu katika maeneo bila ku-*consult* Viongozi wa watu ili kujua kwamba mahitaji ya yule Kiongozi au yule Mtumishi yapo vipi pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa huyu ameleta majungu, ooh yule CHADEMA, yule nini, sasa hivi amekuja Mkurugenzi hata bado hajatambulishwa kwenye Baraza la Halmashauri,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPH O. MBILINYI]

wameshachukua zaidi ya shilingi milioni 76 kwenda China. Hata hajaja kutambulishwa kwamba jamani huyu ndiye Mkurugenzi wetu mpya, wameshaanza kupiga vitu. Sasa Mameya kama hawa hawawezi kufanya Halmashauri na niseme wazi na ninampa pole sana Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, kwa mapokezi hasi aliyoyapata Mbeya. Ile ndiyo Mbeya, ila ninamuunga mkono kwa kauli yake aliyoitoa Mbeya kwamba, CCM Mbeya wanatakiwa kutuomba radhi Wanambeya kwa kutucheleweshea maendeleo. Ninamuunga mkono kwa hilo. Wa kwanza kutuomba radhi kutoka CCM anatakiwa awe Meya wa Mbeya Mjini kwa aliyoyafanya pale. (*Makofi*)

Wewe huwezi kuchukua hela unaenda sijui kwenye shughuli gani wakati sisi pale tuna matatizo. Sawasawa na mzazi uchukue hela ukatoe mchango wa harusi wakati mtoto wako kafukuzwa shule kwa ajili ya ada! Hii itawezekana vipi unachukua hela unakwenda kuchangia harusi ya rafiki wakati una mtoto wako yupo nyumbani anafukuzwa shule kwa ajili ya ada. Haya mambo hayawezekani na kwa *style* hii Halmashauri haziwezi kuendelea hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hawa Ghasia atakuja kujibu, ushauri wangu kwa dada, jibu kama mahitaji ya hoja zetu yanavyotakiwa. Watu wanakusema sana, wanasema unajibu kijeuri, wanasema sijui una uhusiano na Mke wa Rais ndiyo maana unajibu hovyoy. Sasa leo ni nafasi ya wewe kurekebisha ili watu wote waone kwamba wewe unatenda haki na unaisimamia hiyo Wizara kwa masilahi ya Taifa na siyo kwa masilahi binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye Mashirika ya Umma, nirejee masuala ya madeni ya *PSPF, NSSF, PPF* na *LAPF*. Kwanza, ifike mahali Serikali ilipe haya madeni kwa sababu hao nao wanaweza wakaanza kushindwa kusoga mbele ipasavyo, kila saa wanasema kuna madeni ya Serikali, kuna madeni ya Serikali. Pili, hawa watu sasa wabadilike, wabadilishe kwenye aina ya uwekezaji, wawekeze katika masuala yenye faida kwa Wananchi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPH O. MBILINYI]

husususan Wanachama wao ambao kimsingi ndiyo Wafanyakazi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, wawekeze katika nyumba za wafanyakazi, kusafiri ni kujifunza, maana yake kweli Wananchi wanasema mnasafiri sana, lakini kusafiri kama unajifunza haina tatizo. Mimi nimeanza kusafiri juzi tu, unafika baadhi ya sehemu unauliza hivi hii nchi sisi ndiyo watu wa kwanza kufika hapa? Wanakwambia hapana, Mawaziri wanashinda hapa, Balozzi anakwambia jana nilikuwa na Waziri fulani na mkiondoka ninyi anakuja Waziri fulani. Sasa hawaoni haya mambo?

Zamani nilikuwa naenda Marekani na Ulaya, nika-*exempt* kwamba aah watu ni historia ya miaka 200, hawa watu ni historia ya miaka, lakini unaenda Malaysia unakutana na historia ya kuanzia mwaka 1981 kuja huku. Unakutana na dereva taxi anasifia anakwambia *you see this picture, this street it was like this in 1980*, kila mtu yupo *proud* na nchi yake. Sisi tunakwenda, tunaona, tukirudi tukifika pale *VIP* uwanja wa ndege tunafunga mdomo tunaona aibu kusema kwa sababu hatutaweza kutekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashindwa kutekeleza vitu vidogo vidogo kabisa. Tumekwenda kutembelea Kampuni moja tena Kampuni binafsi hata siyo Kampuni ya Umma, tukakuta wale jamaa wana *project* ya Mradi wa Nyumba Vijijini. Nyumba moja inagharimu dola 10,000, lakini ukiiona hiyo nyumba, nitakuleta picha sijaja nazo zipo kwenye simu. Ukiiona hiyo nyumba ni ya Masaki na ni dola 10,000 tu. Dola 10,000 ni shilingi 16,000,000 ya Tanzania. *Let say* tufanye shilingi milioni 20 tujenge nyumba kama hiyo, kwa sababu huku *labour* ipo chini.

Kwa hiyo, kama kule ni shilingi 16,000,000 lazima huku itashuka kidogo kutokana na gharama zingine. Tuseme haya, huku iwe shilingi 20,000,000. Ukimkopesha Dokta nyumba ya shilingi 20,000,000 ya *style* na kama mshahara wake ni shilingi 800,000 umwambie alipe riba ya shilingi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPH O. MBILINYI]

200,000 kwenye ile nyumba, inamchukua miaka sita tu kumaliza deni la nyumba ya shilingi 16,000,000 na nyumba nzuri imenyooka kabisa.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu nyumba kama ile ukiuliza bei gani, utaambiwa shilingi milioni 80 na mambo yote nini; Sheria ya Manunuzi. Hiki kimepita huku, kile kimepita kule, kitu cha milioni tano unakuja kuambiwa hiki kitu ni milioni 50, milioni 60 na watu tumekaa. Sasa unajuliza ni nini faida ya kusafiri?

Hawa watu wa Mashirika Wakurugenzi wote wanasafiri na wanaona. Ifike wakati sasa tuache kuwekeza kwenye *skyscrapers*, *regardless* yana *ten percent* nzuri kiasi gani. Tuangalie tija, kwa sababu mimi nina uhakika nyumba zile ukiwapa hawa Madaktari wetu, hata Walimu, kama Mwalimu ana mshahara wa 300,000, 400,000, amwambie hii nyumba nzuri ya kisasa nakupa utalipa shilingi 200,000 kwa mwezi, atafundisha *tuition*, atalima mchicha, vitu ambavyo anafanya sasa hivi *anyway*, lakini kwa wakati huo atakuwa na faida kwamba analipia nyumba ambayo anaimiliki na baada ya miaka sita, miaka kadhaa, inakuwa imeshakwisha.

Mheshimiwa Spika, ninachosema *Big Results Now has become a big joke now*. Walimu wana-joke, wanatuma *message* za *jokes* wanasema *Big Results Now without Big Salary Now is a Big Problem Now*. Hivi ndivyo wanavyotuma *message* Walimu; kwa sababu tunakwenda tunaangalia hatujifunzi, tukirudi hapa tunafunga mdomo. Sasa ile hatuwezi kwenda. Tunajidai kuiga mambo makubwa, tunaiga vitu vikubwa kwamba sijui tutaleta teknolojia, sijui kila kijiji kitakuwa na *internet*; wapi umeme hakuna. *Internet* itakuwa katika kila kijiji wakati umeme hakuna!

Mheshimiwa Spika, tuige vitu vinavyowezekana. Tukienda China tujulize hawa Wachina wamefanikiwa kwa sababu gani? Wamefanikiwa kwa sababu ya kupambana na adui namba moja wa maendeleo ambaye ni rushwa. Kivipi, toa *capital punishment*, mimi siyo mshabiki wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPH O. MBILINYI]

capital punishment, lakini toa adhabu kali, fungua mtu maisha. Angalia China, mtu kama Bo Xilai, kwa wanaofuatilia siasa za Kimataifa, Bo Xilai alikuwa ndiye mtu aliyepo kwenye *ranks* za juu, alitajwa kuwa Rais wa China anayefuata kabla ya Xi Jinping, ambaye tumempokea juzi. Kwa maana hiyo, bila ile *scandal*, juzi tulipompokea Xi Jinping, tungekuwa tumempokea Bo Xilai, lakini kama miezi sita au mwaka mmoja kabla akabugizi akala rushwa, kakamatwa kawekwa kizimbani, sasa hivi kafungwa maisha na alikuwa mtu ambaye anatarajiwa kuwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hapa mtu anatajwa, akitaja ndiyo anategemea kuwa Rais hata gamba litashindwa kuvuka. Tunaweza kumpeleka mtu jela, fungeni watu tafadhali. Fungeni watu, kwa mfano, wafungeni vifungo virefu ili tukae kwenye mstari. Vinginevyo, tutakaa tu tunapiga hili, tunapiga lile, lakini nadhani sababu ambayo inatufanya sisi au ninyi ambao ni watawala mnajiita Serikali ya CCM, Serikali ya CCM, kinachowafanya mshindwe kuchukua hatua ni kwa kuwa nyote mna mawaa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa kweli utuombe radhi wote kabisa. Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya! (*Kicheko*)

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kidogo katika Ripoti hizi tatu za Kamati.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya niweze kusimama mbele yako. Napenda niseme kwamba, tunapongelea upungufu uliopo ni kwamba, tunataka yafanyiwe kazi, siyo kwa sababu labda ni Wapinzani au tunataka kuitukana Serikali au vyovyote vile au kazi yetu ni kupinga tu. Tunapongea tunakuwa na *data* kamili ambazo tumezipata kwa msaada wa CAG ambaye amelipwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema lolote, napenda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

niseme kwamba, Serikali hii saa nyingine ninaifananisha na mzazi ambaye anafanya vibaya darasani. Anampa mwalimu pesa amfanyie *assessment* ya mtoto wake, mwalimu anamwambia mtoto huyu haingii darasani ni mtoro, hasikilizi walimu, hafanyi *home work*, wala hayuko *serious* na masomo yake. Mtoto anaendelea kufeli kumbe mzazi aliweka ile *assessment* ya mwalimu aliyompa bila kuifanya kazi; ndivyo ninavyoona sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimetoa mfano huo rahisi ili Wananchi waweze kuelewa, mengi yameongelewa hapa na Wabunge mbalimbali kuelezea matatizo ambayo yanaonekana katika Serikali hasa baada ya Ripoti hizi tatu kutolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba ni-*declare interest*, niliwahi kuwa Mjumbe wa *PAC* na sasa nimekwenda *LAAC*. Matatizo mengi naona yanafanana. Tatizo kubwa sana ambalo ninaliona ni usugu wa Serikali kutofanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na *CAG*, Kamati zetu na ushauri ambao unatolewa na Bunge kupitia Kamati za Kisekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Ripoti yetu ya mwaka jana ya *LAAC* ina mapendekezo 14 ambayo Serikali haijayafanyia kazi hata moja. Ukiangalia *trend*, toka 2005 mimi nimekuwa ndani ya hili Bunge, matatizo ni hayo hayo, yaani Serikali ina ule usugu wa kutopitia mapendekezo ya Kamati, wala Maoni, Ushauri na Ripoti za *CAG* na kuzifanyia kazi. Ndiyo maana tunajikuta tunaongea vitu ambavyo vinajirudia kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo ambalo lipo katika Halmashauri zetu. Tulienda kwenye Halmashauri ya Shinyanga, tukaangalia Ripoti zao bado walikuwa na hoja za toka mwaka 2009. Walipewa hoja kumi, walishajibu sita, toka mwaka 2009 mpaka leo hawajazimaliza. Majibu mengine sijui kwa nini hawana! Hilo ni suala ambalo tunafikiri katika mambo ambayo tuliyaona, tuligundua kwamba, kuna ubadhirifu mkubwa sana kwa upande wa Serikali za

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

Mitaa. Sasa wanakuwa hawana majibu ya kutosha ya kujibu, labda ndiyo maana Serikali nayo inakuwa haiwezi kujibu kwa sababu haina majibu ya kutosha, kuna huo ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, maeneo sugu ambayo yalibainishwa na Kamati yangu ya LAAC ni kwamba, Bajeti ya Maendeleo haitolewi vya kutosha kama ilivyopitishwa na Bunge. Kwa mfano, kwa Ripoti ambayo tulikuwa tunaifanyia kazi ya mwaka 20011/2012, ruzuku ya maendeleo ambayo ilitakiwa iende kwenye Halmashauri 113 iliyoombwa shilingi 595,064,422,505, lakini kiwango ambacho kilitoka ni shilingi 345,568,067,477. Kiasi ambacho hakikutoka ni *almost* nusu ni shilingi 249,496,355,000. Sasa utaangalia, hii inamaanisha kwamba, kuna baadhi ya Miradi haikutekelezeka na mingine imetekelezeka nusu. Upungufu huu unaonekana ni kama asilimia 42, yaani tunakaribia nusu. Kwamba, pesa zinaidhinishwa ndani ya Bunge lakini hazitolewi; hiyo maana yake Miradi haitafanyika au haitaisha.

Mheshimiwa Spika, juzi tarehe 6 Desemba, 2013 kama pia ukienda nyuma kwenye Bajeti kuanzia mwaka 2007/2008, kwa mujibu wa *Report* hii ya CAG, utaona Ruzuku ya Maendeleo inayotolewa kwenye Halmashauri haijafikia hata asilimia 45. Kuna asilimia 36 mwaka 2007/2008. Asilimia 34, 36 na mwaka 2010/2011 na 2011/2012, bado tupo kwenye hiyo asilimia 42 tu ya utoaji wa ruzuku.

Juzi wakati wa maswali, tarehe 6 Desemba, 2013 kulikuwa kuna Swali Na. 51 la Mheshimiwa Neema Mgaya, yeye alitaka kujua kwa nini pesa za Maendeleo hazitolewi katika Halmashauri zetu kama zilivyoombwa. Alitaka kujua tatizo hilo litakoma lini na tatizo la msingi ni nini. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, alisimama akajibu vizuri tu, akasema kwamba, tatizo tunategemea sana Wafadhili na pesa hizo zina masharti, wakati mwingine haziji zote au zinakuja nusu. Sasa mimi ninasema, kama tatizo linajulikana, ninaomba Serikali ituambie ina mikakati gani sasa ya kuanza kutumia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

vyanzo vyetu vya ndani angalau tuanze kujitegemea kidogo kibajeti?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika *Report* ya Kamati ya Bajeti, wanashauri tujitahidi kutumia vyanzo vyetu vya ndani angalau kwa asilimia 35 ili tuweze kutimiza Miradi yetu ya Maendeleo, ili iende sambamba na Mpango wetu wa Miaka Mitano. Ninataka kujua *Big Results Now* tunaipataje kama hatuwezi kutekeleza Miradi na kama hatuna uwezo wa kujitegemea wenyewe; ni *slogan* tu ya kutufurahisha au ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika *Report* ya PAC, wameelezea kwamba, toka 2007/2008, Serikali imeanzisha Mpango wa Umeme Vijijini. Lengo lake lilikuwa kumkomboa Mtanzania maskini ambaye yuko pale kijijini ili naye aweze kupata umeme na inawezekana labda wakaweza kuzalisha vizuri zaidi wakiwa na umeme kwa kuanzisha hata viwanda vidogo vodogo. Kinachosikitisha, kwa kipindi chote hicho pesa hazijawahi kutolewa zaidi ya asilimia 50. Hata ukiangalia Taarifa iliyopita ni asilimia 47 tu ndiyo iliyotolewa. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, itabakia kuwa ndoto kwamba tutapeleka umeme vijijini bila kuwa na fedha. Wameshauri kwamba, tuangalie uwezekano wa kutumia vyanzo vyetu vya ndani ambavyo ni rahisi kuvifikia kuliko kusubiri pesa za Wafadhili ambazo zina masharti mengi. Nataka kujua sasa tunajikwamuaje katika haya matatizo ili tuweze kupata hiyo *Big Results Now*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Report* kwa mfano ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, imeonesha kwamba, upo utaratibu wa Halmashauri zetu kukusanya pesa kwa niaba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, lakini bahati mbaya sana hawarudishiwi ile asilimia 20 ambayo ingeliweza kusaidia sana katika mapato ya Halmashauri. Katika Taarifa ya PAC, ukurasa wa 24 na Kamati ya Bajeti ukurasa wa 30, wanaonesha pia Wizara hii ya Nyumba, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ingeliweza kukusanya vizuri mapato yake, ingeongeza kipato fulani na tukaweza kuchangia na kupunguza utegemezi. Vilevile

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

Wizara ya Maliasili na Utalii bado nayo haijaweza kukusanya vizuri mapato yake, pamoja na kwamba inavyo vyanzo vingi vya mapato.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, bado wanalegalega katika kutumia *visa sticker* kupata mapato. Matatizo yaliyopo ni kwamba, *sticker machines* nyingi ni mbovu. Sasa tunashindwa kuelewa; ina maana Wizara haina uwezo wa kupeleka mafundi wakatengeneza hizo *machines* ili tuweze kupata pesa kuliko ilivyo sasa pesa nyingi sana zinapotea? Nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), hili tatizo lilikuwepo na tulikuwa tukilitolea ushauri. Inaonekana bado halijaweza kufanyiwa mkakati wowote hizo mashine zianze kufanya kazi na hizo *sticker* zianze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti katika ukurasa wa 29 pia imeishauri Serikali kuwa, izingatie maoni na ushauri mbalimbali unaotolewa na Bunge. Pia iangalie uwezekano wa kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali, ili angalau tuweze kuanza kujigharamia Miradi yetu. Kwa sababu kuendelea kutegemea Wafadhili kwa kweli hatuwezi kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimetoa mifano michache ya Wizara ambazo zinaweza zikakusanya maduhuli na zikaongezea katika utekelezaji wa kazi zake, kwa kuonesha kwamba ni vyanzo ambavyo ni dhahiri vipo, lakini bado Serikali inashindwa kuvitumia vizuri na kuongeza mapato. Kwa hiyo, kuna kama uzembe na uvivu fulani wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri huo, katika ukurasa wa 29 wa Taarifa ya Kamati ya Bajeti wamesema kwamba, Serikali ina matumizi makubwa mno, mapato kidogo lakini inatumia kwa kiasi kikubwa. Tukiangalia magari ya Serikali, haya magari ya Serikali ni mzigo mkubwa, kwa maana ya kuyanunua na kuyahudumia magari yaliyopo, ukipiga mahesabu inafika karibu shilingi trilioni tano. Mimi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

ninafikiri tujaribu kufuata mifano mingine kama nchi nyingine ndogo, Rwanda wamejitahidi kuhakikisha Mawaziri na wale wote ambao wanatakiwa kukopeshwa magari wanakopeshwa kuliko huu mzigo ubakie kwa Serikali. Ukiangalia *service* za hayo magari, vipuri, mafuta, kulipa madereva na siyo Mawaziri peke yao, angalia Wizara moja inaweza kuwa na Mawaziri wawili, bado ikawa na Katibu Mkuu, kuna Wakurugenzi na Wakuu Idara; kwa kweli ni mzigo mkubwa sana kwa Serikali. Mimi ninaomba kwa upande huu, Serikali iangalie upya, watu wakopeshwe magari kama inavyofanyika kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kinachopoteza pesa nyingi ni misafara mikubwa ya Viongozi. Katika eneo hili pesa nyingi sana zinapotea, misafara ya Viongozi gharama yake ni kubwa sana. Tuangalie jinsi gani tunavyoweza kupunguza hizi gharama za misafara ya Viongozi ili kuhakikisha pesa kidogo zinatumiwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine tuliloligundua katika Kamati yetu ya *LAAC*, ni utovu wa nidhamu wa matumizi ya fedha katika ngazi ya Halmashauri. Ninataka kutoa ushauri mdogo; kwa mfano, kwa upande wa Serikali Kuu, ninajua *TRA* waliwahi kwenda katika nchi mbalimbali ikiwemo Mauritius kujifunza jinsi gani wanavyoweza kupunguza hii misamaha ya kodi. Tunaomba ifanyiwe kazi haraka tuletewe sheria hapa Bungeni ili tuweze kuirekebisha. Kwa sababu sasa hivi misamaha ya kodi inafikia *almost* asilimia 4.3 ya Pato la Taifa. Kwa kweli hiki ni kitu ambacho ninafikiri tunapoteza mapato mengi tena hapo.

Kingine, tukipunguza punguza hiyo misamaha ya kodi tutapata mapato. Tukijitahidi kuangalia vyanzo vyetu vya ndani tutapata mapato ili tuweze kutimiza majukumu yetu na tutapunguza pia madeni. Deni la Taifa nalo pia mwenendo wake siyo mzuri. Ukiisoma Taarifa ya *CAG*, ukaangalia pia na ushauri uliotolewa na Kamati ya Bajeti, utaona kabisa mwenendo siyo mzuri kwa sababu ya kuongezeka kwa mikopo ambayo ina masharti ya kibiashara zaidi. Kwa hiyo, riba inakuwa kubwa, mkopo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

tunaolipa unakuwa na riba kubwa, malimbikizo ni makubwa sana, tunashindwa kuyalipa kwa wakati. Tunashindwa kuelewa sasa mikopo yote hiyo mikubwa lakini maendeleo nayo mbona hayaonekani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo ambayo nimeyaainisha, ninaiomba Serikali iongeze bidii katika ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara zote ambazo zinakusanya maduhuli. Vilevile ninaiomba Serikali iondoe uzembe katika ukusanyaji na kukadiria mapato; kwa mfano, katika ngazi zetu za Halmashauri. Vilevile Serikali iangalie upya kama kuna uwezekano tutunge sheria ambayo itaweka ukomo wa mawakala kupewa asilimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi katika Halmashauri zetu, ukienda katika Halmashauri hii unaona wakala anapewa asilimia 40, Halmashauri imepata asilimia 60 au labda wapo wanaopata asilimia 30, yaani haijulikani. Tukiamua basi iwe wakala asilimia 25, Serikali ipate asilimia 75 ili tuanze kujitegemea. Kwa sababu bado kuna mianya mingi sana ya upotovu wa pesa kupitia kwa Mawakala. Kama tunavyosikia, vitabu vingi havirejeshwi, wahusika wanapotafutwa hawaonekani na kesi za Halmashauri haziishi. Sasa tunashindwa kuelewa ni kitu gani ambacho kipo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia udhaifu katika usimamizi wa mapato ya ndani uangaliwe. Kwa mfano, Halmashauri 58 walikuwa hawajaletewa na Mawakala takribani shilingi 4,466,000,000. Udhhibiti wa ndani wa ufuatiliaji wa makusanyo ya mapato, kwa Halmashauri 30 wameshindwa kukusanya shilingi 8,008,000,000, pesa ambazo zingeliweza kusaidia Miradi mbalimbali ya Halmashauri na kuongeza mapato kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunalo tatizo la kutokubuni vizuri vyanzo vya mapato ya ndani kwa nchi yetu. Tuangalie wale Maafisa Mipango waliopo katika Halmashauri zetu na wale Wachumi wanastahili kuendelea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MHONGA S. RUHWANYA]

kuwepo; wanayo elimu ya kutosha; na je, wanaweza waka-*perform* vizuri kuhakikisha Halmashari zetu zinafanikiwa? Tunaomba tuwaangalie pia wale, kwa sababu kuna wengine ambao unakuta yuko kwenye Halmashauri moja; kuna sehemu tulikwenda mtu amekaa ofisini toka mwaka 1988 ana panga nini huyo? Kwa hiyo, inabidi tuangalie na hili suala la kumuweka mtu katika kituo cha kazi kwa muda mrefu na wala hajiendelezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali pia ilishughulikie tatizo la mishahara hewa. Kwa miaka mitatu nimefanya hesabu, Serikali imepoteza shilingi 2,237,749,000, kuanzia mwaka 2009 mpaka 2012, kwa kuwalipa watu ambao wamekufa, watoro, wasiofika kazini. Taifa letu tumefikisha shilingi 2,237,749,000 kwa miaka mitatu. Kwa hiyo, ninaomba tuangalie hizo ni kero ndogo ndogo wakati Taifa letu bado lina matatizo mengi ndani ya jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kufanya manunuzi yasiyozingatia sheria. Manunuzi ambayo yamefanyika kwa miaka mitano bila kuwa na nyaraka ni ya shilingi 8,316,000,000. Sasa hapa unaona kuna udanganyifu fulani upo ndiyo maana hakuna nyaraka za kuthibitisha hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba nishauri kwamba, Ofisi ya Kamati ya Bajeti itafutwe haraka na wawekewe Wataalam. Pamoja na kazi yao ya kufanya *Budget Tracking* katika kila robo tatu ya kila mwaka, wawe wanatuletea taarifa Bungeni ili tuone tumekwama wapi na tushauri vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Saleh Pamba na msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Dkt. Kamani!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Taarifa hizi tatu, zilizowasilishwa na Wenyevitwa wa Kamati; Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Rajab Mbarouk na Mheshimiwa Kabwe Zitto. Napenda niwapongeze pia Wajumbe wa Kamati hizo, kwa kazi nzuri sana ambazo wamezifanya. Kusema kweli ukizisoma hizi Taarifa zina mambo mengi sana mazuri, ambayo Serikali inatakiwa iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati hizo zote tatu yapo katika maeneo mbalimbali; kuna maeneo ambayo inabidi Serikali iyafanyie kazi haraka; kwa mfano, mapendekezo ambayo yapo katika Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali, inayoongozwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, kuna masuala ya kisheria ndani ya Taarifa hizo. Kuna masuala ya Kanuni, ambazo kama hazitafanyiwa kazi mapema na Serikali, zinaweza kukwamisha kabisa utendaji kazi wa Serikali pamoja na masuala mengi mbalimbali ya ununuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa za Kamati hizo, kwa mfano, kuna Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011 zinatakiwa zichapishwe lakini inaonekana hatua hajichukuliwa katika kutekeleza suala hili. Kwa ujumla wake ni maeneo ambayo yanatakiwa Serikali ijipange, iyafanyie kazi haraka ili iweze kutukwamua katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo ninataka niyawekee mkazo, ambayo yameguswa guswa katika Taarifa hizi za Kamati. Nitaanza na Kamati ya Bajeti, ambayo ninapenda ni-*declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Kuna maeneo makubwa kama matatu ambayo ni ya msingi kabisa, Serikali yetu lazima iyafanyie kazi tuweze kuondokana na matatizo haya ya kimaendeleo ambayo tunayo. Nami nitapenda kuyachangia maeneo hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kuongeza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBA]

mapato ya Serikali; mapato ya kodi na mapato yasiyo ya kodi. Bado ukusanyaji wetu wa kodi na mapato ya Serikali ni mdogo sana, ukilinganisha na uwezo ambao upo wa kukusanya kodi. Kwa upande wa kodi za kawaida na kwa upande wa mapato ambayo siyo ya kodi, tunakusanya shilingi bilioni 700, kwa *non tax revenue*. Hizo ni kidogo sana ukiangalia katika maeneo mbalimbali, kwa mfano, maeneo ya uvuvi, maliasili, misitu, madini na leseni mbalimbali. Jitihada zinatakiwa ziongezeke ili kuhakikisha tunakusanya mapato ya kutosha hasa katika maeneo ya *non tax revenues*.

Mheshimiwa Spika, tayari Bunge lako Tukufu lilikwishafanya kazi, limeisaidia Serikali katika kupeleka Ripoti ambayo tunaita *Chenge One*. Kuna mapendekezo mazuri sana; kigugumizi ni nini katika kutekekeza mapendekezo yale? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachofikiri na kuiomba Serikali ni kwamba, iangalie ile Ripoti, tutakapokuja katika Bajeti ijayo, angalau katika maeneo ambayo yapo wazi na tunaweza kupata fedha, kwa mfano, uvuvi wa Bahari Kuu, basi kazi zifanyike na kuhakikisha fedha hizo zinakusanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo limetiliwa mkazo katika Kamati ya Bajeti ni kupunguza utegemezi. Serikali yoyote yenye heshima duniani ni Serikali ambayo inajitegemea. Baba wa Taifa alikwishatueleza na katika historia hiyo ndiyo *legacy* yetu ambayo Baba wa Taifa ametuachia. Sasa hivi tunajitegemea kwa asilimia 60, asilimia 40 Wafadhili wanatusaidia. Lazima tufike mahali tuweke *target* ya kupunguza utegemezi wa Mataifa makubwa, angalau tuweke asilimia 70 na asilimia 30. Asilimia 70 fedha zetu wenyewe na asilimia 30 utegemezi, kama nchi jirani wanavyofanya; kwa mfano, Kenya, asilimia 85 ya mapato yao wanajiendesha wao wenyewe na asilimia 15 wanategemea Wafadhili.

Mheshimiwa Spika, nasi kama Serikali na kama nchi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBA]

lazima tuweke lengo la kupunguza utegemezi wa Wafadhili katika kuendesha mambo yetu. Kufanya hivyo kutatupa heshima na kutupa uhuru zaidi. Kwa hiyo, ni eneo ambalo lazima tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati imelizungumzia ni suala la kupeleka fedha za maendeleo kwa wakati. Hilo limekuwa tatizo kubwa kwa upande wa Serikali, hasa katika Miradi ya Maendeleo, tujitahidi tutafute utaratibu ambao utatufanya tupate fedha mapema na kuzipeleka katika Miradi ya Maendeleo. Sasa hivi fedha hizo hazipelekwi kwa wakati, zinapelekwa kidogo. Kwa hiyo, tutafute utaratibu ambapo Serikali, inaweza kukopa katika Mabenki, inaweza kukopa Benki Kuu, kwa sababu yenyewe ina uhakika kwamba itakuwa na makusanyo. Kwa hiyo, zile fedha za maendeleo ni lazima tuhakikishe tunazikopa Benki Kuu na tutazilipa baadaye kwa makusanyo ili Miradi ya Maendeleo isikwame hasa katika maeneo ambayo yanawagusa Wananchi ambao wametuleta hapa. *(Makofi)*

Tupeleke fedha hizo katika maeneo muhimu yafuatayo; kwa mfano, tupeleke fedha kwenye maji, umeme vijijini, barabara, afya na kwenye elimu. Kwa maeneo hayo ambayo yanawagusa Wananchi hata tukikopa kutoka Benki Kuu, inaonesha kwamba, tunakopa kwa mambo ya maana ambayo yatawasaidia Wananchi wetu. Kwa hiyo, ni eneo ambalo ninaona Serikali ni lazima ilifanyie kazi.

Eneo la tatu ni kukopa kwa ajili ya Miradi mikubwa mikubwa. Tunayo *ceiling* ya dola milioni 700 ambayo tunaweza tukakopa chini ya utaratibu wa *PCAI*, lakini hatujafikia hilo lengo. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali kwamba tukope ili tufikie fedha hizo ili tuweze kufanya Miradi mikubwa kama ya reli na Miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niingie kwenye Taarifa ya Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa ndiyo eneo la pili ambalo linatumia pesa nyingi, karibu shilingi trilion mbili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBA]

Bajeti hii ni Bajeti inayokwenda kwenye maendeleo yanayowagusa watu, kuna maeneo ambayo ninaiomba Serikali iwekee mkazo. La kwanza, kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa. Sasa hivi Serikali za Mitaa hazijitegemei, asilimia 90 ya mapato yake yanatokana na Serikali Kuu. *Trend* hii lazima ibadilike. Lazima tujiwekee lengo ambapo asilimia angalau kumi ya mapato yake yanatokana na mapato yake yenyewe na *potential* zipo; tunayo misitu, tunayo ardhi ya kutosha, tunazo bahari ya kutosha na tuna shughuli nyingi ambazo zinafanyika kwenye Serikali za Mitaa. Kwa hiyo ni lazima na *target* hii tuibadilishe, tutoke angalau asilimia 80 Serikali Kuu, asilimia 20 iwe ni mapato yao wenyewe. Hiyo itazijengea heshima Serikali zetu za Mitaa, ambazo ndiyo Serikali zenyewe za Wananchi na Halmashauri zetu na Serikali za Vijiji. Kwa hiyo, hayo ni maeneo ambayo lazima tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine la mwisho ambalo nataka nilizungumzie, nalo ni eneo hili ambalo limekuwa Sera ya nchi yetu ya kugatua madaraka. Napenda nichukue nafasi hii, niipongeze sana Serikali, kwamba, imetekeleza kwa upande wa rasilimali fedha, inapeleka fedha za kutosha katika Halmashauri zetu. Tunatakiwa fedha hizi zisimamiwe, lakini usimamizi katika Halmashauri zetu umekuwa mdogo hazisimamiwi sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo nataka niyazungumzie na kuishauri Serikali; tuangalie jinsi gani tutaweza kuongeza rasilimali watu katika Halmashauri zetu. Tatizo kubwa katika Halmashauri zetu ni rasilimali watu. Watendaji ndani ya Halmashauri hawatoshi; kwa mfano, katika Halmashauri yangu ya Pangani kuna *Water Engineer* mmoja tu, anayo Miradi ya bilioni tatu na milioni mia tano. Unafikiri atafanya nini peke yake bila kumwongezea *staff* wa kutosha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili ni eneo ambalo ninafikiri Serikali Kuu na Serikali za Mitaa wanaweza wakakaa pamoja wakaangalia *staffing levels* kati ya Mawizara

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBA]

pamoja na Halmashauri. Katika Mawizara huko kuna watu wengi sana ambao wapo, usishangae kukuta Wizara moja kuwa na *staff* zaidi ya mia nne wakati katika Halmashauri hakuna *staff*. Kwa hiyo, ipo haja ya kuangalia *staff disposition* katika Serikali Kuu na kuhakikisha kwamba, baadhi ya Wafanyakazi ambao wamerundikana katika Mawizara, wanapelekwa katika Halmashauri ili waweze kusukuma maendeleo kule. Hatutaendelea hivi kwa kuwa na *staff* wachache wakati Serikali ni moja, ile inaitwa Serikali ya Mitaa tu, *otherwise*, ni Serikali moja. Kwa hiyo, tutafute utaratibu wa kuwatoa hao wafanyakazi waliopo katika Mawizara na kuwapeleka katika Halmashauri ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, najua kikwazo kilichokuwepo zamani ni kwamba, *pension* zao zilikuwa tofauti. *Pension* ya Serikali ilikuwa kubwa kuliko ya *Local Authorities*, lakini mambo hayo yamerekebishwa. Kwa hiyo, hakuna sababu tena ya Mtumishi kuona akienda kufanya kazi katika Serikali za Mitaa atapata *pension* ndogo na masilahi madogo, kwa sababu yote hayo yamekwisha rekebishwa, *Pension Funds* zote zinatoa masilahi sawasawa.

Naiomba Serikali kwamba, kama kweli tupo *serious* katika kusaidia Halmashauri zetu, basi tuhakikishe tunafanya kazi ya kuangalia *staff* waliopo kwenye Mawizara waliolundikana ili tuwapeleke kule Wilayani na kwenye Halmashauri, wafanye kazi na kusukuma hii Miradi ambayo inabeba fedha nyingi sana za Serikali. Hapo ndipo tutawakomboa Wananchi wetu ili watokane na umasikini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niyaseme hayo. Nawapongeza sana Wenyeviti wa Kamati zetu. Naipongeza sana Serikali, Serikali yote inajitahidi hasa ya Chama cha Mapinduzi, inajaribu kutekeleza llani kwa kadiri ya uwezo wa fedha zake, maana hatuna mapato mengine zaidi ya Wananchi wetu hawa hawa. Barabara zinatengenezwa, Miradi ya Maji inatengenezwa, Miradi ya Umeme Vijijini yote inafanyika kutokana na Serikali ya Chama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SALEH A. PAMBA]

cha Mapinduzi. Tukijirekebisha katika maeneo haya ambayo nimeyazungumzia ni maeneo ya msingi kabisa ambayo yatatusaidia kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana umenipa nafasi hii, ni matumaini yangu kwamba, Ripoti hizi zote tatu ni nzuri sana, Serikali yetu itazifanyia kazi. Tunatumaini kwamba, katika Bajeti ijayo tutaona mabadiliko makubwa sana katika Bajeti ambayo itakuwa *focused* katika kusukuma maendeleo ya Wananchi wetu na kuwapunguzia shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Msemaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Dkt. Kamani!

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hoja zilizopo mbele yetu. Nianze kwa kuwapongeza sana Kamati hizi tatu na Wenyeviti wao, kwa kazi nzuri waliyofanya na Taarifa nzuri waliyotuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naipongeza Kamati ya Bajeti na pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa ubunifu wako wa kuianzisha Kamati hii. Kamati hii imetuletea sura mpya ya kuangalia uendeshaji wa Mfumo wa Bajeti wa Taifa letu kwa ujumla. Nakupongeza sana Mheshimiwa Spika, kwa ubunifu huu. Nampongeza Mwenyekiti wa Kamati hii, Mtemi wa kule kwetu, Mtemi Chenge, kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo moja nililolibaini katika Taarifa hii na ndiyo hali halisi tunayoiona katika maeneo yetu ni pesa kutotolewa kwa wakati; sijaelewa tatizo ni nini? Taarifa hii imetuonesha kwamba, makusanyo ya Serikali kwa kipindi hiki yalifikia asilimia 85.7, lakini pesa iliyotolewa, pesa ya maendeleo iliyogawanya ni asilimia 11 tu ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]

malengo. Fedha kwenye mikoa ni asilimia 17, sasa ninashindwa kuelewa labda wanieleze hawa wataalamu wa kimahesabu kama tuliweza kukusanya asilimia 85.7 hii pesa nyingine imeenda wapi sasa; kwa nini isiende kule kwa uwiano ule ule wa asilimia 85.7? Kwa sababu ingeenda kwa uwiano huo, nina uhakika hali ingekuwa nzuri sana huko kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwatia hamasa hii Kamati ya Bajeti, iendelee kubuni vyanzo vingine zaidi, lakini iendelee kusimamia ugawaji. Kipindi cha awali kulikuwa na manung'uniko kidogo juu ya mahusiano ya Kamati hii na Kamati zingine kana kwamba labda kuna kuingiliana, kuchukuliana majukumu. Haya ni masuala tu, kwa sababu ni Kamati mpya, nina hakika yanaweza yakaondolewa ili Kamati zote zifanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna ubunifu ambao nimeuona kwa mfano, *TRA*, inahimiza unaponunua kitu dai risiti, unapouza toa risiti, ni wazo zuri na vyema Watanzania likatuingia kwa sababu hatimaye Wananchi wote tutaweza kuchangia katika mapato ya Taifa, ambayo hatimaye hii keki tunayong'ang'ania tuigawane vizuri tutaweza kufikia. Kwa hiyo, nahamasisha Kamati hii iendelee na ubunifu huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo nyeti ambayo tuliafikiana kwenye Mpango wetu wa Maendeleo. Tunajua kwamba, lazima kilimo, mifugo, uvuvi, utalii na maji, viwekewe msukumo wa pekee kwa lengo la kunyanyua ule uchumi wa jumla, uchumi mpana wa Wananchi. Vilevile ili Taifa liweze kuwa na vyanzo vingi vya mapato na vya uhakika, nishati na madini, viwanda na biashara, miundombinu na uchukuzi, lazima Bajeti zake zisikwame ili hatimaye uwekezaji uweze kuwa na tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wiki moja iliyopita, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye vilevile ndiyo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Taifa, alikuwa na ziara Mkoani Simiyu. Katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]

ziara ile alikuja kuzindua Mkoa mpya wa Simiyu na Wilaya mbili za Busega na Itilima. Uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala ni kusaidia kusogeza huduma karibu na Wananchi na hii ni kazi ya Serikali nzuri ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ziara ile alizindua ujenzi wa barabara ya lami kutoka Lamadi kwenda Mwigumbi, sijui kilometa 105, Mheshimiwa Magufuli anazifahamu sana. Alizindua pia Mradi wa Umeme Vijijini, Chuo cha Uuguzi Mkula, Matawi ya Benki za Azania na Benki ya Wananchi ya Simiyu, Daraja la Mto Mwanuzi na kukagua shughuli mbalimbali za maendeleo. Hizi zote zinalenga kusaidia kuboresha maisha ya Wananchi ambayo watu wengine mnaona kama hawavioni, lakini lazima tukiri mambo mazuri yanapofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri aliofuatana nao; Mheshimiwa Hawa Ghasia wa TAMISEMI, Mheshimiwa Engineer Mahenge - Naibu Waziri wa Maji na Mheshimiwa Stephen Masele - Naibu wa Nishati na Madini. Kazi nzuri, ilionekana na Wananchi walifurahi sana katika Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Busega. Lazima uwatie moyo watu wanapofanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Kwa Wilaya yangu ya Busega, namshukuru sana Mheshimiwa Hawa Ghasia na nikimshukuru Mheshimiwa Hawa Ghasia maana yake ni Waziri Mkuu; kwa sababu ametuletea timu nzuri sana ya Watendaji katika Wilaya yetu. Mkurugenzi wa Maendeleo mzuri, Wataalamu na Wakuu wa Idara ni wazuri na wanafanya kazi nzuri. Wameungana na Mkuu wa Wilaya mzuri - Ndugu Mzindakaya. Bahati nzuri tuna Mwenyekiti wa Halmashauri mzuri na Mbunge wao nipo pamoja nao na Madiwani tumeafikiana, tunasema tuna kitu kinaitwa uwine mtakatifu wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, unafanya kazi nzuri na mimi nawaomba Wananchi watuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo ninapopingana kidogo na Sera ya wenzetu, ambayo jana nillisikia hapa,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]

nashangaa sana na leo nimeisikia ikirudiwa, eti ukimwona Mwenyekiti wa Halmashauri wanaelewana na Mkurugenzi au DC anaelewana na Mkuregenzi, uelewe kuna jambo baya linafanyika. Mimi sielewi inakujaje! Sisi wote hapa ni Viongozi na katika masomo inafundishwa Utawala Bora. *Good Governance* inaendana na *team work*. Sasa mtafanyaje jambo zuri wakati Mkurugenzi anasema hiki, Mwenyekiti wa Halmashauri anasema hili, Diwani anasema hili, DC ana la kwake na Mbunge ana la kwake; kuna kitu gani kitafanyika hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii Sera imenitatiza kidogo hapa. Naomba CCM kama Sera yetu ni ushirikishaji iendeleo na Wananchi watuunge mkono. Naamini hata makanisani tena ilisemwa na Mchungaji, hivi Mchungaji akishirikiana na Waumini wake elewe kuna jambo linafanyika hapo? Hiki ni kitu cha ajabu, mimi ninafikiri Viongozi tunatafuta tuwashirikishe Wafuasi wetu. Sasa hapo sikuelewa kwa kweli! Hizi kauli za jumla zina hatari sana, zinaweza kuleta madhara uka-*mislead* watu. Kama kuna kosa tulilenge kosa tulirekebishe lakini siyo kauli za jumla. (*Kicheko/Makofi*)

Tunatolea mfano wa magari Rwanda kwamba wanafanya vizuri, wanatumia Suzuki na Vitara. Mkoa wangu wa Simiyu pekee ni Rwanda mara mbili, nikikatiza kutoka Mto Sibiti mpakani na Singida mpaka Ziwa Victoria, Lamadi na Suzuki na Vitara haiwezekani! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifanya jambo jema akasema tuondoe magari makubwa sana twende ya *size* ya kati na linatekelezwa sasa. Tusingeweza kuyaondoa mara moja tuliyonayo ila litekelezwe. Ninaona hata Wakuu wa Wilaya, wana magari ya kati, lakini yanawezesha ku-*cover* maeneo makubwa ambayo ndiyo maeneo ya kazi. Kwa hiyo, tuepuke na kauli za jumla bila kuangalia mazingira halisi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ni ya Chama cha Mapinduzi, wakati wa Uchaguzi Mkuu, Chama cha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]

Mapinduzi kilinadi Ilani ya Uchaguzi, Wananchi wakakiamini wakakipa kura kikaunda Serikali. Chama cha Mapinduzi ndiyo mwenye mali, amempa Mkandarasi Serikali atekeleze. Sasa mwenye mali amekuja kukagua kazi, Mkandarasi unakataaje kwenda kumpokea, unakataaje kwenda kutoa taarifa? Kuna kosa gani Kiongozi wa Chama cha Mapinduzi akitaka Taarifa ya Mtendaji wa Serikali? Ni kosa gani Mkurugenzi akienda kumpokea Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kutumia gari la Halmashauri kwa sababu hiyo ni nyenzo ya kazi amepewa ili atekeleze Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo Wananchi walituumini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tushiriki na wengine mtakapopata zamu yenu ya kutawala tuone kama hamtataka kuwasimamia wale watu. Wito wangu kwa Watendaji wa Serikali, washirikiane na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndiyo Chama Tawala. Kauli zinazotolewa eti hao ni Wanasiasa, hao sijui akina nani wanajidanganya. Tuna Mataifa ambayo wanajiita ni Waasisi wa Demokrasia; Uingereza na Marekani. Chama kimoja kikishinda, *Republican* ikishinda inaondoa na kuunda safu mpya ya Watendaji wa Serikali. Tunaona Mabalazi wanaondolewa, Wakurugenzi wanabadilishwa, kwa sababu inataka iweke Watendaji ambao wanaiamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kuna Watendaji wa Serikali wanaofikiri kuifanyia kazi Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni makosa, basi hao hawastahili kuwa hapo na naomba Serikali mchukue hatua, kwa sababu tunafanya kazi na watu ambao wapo tayari kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambayo ndiyo Wananchi wanatupima nayo; kama wanaimba nyimbo za Vyama vingine ambavyo vina rangi nyingi, basi hawapo mahala pale wasubiri zamu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwatia shime Serikali, yamezungumzwa mengi ya udhaifu wa hapa na pale, chukueni hatua haraka. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]

mwadilifu sana, ni mtu anayejitolea sana kwa ajili ya Taifa hili. Nimebahatika kusafiri naye China, anafanya kazi mpaka usiku wa manane kwa ajili ya kuitafutia neema nchi yetu. Hawapo wengi wa namna hiyo; sasa hivi uadilifu siku hizi imekuwa dhambi? Siasa ya siku hizi inakuwaje, tunataka Viongozi wa namna gani mtu anapokuwa mwadilifu anakuwa hafai? Kwa kweli inanitatiza kidogo, naomba Serikali ifanye kazi yake. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningepomba na Wananchi vilevile, kwa sababu maendeleo hayawezi kuletwa na Serikali peke yake bila Wananchi kushirikiana, lazima Wananchi tuwe tayari kuiunga mkono Serikali. Kwa mfano, kule Jimboni kwangu ambapo kuna Miradi mingi ya Umeme inawekwa, barabara zinachongwa ambazo tangu uhuru zilikuwa hazijatengenezwa, sasa barabara hizi hazitawekwa hewani lazima zipite kwenye ardhi. Wananchi tusidai *compensation* ikakwaza utekelezaji wa Miradi, kwa sababu *compensation* ni haki yao pale inapostahili lakini isikwamishe maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna wanasiasa kule wanapita wao ni kulaumu tu na kudanganya Wananchi na kuandika magazetini, lakini Wananchi naomba washirikiane na Serikali ili maendeleo ya haraka yapatikane.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nimekuona umesimama Mheshimiwa Msigwa!

T A A R I F A

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68. Mzungumzaji aliyepita amezungumza kwamba, Watendaji wa Manispaa, Mkurugenzi na Watendaji wake, wapo kwa ajili ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi; kitu ambacho ni kinyume kabisa na utendaji na taratibu za Utumishi wa Umma. Watumishi wa Umma wanafanya kazi ya Serikali hawafanyi kazi ya Chama cha Mapinduzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MCH. PETER S. MSIGWA]

Wanaongozwa na Kanuni ya Utumishi wa Umma na Sheria za nchi. Kwa hiyo, kupotosha Watanzania hapa kusema kwamba, wapo pale kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni uongo na hawapaswi kutumia magari ya Serikali kwenye shughuli za Chama. *(Makofi)*

SPIKA: Mwongozo au Taarifa? Kama Taarifa siyo sahihi kwa sababu katika Mfumo wa Vyama Vingi kila Chama kinachotaka kutawala kitakuwa na Ilani yake. Kile kitakachokubaliwa na Ilani yake, Ilani ile ndiyo itatumika na wote kutekeleza maamuzi. Kwa hiyo, siyo sahihi. *(Makofi)*

Ya pili, wakati tunamaliza maswali Mheshimiwa Lugola, aliomba mwongozo kuhusu maneno aliyoyasema Mheshimiwa Hawa Ghasia kwamba, ningekuomba ushauri na mimi nikamwambia Katiba hiyo hiyo anayosema ndiyo inayodai ushauri. Sasa ningependa kusoma hiyo Katiba inavyosema; Kifungu cha 63(2), Sehemu ya Pili, itakuwa ndicho Chombo Kikuu cha Jamhuri ya Muungano, ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya Wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. Maana nilisema kwamba, haya maneno ya kushauri yapo kwenye Katiba hiyo hiyo kwa hiyo ndiyo hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, tutarudi saa kumi na moja jioni. Tutakaporudi, baadhi ya Mawaziri watachangia. Nitawasomea kifungu kinachohusiana na Taarifa za Hoja za Wabunge. Hawajibu hoja zenu watachangia, kwa hiyo, nitawasomea kifungu kichostahili.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilibungwa hadi saa 11.00 jioni)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilisema tukirudi tutaeleza msingi wa kuwasilisha Taarifa za Bunge, Taarifa za Kamati za Bunge na namna tunavyofanya kazi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 123, kuna (a), (b) na (c), namna ya kuandika Taarifa. Kwanza kabisa ni mambo ya utambulisho, *introduction* tu, ya pili, mambo yaliyojitokeza na (c), sehemu ya mwisho ambayo itatoa maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge. Kwa hiyo, tunachojadili hapa ni maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge.

Kwa hiyo, tutakapofika Mawaziri hawa watakuwa wachangiaji. Msitagemee hapa anaanza kujibu nani alisema nini, nani alitukana mwenzie, nani kafanyaje, hawatajibu. Kwa hiyo, watachangia Mawaziri wengine nawapa dakika 15, 15. Waziri wa TAMISEMI kwa sababu mjadala mkubwa ulikuwa zaidi kwenye TAMISEMI, kwa hiyo na yeye tutampa dakika 30. Baada ya hapo Wenyeviti wataanza kujibu maoni ya Waheshimiwa Wabunge na yakimalizika hapo tumemaliza.

Sasa namwita Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Lukuvi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kwa muda huu, nichange hoja hizi tatu za Kamati. Kwanza, natoa shukrani sana na pongezi kwa Kamati hizi. Najua kazi hii ni ngumu sana ya kuchambua Ripoti zilizoandikwa kwa miezi mingi na CAG, lakini wamefanya *summary*, najua hii ni *summary* tu wangeweza kuandika vitabu vikubwa. Nawapongeza sana kwa hayo yaliyoandikwa. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao ya siku tatu, nne, yenye afya sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie mambo matatu tu. La kwanza, ninataka nichangie juu ya utaratibu. Wakati Wenyeviti wanawasilisha Taarifa zao, sikuona hata mmoja ana-*appreciate* kwamba, amewahi kuona angalau

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Serikali ikitekeleza matakwa ya Kikanuni. Kwa mujibu wa Kanuni yetu ilitutaka baada ya kuwasilisha Taarifa za CAG mwezi Aprili, tarehe 27 Juni, Serikali iliandaa sehemu ya majibu, lakini pia ilitoa utaratibu wa namna ya kutekeleza na namna ya kujibu Taarifa hizi za CAG. Ndani ya vitabu hivi nilivyonyavyo, tulitoa *copy* 400 kila kimoja tukiamini kwamba, Waheshimiwa Wabunge watasoma, pamoja na Taarifa ya CAG, lakini watavisoma na hivi ambavyo vitapunguza uzito na ukubwa wa namna ya kufanya kazi, kwa sababu baadhi ya majibu humu ndani yamejibiwa na yamekamilika.

Hizi ni Taarifa zilizotolewa na *Hansard* na *Order Paper* ya tarehe 27 Juni, inaonesha kwamba, Taarifa hizi zilifikishwa Mezani. Kwa mfano, ipo hoja kwenye ukurasa wa 130 wa Taarifa ya CAG, inahusu Ofisi ya Waziri Mkuu na kwenye Ripoti imo. Kulikuwa na hoja ya malipo yenye nyaraka pungufu ya shilingi 42,474,500. Ukisoma kwenye kitabu hiki, ukurasa wa 15, tumeitolea majibu na hoja yenyewe imekwisha. Hali kadhalika ukija kwenye hoja ya ATC ambayo nimeiona humu ndani, inaeleza jinsi gani hao wahusika wanavyoshughulikiwa na PCCB.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, nilitaka tu Wenyeviti wenzangu hawa Wabunge watatu waniambie taarifa hizi walizipata au mimi tu ndiyo ninazo hapa na kama walizipata ziliwasaidia kiasi gani na kama hazitoshelezi basi watupe changamoto Serikali tujiandae zaidi. Ujue kwamba, ilikuwa miezi miwili, baada ya Taarifa ile ya CAG tunakiwa tutoe hii taarifa. Tumejitahidi kiasi hicho. Kwa hiyo, nilifikiri katika kurasa zote zilizoandikwa na rafiki yangu Mheshimiwa Rajab na Mheshimiwa Zitto, angalau kungekuwa na sentensi moja ndogo ya shukrani kwa Serikali kwa kujitahidi ku-*respond* kwa mujibu wa Kanuni zetu, kidogo tu. Sisemi watusifie kwa yale yaliyofanyika, lakini angalau tumejitahidi kwa mujibu wa Kanuni tulitakiwa tujitahidi kiasi hicho.

La pili, nilisikia hapa kwamba, baada ya mjadala wa ile Taarifa iliyoishia 2010, kuna Taarifa moja hatukujadili humu ndani, lakini zile zilizoishia Juni, 2010, wapo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Waheshimiwa Wabunge wanasema, yale yote yaliyosemwa humu hatukujibu. Kwa utaratibu sisi tunatoa taarifa mbili, Serikali, tunatoa taarifa za awali kwa zile hoja ambazo tuna majibu ya uhakika tunaziandika humu. Baada ya miezi miwili tunaweka kwenye vitabu hivi na tunachapisha *copy 400* ili kila Mheshimiwa Mbunge apate, tumefanya hivyo. Baada ya mjadala tunatoa *Treasury Notice*, yaani majibu ya mwisho ya hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge kama mlivyofanya leo nazo tulifanya. Tulifanya na hizi *copy* ninazo tena nimezichukua kule Maktaba ya Bunge, tuliwasilisha.

Hizi nazo niliambiwa tunasemasema hapa lakini yote hayatajibiwa, hapana. Maelekezo yote na michango yote iliyotolewa na Bunge lako Tukufu mara ya mwisho, Serikali tumejibu. Ninayo Taarifa hapa ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ninayo Taarifa hapa ya Mashirika ya Umma na hii hapa Hesabu za Serikali tulijibu. Sasa huu ndiyo utaratibu unaotuongoza wa Kikanuni. Kama ni kutekeleza kwa Kikanuni tumefanya. Hatujatekeleza vizuri kujibu hoja zote, lakini angalau tumejitahidi kutekeleza masharti ya Kanuni. Mheshimiwa Rajab unaniangalia, nilifikiri siku nyingine utushukuru kidogo, angalau tumejitahidi kutekeleza wajibu wetu. Maana hapa tunasikia Serikali hii kiziwi sana, Waziri Mkuu huyu jeuri sana, lakini mwongozo huu ndiyo unamtaka afanye haya tumefanya. Sasa inawezekana yaliyomo siyo sahihi sana, hilo ni suala linguine, lakini kwamba hatukufanya kabisa, hapana.

Mheshimiwa Spika, sisi sote ni mashahidi, mwaka 2006 tulipoingia, Mheshimiwa alifanya jitihada kubwa, kabla ya hapo Hesabu hizi za *CAG* zilikuwa chafu kweli, yaani hata ukisoma zile Ripoti zilikuwa haziridhishi hata kidogo. Tukakusanywa pale Ubungo Piazza, tukakutanishwa na wenzetu wa Halmashauri na tukapewa maelekezo. Tukaombwa kila mmoja kati yetu basi atumie nguvu kidogo tu kusimamia katika maeneo yao. Nami naamini nguvu tuliyoitumia humu ndani, tungetumia kidogo tu kuhakikisha kwamba, angalau hoja moja au mbili ndani ya Halmashauri zetu zinajibika vizuri tungeweza. Kwa sababu hapa hakuna Halmashauri ambayo haina mwakilishi mmoja au wawili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Nguvu hii tuliyoitumia hapa nimepeinda, sasa tungeshusha lile rungu kule, tukikaa kule angalau kwa sababu tunakuwa tumeshafanya na tathmini nani na nani anahusika na wapi. Hebu tushushe rungu na nguvu zetu kidogo kule kwenye Halmashauri, tufanye kote huku, lakini tushushe kule ambako mambo mengi yanaharibika.

Baada ya Mheshimiwa Rais kuchukua zile jitihada binafsi za kusimamia jambo hili, ndiyo sasa mambo yameanza kuwa mazuri na hili nalo Mheshimiwa Rajab nilifikiri ungesema kidogo maana taarifa yako imeanza kavu kavu. Mheshimiwa Zitto kidogo ameanza na hiyo *preamble*, lakini wewe umeanza kavu kavu kana kwamba, mambo yako vilevile. Nikukumbushe kwamba, mwaka 2010, Halmashauri ambazo zilikuwa na Taarifa ambazo hazikuridhisha ni nne, lakini leo hakuna. Hiyo si kazi nzuri? (*Makofi*)

Taarifa zilizokuwa na mashaka mwaka 2005 zilikuwa 51, leo zimeshuka mpaka 29. Si kazi nzuri hiyo Mheshimiwa Rajab? Taarifa inayoridhisha ilikuwa Halmashauri 62 lakini leo 104, asilimia 78. Si kazi nzuri hiyo?

Nafikiri nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa nguvu kubwa aliyoiweka katika kuhakikisha wote tunashirikiana katika kusimamia rasilimali ya Taifa. Mmejitaahidi sana pamoja na Wasaidizi wa kila Sekta, Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Mawaziri wa TAMISEMI wamejitaahidi sana. Nchi hii ni kubwa, Halmashauri zinazidi kuongezeka kila leo. Hata ninyi Kamati ya LAAC mngetembea miaka mitatu kuzisimamia zote hamuwezi, lakini angalau tuseme tu kwamba kwa uwezo huo tumejitaahidi.

Mheshimiwa Spika, nilifikiri niseme hivyo, lakini yapo mengine yamezungumzwa, imezungumzwa sana suala la Waheshimiwa Mawaziri kutokuwemo humu. Narudia tena niliyoyasema jana, Mawaziri wote wanapokosekana humu Bungeni hakuna hata mmoja ambaye anakosekana kwa makusudi. Hawa ni binadamu, kama binadamu wengine wanaumwa na wengine wanauguliwa, lakini Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

haisimami. Serikali yenu hii ndiyo mfumo wake, ingekuwa kama Kenya, wanaitwa kwa Ratiba kwamba njoo ujibu swali letu utoke. Kwa Katiba yetu, hawa Mawaziri wakati wote wanaendesha Serikali lakini wanatakiwa kufika Bungeni.

Kwa hiyo, nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Spika, leo umewaona wapo wengi, ratiba zao za kazi za nje zimepungua wamefika. Bado utaratibu wetu upo wazi kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa vibali tu, kwa sababu za msingi na anamwarifu na Spika. Kwa hiyo, ukiona myu yeyote ametoka ndani ya *bench* la Serikali, mjue kwamba na Spika amearifiwa, lakini kwa sababu za msingi na zenye masilahi ya Taifa. Nje ya masilahi ya Taifa labda awe anaumwa.

Nilitaka kuwahakikishia kwamba, hatudharau wala Waheshimiwa Mawaziri hawakosekani hapa kwa sababu wanadharau maswali au wanadharau vipindi vya Bunge, isipokuwa wapo kwenye majukumu ya Kitaifa.

La mwisho, limezungumzwa suala la fedha za Uswiss. Nilitaka kusema kwamba, ni kweli jambo hili lilitufikia na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda timu iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, imeanza kazi, lakini hili tutakuandikia Mheshimiwa Spika halijakamilika. Tutakuiandikia tu kuomba muda zaidi kutokana na kutokukamilika ambako kumesababishwa na sababu zilizo nje ya uwezo wetu. Kuna taarifa ambazo kwa sheria za kimataifa hatuwezi kuzipata.

Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia tu Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tunalishughulikia na Serikali imelichukulia jambo hili kwa uzito mkubwa. Baada ya muda huo ambao tutauomba kwa Mheshimiwa Spika kumalizika, nadhani ripoti hiyo tutaileta. Tunataka tuilete ikiwa kamilifu, siyo taarifa nusu nusu. Najua sasa hivi tunashughulikia haya mambo ambayo tunasema yako nje ya uwezo wetu ili angalau yatuwezeshe kupata taarifa za msingi za uhakika na kukamilisha uchunguzi wetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nilitaka niseme hayo machache, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Bado tuna changamoto ya namna bora zaidi ya kurekebisha upungufu huu kwa pamoja. Nilifikiri nitoe rai tu kwamba, pengine Mheshimiwa Spika, una utaratibu wa kuwaita Wenyeviti hawa kwenye semina mbalimbali za kukaa na CAG. Semina hizo utushirikishe na sisi baadhi ya Mawaziri tunaohusika na hayo, tukae pamoja tupange mkakati wa pamoja wa namna ya kupunguza matatizo makubwa yanayosababisha upotevu wa fedha za Serikali hasa katika Halmashauri zetu.

Inawezekana upo usimamizi lakini pia inawezekana zipo *procedure* tu ambazo pengine tukizifuata au Sheria zinaweza zikatusaidia uhibitaji mzuri zaidi wa fedha. Kwa hiyo, nilifikiri baada ya hapa kama inawezekana, tukaendelea kuzungumza kutafakari zaidi ili angalau wote kwa pamoja tuendelee kushirikiana siyo kwa sababu taarifa hizi zimesomwa na kujadiliwa leo tu yamekwisha. Tuendelee kujadiliana ili angalau fedha za Wananchi hizi ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tulipoanza, kuna haja ya kuona utaratibu mzuri zaidi wa kufanya kazi hizi za kuwasilisha Taarifa ya Kamati, Serikali yenyewe na kitu muhimu ambacho kwa muda mrefu hakikuwa kinaandikwa, *Treasury Observation Notes*. Hii ndiyo inayo-*zero in* maswali ambayo hayakupata majibu na wenyewe *Treasury* wamechukua hatua gani na pengine kuwawajibisha wanaohusika.

Mimi nadhani nakubaliana na yeye kwamba, tutatafuta utaratibu tuone, maana saa nyingine ni *repetition* ya mwaka jana yanalundikana mwaka huu, lakini hivyo vitabu vimegawiwa vyote 400 tuligawa kwa Wabunge. Sasa sijui *Controller and Auditor General* au *Internal Auditors* walivilinganisha na maswali yaliyoko, hili ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

suala ambalo siwezi kujibu hapa lakini kuna umuhimu wa kufanya tuone kama kila mwaka kweli yanatokea hayo ama ni *accumulation* inakuja hapa inalundikana tena. Kwa hiyo, itabidi tuliangalie vizuri, tuone tunaingia kwenye ukurasa ulio bora zaidi kuliko hii inavyokuwa. Kama alivyo sema ndiyo hivyo wanajadili.

Muhimu ni kwamba, hawatajibu sana haya mliyozungumza hapa, watajibu zaidi hoja za *Controller and Auditor General*, watajibu kwa maandishi kwa hatua zote hizi. Haya mengine mmetoa taarifa tu yale mnayoyaona huko, lakini majibu ya Serikali yatakuwa kwenye hoja za *Controller and Auditor General* na hiyo *Treasury Observation Minutes*.

Sasa nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, Janet Mbene!

SPIKA: Ndiyo unachangia, hujibu maswali. Dakika ni 15 tu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu ...

SPIKA: Hutoi hoja unachangia tu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA: Nachangia hoja. Samahani, Mheshimiwa Spika. Naomba niende basi moja kwa moja kwenye hoja zenyewe, kwa sababu muda hauniruhusu sana.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati imeongozwa na misingi ifuatayo; Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Kanuni za Kudumu za Bunge, Ripoti ya Mdhibiti Mkuu, Ripoti ya Mdhibiti na Sheria zote ambazo Kamati ilizingatia kama ambavyo zimeainishwa katika Taarifa hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. J. Z. MBENE)]

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa majibu kwa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa hesabu za mwaka unaoishia Juni 30, 2012 iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2013. Wakati Kamati ikijadili hesabu za mafungu mbalimbali, mambo muhimu yaliyojitokeza ni pamoja na haya yafuatayo:-

Kutozingatiwa kwa utaratibu wa kuanzishwa vitengo vya ununuzi yaani *PMUs*.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na kutozingatiwa kwa utaratibu wa uwezeshwaji wa Vitengo vya Usimamizi wa Ununuzi wa Bidhaa za Taasisi za Umma, baadhi ya sababu zinazosababisha hali hiyo...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri naomba kidogo. Mheshimiwa Machali, unasemaje?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo wako, iwapo mchangiaji anaruhusiwa kusoma wakati anachangia au vinginevyo. Maana yake naona mchangiaji kama yuko anasoma taarifa jambo ambalo nafikiri kwa mujibu wa kanuni zetu sidhani kama liko sawa. Naomba mwongozo wako kama jambo hilo linaruhusiwa au la?

SPIKA: Katika hali ya kawaida, wewe ambaye huwajibiki mahali popote isipokuwa kwa maneno yako, unachangia, lakini huyu anawajibika kwa niaba ya Serikali, atasoma. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Baadhi ya sababu zinazosababisha hali hiyo ni pamoja na ukubwa wa Taasisi, ikama na kadhalika. Hata hivyo, Sheria ya Ununuzi wa Umma sura ya 410 kifungu cha 39 kinampa nguvu Afisa Masuuli kufanya ununuzi kwa kutumia Taasisi nyingine au Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini. Aidha, Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 kifungu cha 37 inazitaka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. J. Z. MBENE)]

Taasisi nunuzi kuanzisha vitengo vya usimamizi wa ununuzi na kuwataka Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa vitengo vya usimamizi wa ununuzi vinapatiwa kasma na bajeti ya kutosha kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, pili, kulikuwa kuna suala la utayarishaji usiokuwa sahihi wa mipango ya mwaka ya ununuzi. Serikali inasisitiza Taasisi nunuzi kuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka kwa kuzingatia mpango wa mwongozo wa bajeti uliopitishwa. Katika mwongozo huo, suala la mpango wa ununuzi wa mwaka unapaswa kufanyika sambamba na maandalizi ya bajeti. Hata hivyo, kumekuwa na udhaifu kwenye maeneo mbalimbali katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake. Katika kutatua baadhi ya kasoro hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuwajengea uwezo Watendaji wa Taasisi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Serikali imetoa mafunzo kwa baadhi ya watumishi yanayohusu masuala ya ununuzi wa umma ili kuondoa kasoro ambazo zimekuwa zikijitokeza katika ukaguzi kama ilivyoonekana kwenye jedwali lילוambatanihwa. Jumla ya idadi ya Taasisi zilizopata mafunzo ni 169 kati ya mwaka 2009/2010 hadi 2011/2012 na jumla ya watumishi waliopata mafunzo ni 3,745.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya jitihada hizo ni kuongezeka kwa uzingativu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake mwaka hadi mwaka kama ambavyo tumeainisha katika jedwali ambalo mtaliona katika chapisho hili ukurasa wa sita.

Mheshimiwa Spika, tatu, ilikuwa ni suala zima la ukusanyaji mdogo na upotevu wa mapato ya ndani unaofanywa na *TRA*. Ili kuweza kupima utendaji wa *TRA* katika ukusanyaji wa mapato ni vyema kuangalia viashiria vinavyokubalika katika kupima suala hilo ulimwenguni. Ufanisi katika ukusanyaji mapato ya kodi unaweza kupimwa kwa kutumia vigezo mbalimbali kutegemea matakwa au lengo la upimaji huo. Kigezo cha moja kwa moja ambacho nchi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. J. Z. MBENE)]

nyingi duniani hutumia kupima ufanisi katika ukusanyaji kodi ni uwiano kati ya makusanyo ya kodi na pato la Taifa yaani GDP.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kisera na za kiutawala ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Jitihada za kukusanya mapato ya ndani nchini Tanzania zimeleta mafanikio ya kuridhisha. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita mapato yetu ya ndani yameongezeka toka asilimia 11.2 ya pato la Taifa la mwaka 2003/2004 hadi mwaka asilimia 17.6 ya pato la Taifa katika mwaka 2012/2013 na yanatarajiwa kufikia asilimia 20.8 ya pato la Taifa katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kiwango hiki cha asilimia 20.8 kipo juu ya wastani wa nchi hizi za kipato cha chini zilizoko Kusini mwa jangwa la Sahara ambako wastani kwa mapato ya ndani ni asilimia 18.2 ya pato la Taifa. Mfano wa Pato la Taifa kwa nchi ya Zambia ni asilimia 20.2, Rwanda asilimia 13.6, Uganda asilimia 13.2, Kenya asilimia 23.5 na Afrika ya Kusini ni asilimia 24.5.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika uimarishaji wa ridhaa ya ulipaji (*tax compliance*) ni kigezo muhimu katika kupima ufanisi kwenye ukusanyaji kodi za Serikali. Ridhaa ya ulipaji kodi inatofautiana kati ya nchi na nchi kutokana na hali halisi ya uchumi, mfumo wa kodi na utawala bora. Mamlaka ya Mapato imefanya jitihada kadha wa kadha ili kukuza kiwango cha ridhaa. Jitihada zilizofanyika ni kama kuendelea kupitia Sheria za Kodi na kuzifanyia marekebisho ili kurahisisha utekelezaji wake.

Serikali pia imeimarisha utoaji wa elimu ya kodi kwa walipa kodi na wafanyakazi. Kuanzisha Ofisi Ndogo za Kodi katika Wilaya zote za Dar es Salaam ili kusogeza huduma karibu na walipa kodi. Kuendelea kuimarisha usimamizi wa kodi (*tax enforcement*), kuanzisha matumizi ya mashine za kielokroniki za kutoa stakabadhi za kodi (*electronic fiscal devices*), kuongeza ujuzi katika shughuli za ukaguzi na kuweka mfumo wa usimamiaji wa kodi unaozingatia viashiria hatarishi vya uvujaji wa mapato (*enterprise wide risk management system*). Hatua hizi zimeleta manufaa kama ilivyoonyeshwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. J. Z. MBENE)]

kwenye kigezo cha ufanisi wa ulinganishi wa ukuaji wa mapato hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, takriban kwa kipindi cha muongo mmoja, ukuaji wa mapato ya kodi ni asilimia 21.5 kwa wastani ambao ni wa kiwango kikubwa. Kwa mujibu wa utafiti wa ukusanyaji mapato kwenye nchi zinazoendelea uliofanywa na Shirika la Fedha Duniani mwaka 2011, hatua za maboresho katika kusimamia mapato unaiweka Tanzania katika mifano ya nchi tatu zinazofanya vizuri zaidi. Nchi nyingine kwa mujibu wa utafiti huo ni El Salvador na Vietnam.

Aidha, katika mpango wa nne wa Mamlaka ya Mapato wa miaka mitano, *TRA* inakusudiwa kuongeza mapato ya kodi kutoka Shilingi trillion 9.5 hadi Shilingi trillion 18.8 takriban maradufu.

Mheshimiwa Spika, suala la nne lilikuwa uwepo wa kesi nyingi Mahakamani za madai ya kodi ambazo hazijatolewa maamuzi. Kamati ilibaini kuwa *TRA* inakabiliwa na kesi nyingi Mahakamani za madai ya kodi zenye thamani ya Sh.153,961,000,000/= ambazo mpaka sasa hatujui hatma yake na endapo *TRA* itashindwa, basi Serikali itapata hasara yenye thamani hiyo. Aidha, *TRA* iliomba msaada kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wizara ya Fedha wa kusaidia ili hukumu ya kesi itoke mapema, lakini mpaka sasa kesi hizo hazijaisha na Serikali iko kwenye hatari ya kupata hasara zenye thamani hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la kutolewa kwa maamuzi ya kesi za kodi hushughulikiwa na mhimili mwingine wa Mahakama ambao una taratibu zake. Kwa msingi huo, Serikali haina maamuzi ya moja kwa moja kuhusu suala hilo. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikiiandikia uongozi wa Mahakama ili kuwaomba kuharakisha uamuzi wa kesi hizo kwa lengo la kuwezesha kukusanya mapato ya Serikali mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala mkataba wenye utata wa leseni za udereva Tanzania. Kamati ilibaini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. J. Z. MBENE)]

kasoro kadhaa katika baadhi ya vipengele vya masharti ya mkataba wa utengenezaji wa leseni za udereva ulioingia kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Kampuni ya *M/S Truck Innovations Ltd.* ya nchini Israel ambavyo zinaiweka Serikali katika hatari ya kupoteza mapato makubwa. Mkataba wa leseni za udereva umeendeshwa kwenye msingi kwa *Build Operate and Transfer (BOT)*.

Msingi wa mkataba ulikuwa ni kwa mkandarasi kugomboa gharama zake, wakati mkataba huo unaandaliwa ilitarajiwa kuwa leseni 800,000 zingetosha kugomboa gharama hizi. Mkataba ulisainiwa katika bei ya kubadilisha ya fedha ya Sh. 1,300/= kwa Dola bei ambayo imebadilika hadi kufikia Sh. 1,600/= kwa Dola katika muda wa mkataba. Mabadiliko hayo ya thamani ya Dola ambayo hayakutarajiwa wakati mkataba unasainiwa yalitokana na kuyumba kwa uchumi wetu hususan wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani na ilisababisha kuwepo kwa gharama zisizogombolewa hata baada ya leseni laki nane kutimia.

Mheshimiwa Spika, mkataba huo ulitaka kuwa kabla ya kukabidhiwa ufanyiwe ukaguzi wa *CAG*. *CAG* anafanyia ukaguzi mkataba huu pamoja na hesabu za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 ambao umekwishanza na taarifa ya *CAG* itatolewa kabla ya tarehe 31 Desemba.

Aidha, uwepo wa *escrow account* baada ya kukabidhiwa unalenga kuhakikisha kuwa *TRA* inakuwa na taarifa kamili za *source code* zilizotumika katika mradi wenyewe. Kwa sasa mkandarasi pekee ndio mwenye *source code* hiyo. Baada ya kukamilika kwa mkataba na *TRA* kupewa uendeshaji wa mradi, mkandarasi ataweka *source code* kwenye *escrow account* ili kuwezesha *TRA* kupata taarifa za kiufundi wakati wowote zitakapohitaji kupitia kwenye hiyo *escrow account*.

Mheshimiwa Spika, upungufu mwingine ni katika utekelezaji wa mpango wa kupeleka umeme vijijini unaosimamiwa na *REA* chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. J. Z. MBENE)]

Kamati imebaini kuwa fedha zinazopelekwa REA kwa ajili ya umeme vijijini zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka na hivyo kusababisha kutokamilika kwa kiasi kikubwa kwa malengo ya Wakala huo.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa fedha za bajeti zilizokuwa zinapelekwa REA kwa miaka ya nyuma kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali, ilitokana na kutokuwa na vyanzo vya mapato visivyokuwa vya uhakika. Lakini kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali imeanza kutekeleza Sheria ya tozo ya mafuta. Chanzo hiki ni cha uhakika kwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wakala wa Umeme Vijijini hivyo upungufu wa fedha unatarajiwa kutokuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni ulipaji wa madeni ya miaka ya nyuma uliofanywa na Wizara ya Ujenzi kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Kwa vile Kamati imeagiza kufanyika kwa ukaguzi maalum (*special audit*) utakaofanywa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivyo Serikali itasubiri taarifa hiyo ili iweze kuyafanyia kazi mapendekezo yatakayotolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ulipaji usioridhisha wa deni ambalo Serikali inadaiwa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa PSPF, ni kweli kwamba kumekuwa na ulipaji mdogo wa deni la Serikali kwa PSPF. Hali hii imesababishwa na ukubwa wa deni ikilinganishwa na hali ya upatikanaji wa fedha. Hata hivyo Serikali imedhamiria keundelea kulipa deni hilo kwa mwaka wa fedha kwa kadri bajeti itakavyoruhusu. Shilingi bilioni 60 zimelipwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kwa mwaka huu wa fedha Serikali imepanga kulipa Shilingi bilioni 50.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni dhamana zilizotolewa na Serikali kwa Mashirika ya Umma. Serikali inapotoa dhamana huwa inazingatia masharti na vigezo vilivyopo kwenye Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Hata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. J. Z. MBENE)]

hivyo dhamana zilizotolewa kwa Bodi ya Mkopo na *TFC* zilizingatia unyeti na uharaka wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Mashirika hayo. Hata hivyo, Bodi ya Elimu ya Juu imeshaanza kulipa *PPF* deni lake na inaendelea kulipa na kwa hali hiyo, hakuna tatizo la kutokulipwa dhamana hizo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala vilevile la maamuzi yenye shaka ya utengefu wa madeni yaliyofanywa na Shirika Hodhi la mali ya Serikali la (*CHC*). Kiasi cha madeni ya Shilingi bilioni 98 yaliyorithiwa na *CHC* kutoka *PSRC* na utengefu (*Provision for doubt to debts*) ilikuwa wa Shilingi bilioni 83 ambayo sehemu kubwa ni riba ya madeni husika, ni uamuzi uliofikiwa na kuidhinishwa na Bodi. Uamuzi au utaratibu huu unakwenda sambamba na kukubaliana na taratibu za utengenezaji na utoaji taarifa za Hesabu wa Kimataifa na ni utaratibu uliokuwa ukifuatwa pia na *PSRC* kabla haijarithiwa na *CHC*.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba madeni haya yaliingia kati ya mwaka 1995 na 2004 ambayo ni kati ya miaka 7 na 16 hadi hesabu za mwaka 2011 zilipokuwa zinatengenezwa. Riba ilizalishwa kwa sababu madeni hayakulipwa kwa wakati. Hivyo basi, utengefu wa madeni yenye wasiwasi ulitokana na madeni kutokulipwa kwa wakati. Lakini pamoja na hayo, hii haiondoi jukumu la *CHC* kuendelea kufuatilia madeni haya na kuhakikisha kuwa yanalipwa kadri inavyowezekana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Salum.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):

Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi hii kuweza kuchangia hoja zilizoletwa mbele yetu kwa kutoa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

ufafanuzi na kutoa maelezo kwa baadhi ya hoja ambazo zimo katika taarifa ya Kamati. Lakini vilevile hoja ambazo zimekuwa zikitolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge.

Kwa ufupi, hoja zote ni za msingi lakini nyingine pengine zinatokana na upungufu tu wa taarifa ambazo sisi kama Serikali tunazo, lakini Waheshimiwa Wabunge na wao wanazo. Kwa hiyo, kwa upande wangu nitajikita zaidi katika ku- *reconcile* taarifa mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kulikuwa kuna hoja ambayo imepigwa sana kelele na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kuongezeka kwa misamaha ya kodi. Misamaha ya Kodi inayotolewa, msingi wake ulikuwa ni kuweza kuvutia wawekezaji, na baadhi ya misamaha hiyo imo katika sheria. Kwa hiyo, ilikuwa ikitolewa kutokana na sheria zilizokuwa zimewekwa. Lakini kadri tunavyokwenda, wakati *investments climate* inaimarika, misamaha ya kodi nayo inaanza kuwa kero, pengine kwa sababu imezidi zaidi ama pengine wengine wanapata zaidi, lakini hatuoni labda *return* yake na vitu kama hivyo.

Katika stadi ambazo sisi Wizara ya Fedha (*Commission*) tumefanya *analysis* na matokeo yake tumeona kwamba misamaha ya kodi kufikia mwaka 2012/2013 imepungua. Wakati mwaka 2011/2012 ilikuwa ni asilimia 4.3 ya pato la Taifa, stadi yetu ambayo tulifanya, tumegundua kwamba kwa sasa 2012/2013 misamaha ya kodi kwa pato la Taifa imefikia asilimia 3.1. Hiyo ni kwa sababu tunasikia kilio na sisi kama Serikali kwa sababu ndio wenye mamlaka na jukumu kubwa la kutekeleza kupeleka maendeleo kuharakisha maendeleo kwa wananchi na kwa sababu kuna misamaha mingine tayari imeshakuwa imepitwa na wakati, tumechukua hatua mbalimbali. Tumefikia asilimia 3.1 na *intiative* zote zimeonekana, tumepitisha Wabunge, tumepitisha kwenye *Finance Act* ya mwaka 2012/2013, 2013/2014, tunakuwa tume-*reduce* misamaha ya kodi mbalimbali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

Kwa hiyo, kwa sasa tuko asilimia 3.1, lakini hatuishii hapo. Tunaendelea na kwa sasa hivi tumeshakamilisha *VAT Reform Act* kwa sababu misamaha mingi ya kodi inatokana na *VAT exemptions*.

Kwa hiyo, Sheria ya Maboresho ya *VAT* tumeshakamilisha na sasa hivi tumeshatayarisha Waraka wa Baraza la Mawaziri, tukishapata *blessing* ya Baraza la Mawaziri Waheshimiwa tunaleta hapa Bungeni tunategemea kupata *support* yenu kubwa sana. Lengo, tunataka kufuta baadhi ya misamaha ya kodi ambayo kwa dunia ya leo, kwa uchumi wetu wa Tanzania wa leo, haiwezi ku-*reduce any more*, lakini pale ambapo misamaha ya kodi ni lazima, basi tutai-*reduce* katika kiwango ambacho tunahakikisha kwamba itakuwa *effective* kwa uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, hilo ndiyo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kulikuwa kuna jambo lingine la msingi ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisema kuhusiana na kumwezesha *CAG* kupata fedha na kukagua Vyama vya Siasa. Sisi kama Serikali hatuna tatizo na hilo *as long as Controller and Auditor General* anaingiza vifungu katika bajeti yake, sisi tutampa fedha za kuweza kufanya hiyo kazi kwa sababu ipo katika mamlaka yake. (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisema, ni kuhusiana na deni kubwa la Taifa. Hili ni jambo ambalo tumekuwa tukilizungumza mara kwa mara na limekuwa lijitokeza katika michango yote ya Waheshimiwa Wabunge. Labda pengine tutaendelea kuelimishana, tutaendelea kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maeneo, lakini vilevile Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba tuone sasa hiyo mikopo ambayo Serikali inachukua hasa inakwenda kutekelezwa nini? Sasa mikopo hiyo imechukuliwa, hizo taarifa zote tunazo, Waheshimiwa Wabunge tutawapatia taarifa hizo kwa sababu hatuna la kuficha, tunachukua mikopo kwa ajili ya kuwekeza katika miundombinu ya uchumi wa nchi hii na miundombinu hiyo ya uchumi ndiyo ambayo itafaidisha, maana kama hujawekeza kwenye uchumi huwezi kufika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

pahali popote. Tunachukua mikopo, tunawezeza katika miundombinu ya uchumi.

Deni limefikia *around 23 trillion* kweli ya *GDP*. Lakini kukua kwa deni hakumaanishi kwamba deni kutoka mwaka 2012/2013, 2013/2014 ni kwamba ni mikopo mingi mipya ambayo Serikali imechukua, hapana. Deni lililopo la Taifa hususan hilo deni la mikopo ya nje, lina-*constitute* hata hiyo mikopo ambayo ilikuwa imechukuliwa wakati huo, leo hii ndiyo ina-*mature* na tunaanza kulipa.

Kwa hiyo, siyo kama tu tumechukua *lumpsum* kuanzia mwaka 2012 mpaka mwaka 2013 tumeingiza pale kwenye deni la Taifa, limeongezeka kwa sababu hiyo, hapana. Kuna vitu vingi vina-*constitute* deni la Taifa. Lakini kuna maeneo ambayo labda pengine Waheshimiwa Wabunge wengi sana walitaka tuelezee kifupi tu madeni labda haya karibuni tuliyokuwa tumeyachukua tumewezeza wapi? Taarifa zipo, labda tu kwa ufupi sana tunaweza kusema kwamba Serikali imekopa kweli, hilo deni la Euro milioni 61.

Mheshimiwa Spika, haya ni madeni ya mikopo ambayo tumechukua mwaka 2010/2011 na 2013/2014 tulikopa Euro milioni 61 ambazo ni sawa na *128 billion* kutoka *HSBC*, tumewezeza kwenye mtambo wa kufufua umeme Megawati 60 Mwanza. Serikali tumekopa kwingine Dola za Kimarekani 103 huko *HSBC* tumewezeza katika mtambo wa kufua umeme Megawati 100 Dar es Salaam, Ubungo. Tumekopa Dola milioni 350 kutoka Benki ya *Credit Trees* kugharamia ujenzi wa barabara pamoja na madaraja mbalimbali. Sehemu zote hizo ni katika miundombinu ya kiuchumi.

Eneo lingine ambalo linahusiana na hili ni kuhusiana na mikopo ya kibiashara, hususan Mheshimiwa Hamad Rashid analifahamu vizuri. Labda Waheshimiwa Wabunge, tufahamu kwamba wakopeshaji dunia hii wako wengi sana na tunapata watu wengi sana. Tunapata watu wengi sana ambao wanakuja, sisi tunaweza tukatafuta hii hela *fine*, wote tunawapokea. Lakini haimaanishi kwamba wote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

tunawachukua kwa sababu kuna vigezo maalum ambapo sisi Serikali tunaangalia wapi na nani tumkope.

Kwanza ni urahisi wa ule mkopo wenyewe ni (*cost of borrowing*), gharama ya ule mkopo wenyewe. Kila anayekopesha anatofautiana. Kwa hiyo, sisi kwa sababu ya hali ya uchumi wetu, mkopo tunautaka. Kwa hiyo, tunaangalia ni wapi ambao wana gharama nafuu. Hiyo ni *logic*, hata katika maisha ya kawaida ya binadamu, nadhani Wabunge wote humu ndani sijui kama kuna Mbunge ambaye hana mkopo. Kwa sababu ndivyo hali halisi ilivyo. *Financial markets* zina-*exists* kwa sababu ya kumwezesha *lender* na *borrower* ku-*exchange* hizo *finance resources* a *cross time*. Kwa hiyo, hiyo ipo.

Tukienda kukopa maana yake siyo kama ndiyo tunategemea, hapana. Waheshimiwa Wabunge, tunapokwenda kukopa tunaweka hela yetu ambayo tulikuwa tuitumie baadaye ndiyo tunaiweka. Mtu anakwambaia una kitu kipi cha kuweze kuni-*convince* nikukopeshe? Kwa hiyo, *it is the same*. Ni hela yako isipokuwa unai-*vary* matumizi yake baina ya *time*. Wewe unataka kutumia leo, yule anayekukopesha anasema nitastahimili, mimi changu nitatumia baadaye, maana ndipo utakaponilipa. Kwa hiyo, inategemea *cost of borrowing* how *cheap is it*. Wengi wapo, lakini wanatofautiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni *timing*. Anakuja mtu anataka kukukopesha, ndiyo *we need the money*. So, anasema yeye ataleta baada ya miaka mitatu, baina ya miaka minne; *no, we need the money now* kwa ajili ya kuwekeza, hatutaki baada ya miaka mitatu au minne. Kwa hiyo, vipengele pamoja na hivyo vingi vinafanya tuchague nani na ni yupi wa kwenda kumkopa na kwa kiasi gani. Kwa hiyo, hayo yapo mengi, Waheshimiwa tunakuwa tunapata huo utaratibu kidogo kidogo na mwisho nadhani tutakuwa katika njia moja.

Mheshimiwa Spika, tukisema kwamba tusikope, nadhani hilo haliwezekani maana ni lazima tuambiane ukweli.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

Ingawa *resources* tunazo, lakini *resources* zetu ni za muda mrefu zaidi. Sisi tunataka kuwekeza leo, tunataka kuwekeza jana ili hizi *resources* tunazowekeza leo zi-*generate revenue* kuweza ku-*service* huo mkopo ambao tutalipa baadaye. Kwa hiyo, cha msingi hapa tunachukua mkopo; wapi tunawekeza, ndilo la umuhimu. Kusema kwamba hatukopi siyo jambo la ukweli.

Mheshimiwa Spika, juzi Marekani wame-*increase debt ceiling* yao. Uchumi wa Marekani wameongeza *debt ceiling*. Kwa hiyo, hili haliwezekani. Lakini uzuri wetu sisi kama Tanzania, tunasema siku zote kwamba deni linaendelea kuhilimika.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukomo wetu wa kukopa kwa *GDP* ni 50, lakini leo ndio kwanza tuko 19.3. Waheshimiwa Wabunge wengine wataweza kusema kwamba basi *why don't we go* kukopa leo? *No!* Ukomo upo 50, lakini kwa kila mwaka tunakuwa *guided on how much* tunakopa. Kwa hiyo, *as long as* ukomo uko 50 lakini bado tunakuwa *guided* kwamba kwa kila mwaka kutokana na ukuaji wa uchumi wenu, hiki ndicho kiwango cha ninyi kwenda kukopa. Lakini pengine bado tunahimili deni letu kutokana na *a present value* ya *debt* pamoja na *exports* zetu.

Bidhaa zetu tunazosafirisha, ukifanya kwa hesabu zetu za leo ukilinganisha na deni letu, tunahimili. Ndio kwanza tuko 70.7% na ukomo wetu kutokana na uchumi wetu kutokana na bei yetu ya leo ni 200. Ndiyo kwanza tuko 70.7. Kwa hiyo, *it is a little bit technical thing*, lakini tutajitahidi kwa sababu tunataka sote twende sambamba kwenye eneo hili, kusiwe kuna mkanganyiko wa hizi taarifa, tutajitahidi sisi kama Serikali tuwe tunatoa taarifa hizi mara kwa mara. Kwa hiyo, *all in all* deni linahimilika na tutaendelea kukopa, kikubwa tutaangalia vyanzo ambavyo vitatupa unafuu wa mkopo huo. (*Makofi*)

Kuna jambo lingine ambalo limepigwiwa sana kelele na Waheshimiwa Wabunge kwamba Hazina tunachelewesha sana fedha kutoka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwanza, naomba tufahamu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

kwamba ili fedha itoke, Hazina kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania inakusanya fedha hii kwa mapato yetu ya ndani. Inakusanya hii fedha, ikishakuipata ndiyo inaipeleka. Hazina haina *mandate* ya kuweza ku-*hold* fedha tu ikakaa nayo isitoe. Inakusanya, inapeleka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, kuna mchakato wake ili fedha itoke kwa upande wa miradi ya maendeleo. Tuisahau *role* ya Tume ya Mipango katika hili. Tume ya Mipango ina *role* kubwa, wao hasa ndiyo wenye mamlaka ya kuweza kufanya *analysis* na *assessment* ya *proposal* za miradi ya maendeleo kabla ya kupeleka Hazina kutolewa hizi fedha.

Kwa hiyo, tuisahau hiyo *role* ya Tume ya Mipango. Lakini kwa *data* tulizonazo, kuanzia kipindi cha Julai mpaka Novemba, 2013 Tume yetu ya Mipango kiasi cha fedha ambazo ni za ndani, (*domestic resources*) ambazo zimeidhinishwa na Tume ya Mipango zinafikia *1.41 trillion* katika kipindi cha Julai hadi Novemba. Taarifa zetu za *exchequer* katika Hazina mpaka Novemba, 2013 tumetoa *1.08 trillion* ambayo ni sawa na asilimia 76.6 ya fedha zote ambazo zimeidhinishwa na Tume ya Mipango kwa miradi hii ya maendeleo.

Kwa hiyo, hapa nadhani kunakuwa kuna changamoto vilevile ya mkanganyiko wa hizi taarifa. Sisi taarifa zetu zinaonesha kwamba hizi ni fedha ambazo tumeshazitoa asilimia 76.6 ya fedha zetu za ndani tayari zimeshatolewa kwa ajili ya kwenda ku-*implement* miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna fedha ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri kwa upande mwingine, hizo na zenyewe nazo tumekwishazitoa lakini cha msingi Waheshimiwa Wabunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, yeye tunampa nusu saa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zilizoko mbele yetu kutoka katika Kamati zetu tatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru CAG na nizishukuru Kamati zetu kwa sababu kama nilivyosema, ni lazima tusaaidiane katika kuimarisha utendaji wa Serikali na hasa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, naamini kabisa, ushauri wao na yale wanayoyaona, yatatusaidia sana katika kuboresha utendaji wetu.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ambazo zimezungumzwa, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeguswa katika maeneo kama manane hivi. Sehemu ya kwanza ni *issue* ya kwamba kuna Halmashauri zimepewa fedha nyingi sana kuliko vile ambavyo ilitakiwa kuidhinishiwa. Mifano ambayo imetolewa ni Halmashauri ya Jiji la Tanga, Korogwe pamoja na Mbarali.

Sasa kwa upande wa Mbarali, nakiri ni kweli kwamba Halmashauri ilipelekewa fedha za MMES nyingi kuliko ambavyo ilistahili kupelekewa. Lakini namshukuru CAG na pia nichukue nafasi kumshukuru sana Mheshimiwa Kilufi - Mbunge wa Mbarali kwa jinsi ambavyo ameshirikiana na Ofisi yangu katika kuchukua hatua katika eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ilikuwepo katika taarifa ya CAG, lakini ilikuwa kidogo haikai vizuri na haikuwezeshi kuchukua hatua. Lakini alituletea, alinisaidia, na mimi mwenyewe mwezi Januari nilikwenda Mbarali, nilifanya Mkutano na watumishi pamoja na Waheshimiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

Madiwani na pia nilifanya kikao na Kamati ya Ulinzi na Usalama na niliwaelekeza nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa sababu kutokana na maelekezo yetu wameweza kuwafukuza watumishi wafuatao, naomba niwataje. Wamemfukuza Mweka Hazina ambaye ni Bwana Frednand Manyele, Bwana Bakari Ramadhani ambaye alikuwa Afisa Mipango, wamemfukuza Bwana Mikidadi Mwazembe ambaye alikuwa Mtendaji wa Kata, Bwana Ponsiano Ng'wando ambaye pia alikuwa ni Mtendaji wa Kata na pia wamewapeleka Mahakamani hao niliowataja pamoja na Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Ubaruku ambaye ni Bwana George Mbilla kutoka Chama cha CHADEMA, ambaye yeye pia alishirikiana na watumishi hawa katika kuiibia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mkaguzi wa Ndani katika Halmashauri hiyo amefukuzwa. Lakini siyo hivyo tu, tuliagiza kufanyike tena ukaguzi maalum kutokana na malalamiko ambayo mengi aliyaleta Mheshimiwa Mbunge. Baada ya kufanya huo ukaguzi maalum, wapo watumishi wengine ambao wamebainika kwamba na wenyewe pia walishiriki kwa namna moja au nyingine katika kuiletea hasara Halmashauri na tayari Halmashauri imeanza mchakato wa kuwachukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, watumishi hao ambao tayari wameshapewa *charged* kwa maana kupewa mashtaka na Halmashauri ili na wenyewe waweze kuwachukulia hatua nyingine ni pamoja na Bwana Emmanuel Makalla kutoka Kitengo cha Manunuzi, pia Bwana Rajab Ngarawa - Afisa Mapato, aliyekuwa Kaimu *DED* - Bwana Swege Kaminyoge na Afisa Maendeleo ya Jamii - Bwana Mganga Ngurumo na Mhasibu - Bwana Wilfred Mbelo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo kwamba hatuchukui hatua na ndiyo maana pale tunaposema Waheshimiwa Wabunge watusaidie tushirikiane pamoja na Waheshimiwa Madiwani ni kwamba inawezekana. Tukitegemea Waziri wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

TAMISEMI atamfukuza Mtendaji wa Kata au atamfukuza Mweka Hazina ni kwamba akienda Mahakamani akinishtaki atanishinda kwa sababu kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2007, Mamlaka ya Nidhamu ya Wakuu wa Idara pamoja na watumishi wengine ni Halmashauri husika. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Kilufi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie lile la Tanga ambalo inaonesha kwamba kuna zaidi ya Sh. 2,016,000,000/= zilipelekwa huko, kama wengine ambavyo wamesema kwamba Serikali tulijipasia. Hapa hakuna ukweli, Serikali haikujipasia, isipokuwa kilichojitokeza ni makosa ya yule ambaye amekwenda kukagua kule. Hili ni kosa la Ofisi ya CAG. Kutokana na utaratibu mpya wa sasa hivi uliopo wa IPSASs kuna fedha za nyuma ambazo na zenyewe zinatakiwa ziingizwe wakati wa ufungaji wa mahesabu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa upande wa Tanga na Korogwe hakuna fedha ya ziada iliyopelekwa, fedha zote zilizokuwepo pale ni fedha halali, zimepitishwa na Bunge lako Tukufu, isipokuwa ni matatizo ya yule mtaalam ambaye alitumwa na Ofisi ya CAG kwenda kukagua, nadhani IPSASs kidogo yeye ilimpiga chenga. Hata tulipokutana *St. Gasper*, kwa sababu tuna utaratibu wa kukutana kila mwaka, kukutana na Wakurugenzi wa Halmashauri, Waweka Hazina na Wakaguzi wa Ndani na huwa tunamwalika CAG anakuja na hili lilijitokeza; na Mweka Hazina wa Jiji la Tanga alisema kwamba ana ushahidi, anajua taratibu ziko hivyo kwamba yule Mkaguzi alikokotoa vibaya, lakini hakuna fedha iliyozidishwa.

Mheshimiwa Spika, hizo fedha ambazo yeye anasema zilizidi, kulikuwa na fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya Mfuko wa Afya ambazo ni Sh. 447,788,650/= ziko kwenye bajeti, fedha za TACAIDS ziko kwenye bajeti, fedha za Miji Mkakati ambazo ni Sh. 12,000,000/= na pia kulikuwa na fedha ambazo ni nyingi hapa zinaonekana Sh. 1,197,947,537/= ambazo zilikuwa ni za kuwalipa fidia wananchi ambao walikuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

wanapisha maeneo yao ili kufanya upanuzi wa bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kusema ukweli, kwa kule Mbarali ni kweli limejitokeza na hatua zimechukuliwa. Lakini kwa upande wa Tanga na Korogwe ilikuwa ni matatizo ya kiuhasibu ya ukokotoaji kwa yule ambaye alikwenda kukagua na pia kama labda Kamati ina wasiwasi, naiomba, inaweza ikamwita CAG na hili ataliki na kwa sababu mengi tulishajibu kama ambavyo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Urativu na Bunge) - Mheshimiwa Lukuvi, alisema kwamba mengi tulishayajibu na yalishakwisha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imezungumzwa sana hapa na ikavuta hisia ni *issue* ya kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kupitia Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa kwamba imetumia zaidi ya Shilingi milioni 600 fedha za wafadhili na kwamba Hawa Ghasia ameshindwa kuisimamia Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na kwamba anasababishia wananchi madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba yale mengi ambayo yalikuwa yanazungumzwa pale mimi sidhani kama ni maneno ya wafadhili. Yale ni magazeti, waandishi wenyewe huwa wanapenda yepi yanayowapendeza, lakini pia wanapenda kuangalia yepi yatavuta hisia za watu na sisi wenyewe kwa kiasi kikubwa kwa hizi siku mbili nadhani tumeuza sana kwa sababu ile ya maboresho ya Serikali za Mitaa yalikuwa ukiyataja kwamba na Hawa Ghasia amehusika na hata magazeti yalivyokuwa yanasema, yalikuwa yanaleta picha kwamba Hawa Ghasia ni mwizi na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, napenda nikiri kwamba ulifanyika ukaguzi wa mahesabu ya fedha za maboresho kwa mwaka wa fedha 2009/2010, 2011/2012 na ukaguzi huu ulifanyika tarehe 18 Februari, 2012 hadi mwezi Juni, 2011 na baada ya ukaguzi huo, kweli yalionekana, yaani waliangalia kwa undani mafanikio na changamoto ambazo zipo katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

maboresho ya Serikali za Mitaa. Baada ya kuangalia, yalikuwepo mafanikio, lakini pia kulikuwa na changamoto. Mojawapo ni katika baadhi ya maeneo ambayo yalionekana kulikuwa na matumizi ambayo kwa kweli hayafuati taratibu.

Mheshimiwa Spika, sasa ofisi yangu ilifanya nini? Au mimi baada ya kuletewa ile taarifa tulifanya nini? Kwanza, kwa sababu katika huu mradi kulikuwa akaunti mbili; akaunti za Dola na akaunti za Shilingi. Kwa hiyo, kulikuwa na mkanganyiko, maeneo mengine ambapo ilihitajika watumie Dola na Dola wanazo, walikuwa wanatumia Shilingi; na maeneo ambayo walikuwa na Shilingi walitakiwa watumie Shilingi na wanazo walikuwa wanatumia Dola. Kwa hiyo, kitu cha kwanza tulichofanya tarehe 23 Januari, 2013 tulisimamisha matumizi ya fedha za Dola katika mradi huu. Tulisema sasa hivi matumizi yote yatakuwa ni kwa Shilingi.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine ambacho nilikifanya ni kusimamisha Mkataba wa watumishi wale ambapo ni Bwana Malya na Bwana Mwaipingu kama sikosei. Mmoja alikuwa ni Mhasibu na Mshauri wa masuala ya fedha ambao walikuwepo katika Mradi wa Maboresho ya Utumishi wa Umma. Tulisitisha mkataba wao kwa sababu walijiriwa kwa mikataba, na pia tulisitisha kiinua mgongo chao, tulihakikisha kwamba hawapewi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambayo niliichukua ni kuivunja Sekretarieti iliyokuwepo na kuunda Sekretarieti mpya kwa sababu kama unavyofahamu hawa wafadhili mara nyingi wanapenda hii miradi iwe pembeni pembeni, isiwe ni sehemu ya Wizara. Lakini pia tulimwandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumwomba ushauri, nini tufanye kwa sababu hawa wote walikuwa ni watumishi ambao wamestaafu, walijiriwa kwa mikataba na tuliteua watu wengine waende wakasimamie mradi. Pia tuliundoa ule mradi kwa sababu mwanzo ulikuwa unawajibika kwa Mkurugenzi wa Idara, lakini baada ya kuona haya matatizo, tulitaka sasa wale wanaosimamia mradi wawajibike moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Wizara.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

Pia, tuliwaandikia wenzetu wa Toyota ambao na wenyewe tulipeleka madai kwa Kampuni ya Toyota ambayo ilibainika kupokea fedha zaidi ya stahili wakati wa manunuzi ya magari.

Mheshimiwa Spika, pia suala lingine ambalo nataka niliweke wazi siyo Shilingi milioni 600. Baada ya ufuatiliaji ni tulikuta ni Sh. 444,088,330/=. Kwa hiyo, suala la kuchukua hatua, tumechukua, na pia ieleweke kwamba haya ni mahesabu ya mwaka 2009/2010 - 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maelezo kwamba wafadhili wamesema wanamshangaa Rais kwa kumchagua Hawa Ghasia Wizara kubwa ambayo inahitaji mtu makini, kwa kweli yale ni maneno ambayo waandishi waliamua kuandika na ningefurahi sana kama watu wangeleta ile kauli ya wafadhili wenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilizungumzwa sana ni kwamba watumishi wabadhilifu wanapogundulika hatuwachukulii hatua na badala yake tunawahamisha kuwapeleka katika Halmashauri nyingine kwamba hatuchukui hatua. Halmashauri ambazo zilitajwa ni kama Halmashauri ya Kishapu, Bagamoyo, Mwanza na Mvomero.

Mheshimiwa Spika, watumishi 14 waliohusika na ubadhilifu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, wote wamesimamishwa kazi na masuala yao yako TAKUKURU na kwa *DPP*. Sasa kwa uwezo wangu kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, siwezi kumharakisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mahakama. Mimi ninapoishia ni kumvua madaraka, kumsimamisha kazi, wale wengine ndio sasa wanatakiwa waende na utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, hata ukienda kwa upande wa Bagamoyo, hatua tumechukua, kesi zipo Mahakamani na kati ya wale yupo Mkurugenzi Bibi Rhoda Msemwa; wakati anapelekwa Mahakamani alipelekwa akiwa kama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

Mkurugenzi tayari sisi Ofisi yetu tumeshamvua madaraka.
(Makofi)

Pia, alitajwa Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza kwamba tumemhamisha kumpeleka Dar es Salaam. Mpaka sasa hivi Ofisi yangu hatuna tuhuma zozote ambazo tunaweza kumfukuza Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza. Kwa hiyo, tusingeweza kumhamisha.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhamisha Watendaji ni suala la kuboresha utendaji katika Halmashauri. Wapo Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamekuja kulalamika kwamba katika Halmashauri yangu Watumishi wamekaa zaidi ya miaka 15 au 14. Ni kweli mtumishi akikaa kituo kimoja zaidi ya miaka 10 kwa kweli atafanya kazi kwa mazoea, kwa hiyo, tunawahamisha katika kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Spika, pia lilizungumzwa suala la Mvomero na ilizungumzwa kwamba Mhasibu aliyehusika katika kujenga jengo kwa Shilingi milioni 400 amehamishwa, amepelekwa Ilala.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu zetu, haiwezekani mtumishi mmoja Mhasibu peke yake akaamua kwamba jengo hili lijengwe kwa Shilingi milioni 400. Tunafahamu kwamba katika kila Wilaya na kila Halmashauri tuna vitengo na Kamati za Manunuzi na katika kufuatilia ujenzi wa Jengo la Mvomero ni kwamba jengo lile utaratibu wa kufanya makisio, utaratibu wa ujenzi, usimamizi na ujenzi wenyewe vyote vilikuwa chini ya *TBA*. Kwa hiyo, Mhasibu hakuhusika. Lakini hata hivyo, pamoja na *TBA* kwamba zile gharama za Shilingi milioni 400 zimefuatiliwa na zimeonekana ni halali kufuatana na mazingira ya eneo lile kwamba zile nyumba zilizojengwa na wengine bila kufuata taratibu ambazo *TBA* wamefuata, zote zina nyufa. Sasa lile jengo limejengwa kwa ubora ambao kwa kweli ulizingatia kuzuia nyufa.

Mheshimiwa Spika, pia lilizungumzwa suala la sheria ndogo kwamba zinakaa muda mrefu sana bila kuwarejeshea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

katika Halmashauri na suala hili hata tukikutana na Mameya, wamekuwa wakilizungumza. Mara ya mwisho niliowaomba kwamba sasa hivi mnapoleta sheria, badala ya Mkurugenzi kumwandikia Katibu Mkuu, niliwashauri Wenyeviti wa Halmashauri na Mameya zile barua waniandikie mimi, kwa sababu kwa uzoefu wangu nilikuwa naona ukipeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hazichelewi na wala mezani kwangu hazichelewi.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi katika mwaka huu wa fedha tulipokea sheria ndogo 39, na kati ya hizo, 29 tayari zimesharejeshwa kwa wenyewe, zimeshaanza kufanya kazi na sheria 10 tumezirejeshwa kutokana na makosa madogo madogo yaliyokuwepo. Lakini tunakubaliana na ushauri uliokuwepo wa kutoa mafunzo kwa Wanasheria na sisi tumepanga kufanya hivyo na pia tunakubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati kwamba tuwe na sheria za mfano. Kwa hiyo, tumetengeneza sheria za mfano ambazo tutazipeleka kwenye Halmashauri ili na wenyewe wawe wanafanya *modification* kufuatana na mazingira ya maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa ni suala la ukaguzi wa miradi kwamba linafanywa na Kamati ya Fedha tu ambayo kwa kweli kimsingi haiwezi kukagua maeneo yote na miradi ni mingi katika Halmashauri. Sisi tunakiri ni kweli tumeliona na tunaunga na Kamati kwa waliyoyasema na wote waliosema.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumze kwamba tumebadilisha Kanuni zetu za Halmashauri, sasa hivi tunaruhusu Kamati zote zitakwenda kukagua miradi yao ya Sekta zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika baadhi ya maeneo unaambiwa kuna mradi hewa, sasa unashindwa kuamini kwamba Kata hiyo wanasomewa taarifa kwamba limejengwa bwawa, mfano Kishapu, na bwawa halipo. Unashangaa, hivi Mheshimiwa Diwani alishindwa kusema kwamba kwangu hilo bwawa mnalolizungumza halipo? Kwa hiyo, kwa kuona hivyo ndiyo maana tukaamua kwamba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

katika sheria zetu ambapo lengo kwa kweli ni kuhakikisha tunaboresha usimamizi, tumesema Waheshimiwa Madiwani kabla ya kwenda katika Baraza la Halmashauri, wafanye vikao katika Kata zao, wakague miradi ya Kata zao na waandike taarifa ambayo wakienda katika Baraza la Madiwani, Mheshimiwa Diwani atoe taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Kata zake. Yote hiyo ni katika kuimarisha mifumo ya usimamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hatukuishia hapo, tumesema Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi, kila wanapofanya Baraza la Madiwani waulizwe maswali ya papo kwa papo kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu anaulizwa ili kuwapa fursa Waheshimiwa Madiwani na wenyewe kuweza kupata uelewa wa mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tunafanya kazi sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naliomba kwa Waheshimiwa Wabunge, nimekuwa nikirudia kwamba ni lazima tusaidiane. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI peke yake haiwezi ikaenda kusimamia kila Halmashauri. Mimi nakwenda na ninafanya ziara, Manaibu wangu wanafanya ziara, lakini huwezi kwani watakukwepa tu. Ndiyo maana mimi nampongeza sana Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Obama na Mheshimiwa Mahanga kwa sababu wanakuja wanakwambia ukienda tazama hiki, kafanye hiki na hiki. Kwa hiyo, unapokwenda na wewe hata ukipangiwa ratiba na wewe unakuwa na maeneo ya kuyatazama.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mimi humu ndani Wabunge zaidi ya asilimia 70 nimemfuata mmoja mmoja nikiwauliza vipi Halmashauri yako? Vipi Mkurugenzi wako? Zaidi ya asilimia 80 hapa wanasema Wakurugenzi wao kwa sasa hivi ni wazuri. Sasa ninashangaa, hao Wakurugenzi ambao tukikaa hapa tunawasema, wako wapi?

Mheshimiwa Spika, leo wakati wanauliza nimetoka nje mimi nilikuwa na Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Msigwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

na Mheshimiwa Mahanga; katika maongezi tu ya kawaida nikawauliza, hebu niambieni; Mheshimiwa Msigwa kasema Mkurugenzi wake ni mzuri mzuri, kamsifia; Mheshimiwa Mahanga kaniambia Mkurugenzi wake wa sasa hivi ni mzuri sana; akapita Mheshimiwa Leticia Nyerere nikamwita nikamwambia mimi nafanya *research* hebu niambie Mkurugenzi wako wa Kwimba, akasema Mkurugenzi wangu ni mzuri sana, tatizo anachelewa kupelekewa fedha.

Wakati hatujaondoka pale, nikamwita Mheshimiwa Mbassa, nikamwambia Mheshimiwa Mbassa njoo samahani; hakujua tulikuwa tunafanya kitu gani. Nikamwuliza Mheshimiwa Mbassa, hebu niambie Halmashauri yako, Mkurugenzi wako yukoje? Akaniambia Mkurugenzi wangu ni mzuri, saa moja yuko ofisini, baada ya hapo anakwenda anakagua miradi na anafanya kazi sana, namshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa, nimewauliza Mheshimiwa Kamani, Mheshimiwa Shellukindo, Mheshimiwa Kayombo, Mheshimiwa Lusinde; baadhi yao ukiacha wachache ambao hawafiki hata asilimia 10, tukikaa mmoja mmoja, kwa sababu mimi nawauliza wanisaidie; sasa ninapokwenda kuzungumza na Mbunge mmoja mmoja, wananiambia Wakurugenzi wao ni wazuri. Lakini tukija humu ndani inakuwa kama vile ukiita mwizi, basi kila mtu anakimbilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya uhamisho wa Wakurugenzi, kuna watu wamekuja wanalia mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanaomba Wakurugenzi wao wasihamishwe. Siwezi kuwataja hapa, wanasema wazuri. Sasa wazuri hawa ni akina nani na wabaya ni akina nani?

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nakiri kwamba huwezi ukawa na Wakurugenzi mia moja sitini na kitu wote wakawa wazuri. Lazima katika msafara wa mamba na kenge wamo. Nakiri kabisa katika Wakurugenzi tulionao tunaweza kuwa na asilimia 20 au hata asilimia 15 ambao siyo wazuri na ndio hawa ambao tunawachukulia hatua. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

Mheshimiwa Spika, ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunaposimama, wale wazuri tuwasifie ili tuwape moyo waweze kufanya vizuri na wale wabaya nao tuwaseme kama tunavyowasema na nguvu zetu zote tuelekeze kwa wale wabaya ili na wenyewe waweze kujirekebisha wawe kama wengine. Sasa tukisema wote wabaya, tunawavunja moyo hata wale Wakurugenzi wazuri. Hata wale wabaya watawacheka wazuri; kiko wapi?

Mheshimiwa Spika, mimi kabla ya kuwa Mbunge nilikuwa mtumishi katika Halmashauri. Zamani ilikuwa zikikaa hizi Kamati, wakisoma taarifa zao walikuwa wanayasema haya haya, lakini katika zile taarifa zilikuwa zinasomwa Halmashauri zilizofanya vizuri na zilikuwa zinapongezwa na zilikuwa zinatajwa Halmashauri zinazofanya vibaya.

Mheshimiwa Spika, siyo vibaya tukiendelea hivyo, wale waliofanya vizuri tuwasifie ili tuwatie moyo na wale wabaya tuwataje na makosa yao na sisi tunaahidi tutawachukulia hatua. Kwa kufanya hivyo wale waliofanya vizuri wataendelea kufanya vizuri na wale wanaofanya vibaya kwa kweli tutahamishia nguvu kwa wale wabaya. Lakini mkisema hapa wote ni wabaya, nakata tama, yaani hata sijui sasa nianzie wapi na niishie wapi. Lakini mkiniambia bwana katika Wakurugenzi wako hawa mia sitini na kitu, 20 hawa hebu hangaika nao. Nawaahidi nitahangaika nao kuhakikisha kwamba tunawachukulia hatua kama vile ambavyo tunahangaika nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Machali alisema kwamba mimi nimekwenda kwake nimeshindwa, hakuna nilichokifanya. Mimi nilitegemea miongoni mwa watu ambao wangenisifia, angekuwa Mheshimiwa Machali. Nimekwenda kwake, nimefanya kazi; ile CD aliyosema kwamba anakukabidhi, mimi ndio niliyeagiza nitengenezewe hiyo CD, lakini yeye akaiteka ile CD akaichukua yeye kwanza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa sana hapa ni suala la mikopo ya wanawake

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]

na vijana kwenda katika Halmashauri. Ni kweli zipo Halmashauri hazipati hizo. Napenda niaahidi Kamati kwamba tutasimamia kuhakikisha pesa za mikopo ya wanawake na vijana inakwenda kama ambavyo inatakiwa. (*Makofi*)

Pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwamba hebu tuhudhurie kwenye vile vikao, mkihudhuria kwa kweli mtasaidia sana kwani mna michango mikubwa. Katika baadhi ya Halmashauri Waheshimiwa Madiwani wanapigwa chenga tu za mwili, lakini mimi nina uhakika kabisa ninyi kwa uzoefu na uelewa wenu maeneo mengine hamwezi kupigwa chenga. Kama ambavyo wengine wamesema, ni kweli katika baadhi ya Halmashauri, baadhi ya wenyeviti wetu...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na niaahidi Kamati kwamba tutayafanyia kazi yale waliyoyazunguma. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante! (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunapojadili ni lazima tutofautishe. Wewe humtegemei Waziri wa Fedha aanze kuhutubia kama siasa, kumbe yeye anazungumzia hesabu. Jamani tuelewe! Maana mnasema Spika anapendelea Serikali eti kwa sababu nimeruhusu Waziri asome. Naruhusu Waziri asome na nitaruhusu Mwenyekiti asome na nitamruhusu na Mwenyekiti mwingine asome na mwingine asome, kwa sababu majibu yao ndiyo *authority*.

Maana yake hapa mwingine tena kaniambia mimi namruhusu mtu kusema, na mwingine ana-*challenge* zile *figures* za misamaha. Sasa ile karatasi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ugawe kwa sababu tumekuruhusu uisome na uigawe hapa na hawa Wabunge wataitumia hiyo kazi kwenda kutafuta habari nyingine kama ni sahihi ama siyo sahihi. Lakini angejisemea maneno hapa, mngeanza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

kugombana na maneno yake ambayo hayana *authority* yoyote. *That paper has got an authority.* Agawe, wataisoma, wataifuatilia, watakuja kusema ulichokuja kusema Mheshimiwa Waziri siyo sahihi.

Sasa ndiyo hivyo tuyotaka, tuache maneno mengine. Wengine tunapokaa hapa ni watu wazima, tunajua *how to run the Government.* Kwa hiyo, siyo kila kitu unachokisema wewe *you are right* na anachokisema mtu mwingine siyo *right, it is not correct.*

Sasa naomba Wenyeviti wangu waanze sasa kujibu hoja zao. Hizi zilikuwa ni hoja za Wenyeviti na nianze na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa dakika zake 30, atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa dakika 30 na kisha Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwa dakika 30.

Mheshimiwa Rajab. Wewe unakuja mbele!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED - MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru. Kwanza nitoe pongezi zangu kwako, lakini vilevile baada ya kukushukuru wewe niwashukuru vilevile Wajumbe wa Kamati yangu ya Hesabu za Serikali za Mitaa lakini pia niwashukuru na wale wote ambao wameweza kuchangia hoja ama taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, zaidi shukrani za pekee nizipeleke kwa Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia kwa kweli kwa namna ambavyo ameweza kuweka baadhi ya mambo na kuyatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi waliweza kuchangia taarifa yetu na naomba nisiwataje kwa majina ila tu naomba kuwatambua wote kutokana na michango yao ambayo wamechangia kwa maelezo na mmoja ambaye amechangia kwa maandishi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende katika kutaja yale maeneo muhimu ambayo yanahitaji ufafanuzi ambayo yalitolewa michango na Waheshimwa Wabunge. Kwanza nianze na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Mheshimiwa Lukuvi ambaye amenisema kwamba hatukuipongeza Serikali. Mheshimiwa Lukuvi kupongeza siyo lazima useme kwamba nakupongeza, lakini maandiko yako ndiyo ambayo yanaonesha namna gani tukupongeze.

Nataka nikwambie tu, ni kweli vitabu vipo hivi vya majibu ya Serikali, tulichosema Kamati ni kwamba, hoja za Kamati 14 hazikupatiwa majibu. Kilichoandikwa katika hii taarifa ni kwamba hoja za Kamati za Serikali za Mitaa zilizowasilishwa tarehe 17 zimekwishafanyiwa kazi ambapo mapendekezo yaliyotolewa yamejumuishwa katika mpango mkakati wa Serikali katika kuimarisha usimamizi wa mapato. Hukujibu Kamati, hapa umetoa maelezo tu.

Kama hiyo haitoshi, basi labda nikwambie tu kwamba moja katika *findings* za CAG ni kwamba Halmashauri 131 hazikutekeleza mapendekezo au kujibu hoja za ukaguzi kikamilifu ambazo zina thamani ya Shilingi bilioni 78. Sasa maelezo yaliyomo katika hiki kitabu ni kwamba umeitisha kikao na Wakurugenzi. Hapa hujajibu hoja. Sasa mimi nitakupongeza vipi? Siwezi kukupongeza! Jibu hoja ili niweze kukupongeza. Lakini kilichofanyika, mmeitana St. Gaspar mmekwenda kuongeza gharama tu za matumizi ya Serikali. (Makofi)

Tunachotaka tuone, hizi Shilingi bilioni 78 zimekwenda wapi? Hiki ndicho tunachokitaka sisi kwa niaba ya wananchi. Kwa hiyo, tutakupongeza utakapokuwa umejibu hoja za ukaguzi kikamilifu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge hapa walizungumzia suala la asilimia 20 ambayo inatakiwa iende katika vijiji kutokana na zile kodi ambazo zimeondolewa na Serikali, ambayo tulikuwa tunaziita kodi za manyanyaso. Lakini vile vile kuna 5% kwa ajili ya vikundi vya akina mama na 5% kwa ajili ya vikundi vya vijana. Nampongeza Mheshimiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Waziri kwa ahadi aliyoichukua mbele ya Bunge hapa kwamba atahakikisha sasa hizi anazisimamia ili ziende.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kukwambia, tatizo la kutokwenda hizi fedha siyo la Serikali. Serikali inapeleka hizi fedha asilimia 20, tatizo liko Halmashauri na zaidi ni kwa Madiwani, kwa maana ya kwamba ni pamoja na sisi Wabunge. Hizi fedha zinapelekwa na Serikali, kwa maana ya kuzisimamia tu kwamba sasa ziende kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge kwamba hili nalo tulichukue, tujue kwamba liko katika mikono yetu vile vile.

Suala la 5% kwa wanawake 5% kwa vijana, ninachowaomba, hususan wenzangu Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tumetoa ahadi kwa Watanzania au kwa wapiga kura wetu kwamba tutawasaidia na tutajitahidi kuondoa matatizo yao katika baadhi ya maeneo. Tuishukuru Serikali kwamba imeweka sheria kwamba 5% kutoka katika mapato ya Halmashauri yaende katika vikundi vya akina mama na 5% ya mapato yake ya ndani yaende kwa ajili ya vikundi. Sasa katika vikao vyetu vya Halmashauri haya tusipoyasisitiza, tukawaachia tu Watendaji wakafanya wanavyotaka, hizi fedha hazitakwenda. Hatutawatendea haki wale ambao wametupa kura zao. Suala hili amelichangia sana Mheshimia Bura, Mheshimwa Moza pamoja na wengine.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilijitokeza ni suala la kesi zilizoko Mahakamani, Mheshimiwa Kafulila alilizungumza kwa nguvu sana; nataka niseme tu kwamba kuna udhaifu mkubwa bado katika suala zima la kushughulikia kesi zilizoko Mahakamani. Halmashauri zetu zimekuwa na mzigo mkubwa wa kesi katika Mahakama, kesi ambazo nyingi ni za kutengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wanasheria ambao tunao katika Halmashauri zetu ndio ambao wanashirikiana na watu ambao hawazitakii mema Halmashauri hizi, hutengeneza kesi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

ambazo hazina miguu wala kichwa na kuzitia Halmashauri zetu katika mlolongo huu wa kesi za Mahakamani.

Vile vile Mheshimiwa Kafulila alizungumzia suala la *DPP* na mimi nakubaliana naye kwamba kesi nyingi zilizoko Mahakamani *DPP* pia ni kikwazo. Tunaitaka Serikali, hili ilianganalie.

Mheshimiwa Spika, tuna mfano mmoja hai katika Halmashauri ya Kinondoni. Kuna mwekezaji pale kaingia ubia na Halmashauri. Halmashauri inapoteza takribani Shilingi milioni 900 kwa mwaka pale; basi kwa sababu tu ya yule Mwanasheria kutengeneza kesi na yule Mzungu ya kipuuzi basi Halmashauri inakosa mapato. Sasa wanasheria wetu ni lazima wachunguzwe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali upo, tupelekee wanasheria wazuri. Baadhi ya Wanasheria wako hawa wanaziharibu Halmashauri zetu. Ni wa kwako! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili alilizungumza Mheshimiwa Mturano pamoja na wengine.

Mheshimiwa Spika, suala la makusanyo katika Halmashauri, bado Halmashauri zetu Maafisa Watendaji, Maafisa Mipango sio weledi, wengi wao wanaonekana taaluma ya Mipango hawana kiasi kwamba wanashindwa kuibua vyanzo vipya vya mapato; lakini vile vile, vile vilivyopo kuweza kuviendeleza.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza! Nichukue mfano wa Halmashauri ya Jiji la Tanga. Jiji la Tanga linakusanya *three billion*. Lianganalie Jiji la Tanga lilivyo na ukubwa wake na rasilimali iliyonayo inapata Shilingi bilion tatu, inashindwa na Halmashauri ya Bagamoyo. Kule kuna *Airport*, kuna Bandari, Mabasi yanakwenda kila siku, kuna matangazo mbalimbali ya biashara, lakini wanashindwa na Halmashauri ya Bagamoyo. Sasa hii inaonesha ni namna gani baadhi ya hawa Watendaji wetu ambavyo hawana uwezo wa kuibua maeneo mapya ya kuweza kupata mapato.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama Serikali itaweka usimamizi mzuri wa vyanzo hivi vya mapato, basi nina uhakika kwamba Halmashauri zetu zina uwezo wa kufikia asilimia 20 ya kujitegemea. Haina wasi wasi! Maana yake ni ajabu Jiji zima la Tanga, yaani kwa Mkoa mzima wa Tanga, unashindwa na Jiji la Mwanza? Jiji la Mwanza linakusanya *10 billion!* Leo Mkoa mzima wa Tanga haufikishi *10 billion*. Hii yote ni kwa sababu pale kuna watu wamekaa kwa ajili ya ufsadi tu. Fedha zinapotea, mianya ya rushwa pamoja na mambo mengine ya kibadhirifu ni mengi. Ndiyo maana mapato mengi yanapotea na makusanyo hayakusanywi katika Halmashauri. Tunaionba Serikali, hili kwa kweli ilifanyie juhudi na iliwekee ufafanuzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *excess vote* pamoja na *exchequers notification* ambalo lilizungumzwa hapa. Mheshimiwa Waziri wakati anazungumzia suala hili la *excess vote* alikubali kwamba Halmashauri ya Mbarali kulikuwa na *excess*. Waliomba milioni 70 ama 75 wakapelekewa Shilingi milioni 800. Sasa kilichonipa tatizo hapa ni moja, kwamba Mheshimiwa Waziri anasema wamewachukulia hatua Watendaji. Watendaji sio waliofanya hili kosa.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yetu ya Kamati, tulisema kwamba kumeibuka mtindo ambao tunahisi ni mtandao wa kifisadi baina ya Hazina, TAMISEMI na Halmashauri. Hizi fedha Halmashauri baada ya kupelekewa, wao wemezitumia. Sasa unaposema umewawajibisha Watendaji, hukuondoa tatizo.

Mimi ninachojua, umewahamisha Watendaji hawa na wengine kuwapeleka Mahakamani kwa sababu hii Halmashauri ilipata hati chafu. Hicho Mheshimiwa Waziri ndio kitu labda ambacho ulikichukulia hatua. Lakini fedha hizi za *excess vote* tunajua ni fedha ambazo zinatoka Hazina, zinapelekwa Halmashauri, yaani ni zaidi ya kile kilichoombwa na zaidi ya kile ambacho Bunge kimekipitisha. Kwa hiyo, hizi fedha zinatumiwa bila ya idhini ya Bunge. Ndio tukasema, hapa kuna mtandao wa Kifisadi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mheshimiwa Spika, Shilingi million 500 ambazo zimepelekwa Korogwe, hizi fedha tumezikuta pale katika ukaguzi wetu zimetumika kwa ajili ya Uchaguzi na kwa ajili ya kuwalipa viinua mgongo Madiwani; ni fedha ambazo zimekwenda ziada katika lile fungu ambalo limepitishwa na Bunge. Hizi fedha zilitakiwa zirudishwe Hazina kwa vile zimekwenda ziada, lakini wao wakazitumia. Tatizo liko hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa bado Kamati inasisitiza kwamba kuna mtandao wa kifisadi baina ya Hazina, TAMISEMI na Halmashauri. Wanazitumia Halmashauri zetu hizi kwa ajili ya kutakatisha hizi fedha haramu. Fedha haramu siyo lazima zipeleke nje. Sasa hivi wanatumia mtindo huu kutakatisha hizi fedha katika Halmashauri zetu. Hizi fedha zinarudi huko huko.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala la *exchequers notification*. *Exchequers notification*, Kamati ilibaini kwamba kuna fedha nyingi ambazo zinapigwa tiktaka. Unajua mpira wa kona unapopigwa, kabla ya kutua chini unakuwa umeshapigwa tena uko juu. Hizi fedha ni kwamba Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinapewa taarifa kwamba Halmashauri tumeipelekea Shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Halmashauri zinajitayarisha na kule Hazina hizi fedha zinakuwa zimetoka. Sasa cha ajabu ni kwamba hizi fedha kule katika Halmashauri husika, hazikufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi ndiyo tunasema ni fedha ambazo zinapigwa tiktaka, hazifiki zinakohusika, zinakatwa juu kwa juu, goli linaingia ndani. Hapa ndiyo ambapo Kamati inapapigia kelele! Sasa sisi kama Kamati kwa kweli hili hatukuweza kuliacha, tumelisema na mategemeo yetu ni kwamba Serikali pamoja na mambo mengine italifuatilia suala hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Keissy alizungumza suala la Wabunge, nataka nimpongeza Mheshimiwa Keissy kwa mchango wake ule. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nataka niwe mkweli na niwe muwazi. Baadhi ya Wabunge wako mikono yao imetapakaa damu za dhambi katika Halmashauri zao. Baadhi ya Wabunge wako ndio ambao wanasababisha Halmashauri zao kutenda vibaya. Baadhi ya Wabunge wako, ndio ambao wanachukua baadhi ya miradi katika Halmashauri. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ahsantee!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, la ajabu kabisa, baada ya kuitengeneza miradi hii ikawa mizuri wao ndio ambao wanaifisidi miradi hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano mdogo; wakati tunafanya ziara katika Mkoa wa Tanga namshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mzee wangu, Mzee Kumchaya kwa mara ya kwanza Tabora nilimwona mtu mzima anatoa chozi mbele ya Kamati kwa namna ambavyo Watendaji wanashirikiana na baadhi ya Wabunge kuharibu miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge anathubutu kuchukua mradi wa Shilingi milioni 140 tena kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kwa ajili ya mama na watoto. Mradi ambao ulitakiwa ukamilike kwa kipindi cha miezi sita, sasa hivi una miaka mitatu haujakamilika na fedha Shilingi milioni 140 kati ya Shilingi milioni 150 zimeshatumika.

Nasema tena hiyo ni Tabora na iko Tabora Mjini na ni Mbunge wa CCM Viti Maalum ambaye amefanya dhambi hiyo. Sasa leo Mbunge huyu huyu anasimama ndani ya Bunge anaipongeza TAMISEMI, anapongeza kila kitu. Kumbe matokeo yake, yeye mwenyewe anarudi anakwenda kuihujumu TAMISEMI.

Sasa Waheshimiwa Wabunge hasa wa CCM jiangalieni sana. Sisi mnavyofanya hivi kwetu sisi ni faraja Wapinzani kwa sababu mnatupa mada za kuongea. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mheshimiwa Spika, tatizo hilo hilo hapo hapo Tabora, tumelikuta katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Wakati tunaangalia mradi wa Shule katika moja ya Majimbo yaliyoko Nzega, kuna majimbo mawili tu pale. Tumekwenda kuangalia darasa, limemalizika karibu miezi mitatu iliyopita, bado halijahamiwa. Kamati ilipokwenda pale, ilimkuta kijana anaichimba sakafu. Tukamwuliza wewe kijana, nani kakupa hii kazi? Kwanza jina lako nani? Akasema jina langu mimi Mchumia Tumbo. Ah, sasa wewe Mchumia Tumbo, nani kakupa hii kazi? Akasema, simjui. Nani atakulipa? Akasema, sijui!

Tukambana kwa kumtumia Kamanda wangu Mheshimiwa Kangi Lugola, Afisa Mstaafu wa Polisi, kwa kutumia mbinu zake za Kipolisi akambana yule kijana kumhoji, akamwambia; ah, sasa hii miradi si inachukuliwa na ndugu yake Mheshimiwa Mbunge! Sasa unafikiri patakuwa na nini?

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo matatizo tuliyonayo.

WABUNGE FULANI: Wataje! Wataje!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Keissy alizungumza kuhusu kuingilia utendaji wa Halmashauri.

WABUNGE FULANI: Wataje! Wataje!

SPIKA: Mheshimiwa utataja kwa ruhusa yangu. Endelea kujibu hoja, usiwasikilize hao. Wewe jibu tu dakika zako karibu zinakwisha.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Nzega ilipata mrahaba kutoka *resolt* wa Shilingi bilioni 2.3, zile fedha mpaka leo zimeshindwa kuendeleza Halmashauri hiyo kwa sababu tu Wanasiasa sisi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

tumetaka kuingillia zile fedha. Tilitaka kuzitumia katika njia ambazo pengine hazitaleta faida kwa wananchi wa Nzega. La kushangaza ni kwamba Nzega bahati mbaya hata ile mita moja ya lami hawana, wana *2.3 billion* zimekaa katika akaunti kwa sababu ya mvutano tu. Sasa uone namna gani ambavyo na sisi Wabunge tuna-*collude* katika kupunguza maendeleo katika Halmashauri zetu.

TAARIFA

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mimi ndio Spika, kwa nyle mnatumia maneno yenu? Naomba uendelee, umalize kwanza dakika zimekwisha. Namruhusu amalize kwanza kwa sababu dakika zimekwisha.

MHE. RAJAB M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kulizungumwa suala la uhusiano hapa na kufanya kazi *as a team work*, aliyezungumza ni Mheshimiwa Dkt. Kamani. Tunapofanya kazi katika Halmashauri kama *team work*, ni kweli matarajio ya wananchi yanaweza kufikiwa.

Nimpongeze sana Mheshimiwa Said Nkumba, tumekwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, kwa kweli namna ambavyo ameweza kushirikiana na Watendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge sasa hivi inaweza kujenga jengo kwa fedha zake la Shilingi bilioni tano. Miradi yake kwa kweli iliiridhisha sana Kamati kwa namna tu ambavyo ameweza kufanya ushirikiano mzuri na wenzake. Kwa hiyo, suala la *team work* kwa kweli kufanya kazi kama *team work* ni vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimika Spika, kuna fedha la *CDCF*. Kwa kweli fedha za *CDCF* bado ni tatizo, haziendi kwa wakati nahazijulikani ni muda gani zitaingia na muda gani Waheshimiwa Wabunge waende pale kwa ajili ya kuzipangia matumizi. Baadhi yao wameshauri kwamba ni vyema fedha hizi vile vile ziongezwe. Ni jambo zuri kwa kweli. Ukiangalia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

jiografia yetu, ukiangalia na hali halisi ya namna wananchi walivyoitikia wito wa kuijua hii CDCF sasa; ni vyema kwa kweli Serikali iangalie upya namna ya kuongeza fedha katika mfuko huu wa CDCF. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nidhamu kwa ujumla katika matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri zetu, imepungua. Lazima ukweli huo tukubali. Bado nidhamu ya matumizi iko chini kupita kiasi. Ni vyema sasa Serikali ikalichukua suala hili ikawa kama ni moja ya vipaumbele vyake. Bila ya kulichukua kama ni kipaumbele, kwa kweli hatuwezi kufanikisha lolote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hapa alizungumzia suala la Watumishi wabadhirifu kutokuhamishwa au kuchukuliwa hatua. Alizungumzia Watumishi wa Kishapu. Nataka nimwambie kwamba wako kweli baadhi amewachukulia hatua, lakini sio wote. Nataka kumpa mfano mmoja tu; aliyekuwa mshika fedha pale Kishapu, wakati panafanyika ule ufisadi wa Shilingi bilioni sita, huyu kapandishwa cheo, yuko katika Halmashauri ya Kiteto, ambaye sasa hivi ni Mweka Hazina. Sasa kwa kweli kama unachukua hatua, basi unachukua hatua nusu nusu. Wako wengine unawaacha na huwachukulii hatua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala ya Mvomero, ni jambo la ajabu, na Serikali imekuta jambo la ajabu pale Mvomero. Mvomero, nyumba ya Mkurugenzi imejengwa kwa Shilingi milioni 400. Leo ina mwaka karibu wa tatu haijahamiwa kwa sababu haijamalizika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda unavyokwenda, kuna suala la Mwanza. Wananchi wa Mwanza waliandaa *petition* wakaipeleka kwa Waziri Mkuu. Sasa leo Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba hakuna makosa kwa Mkurugenzi yule, ama hana taarifa yoyote, kwa kweli ni jambo la kushangaza. Lakini kwa sababu wachaguliwa wa Jiji la Mwanza wapo hapa, naamini kwamba hili watalifanyia kazi. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito wa matatizo ambayo Kamati iliyabaini na kuyawasilisha hapa Bungeni kupitia yake, na kwa kuzingatia michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, na kwa kuzingatia kuwa matatizo haya yamekuwa ni sugu katika Halmashauri yetu, licha ya Bunge kuishauri Serikali kila mwaka na bila Serikali kuwajibika; Kamati inasisitiza na inaliomba Bunge lako, pamoja na yote ambayo tumeeleza, lakini litoe baadhi ya maagizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kutokana na majibu ambayo Serikali sasa hivi imeyatoa, ni vyema sasa Bunge lako liagize kwamba CAG afanye uchunguzi maalum kwa kubaini mtandao ambao Kamati uliita wa kifisadi wa *excess vote*, wa *exchequers notification*, uhamisho wa watumishi wanaotuhumiwa pamoja na matumizi mabaya ya fedha za Serikali ambazo unajirudia kila mwaka. Ni vyema sasa CAG akafanya uchunguzi maalum katika maeneo hayo.

Pia ni vyema kuagiza kutazama na kupitia upya Sheria za Matumizi ili kubaini mianya iliyopo katika sheria hiyo ambayo inatoa fursa kwa watumishi ambao sio waaminifu kuitumia vibaya na kuisababishia hasara Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kwa kuwa Serikali inapeleka fedha nyingi katika Halmashauri zetu, uwezo wa Madiwani wetu ni mdogo. Ni vyema Bunge likaiagiza Serikali kwamba michango yote ya hali na mali ambayo inatolewa na wananchi, ionyeshwe katika hesabu za Halmashauri. Hii ni kwa upande wa michango ambayo inatolewa na wananchi. Lakini Madiwani waongezewe uwezo, weledi pamoja na marupurupu yao yaweze kuangaliwa upya, kwa maana ya maslahi, na mazingira yao ya utendaji wa kazi yaboreshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri hapa kayaeleza, mimi nina maoni kwamba ni vyema Bunge sasa liagize kwamba Mawaziri wote wanaohusika na TAMISEMI, ni vyema wajipime, wajitafakari kama wanatosha kuendesha na kusimamia Wizara kubwa na nyeti kama hii ambayo ni muhimu kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. R. M. MOHAMMED - MWENYEKITI WA KAMATI
YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA]]

maendeleo ya Watanzania ili haya matatizo ambayo tumeyazungumza leo yasiweze kujirudia. Hili nalizungumza nikiamini kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ananisikia. Labda nilirudie pengine hakunisikia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, tunataka sasa Mawaziri wote wanaohusika na TAMISEMI wajipime na wajitafakari kama wanatosha kuendesha ama kusimamia Wizara kubwa na nyeti kama hii ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kutoa hoja kuwa sasa Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Kamati pamoja na maoni na ushauri wa Kamati, na kwamba taarifa hiyo na mapendekezo yake yawe sasa ni maagizo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali, na kwamba utekelezaji wake ufuatiliwe na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

SPIKA: Ahsante. Hii taarifa ni ya Bunge, siyo ya Kambi ya Upinzani. Hii ni taarifa ya Bunge, imekubaliwa na mapendekezo yao yaliyokuwa kwenye taarifa yao yataangaliwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hii tumeimaliza. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipatia fursa hii jioni ya leo, niweze tu kuhitimisha hoja ya Kamati ya Bajeti ambayo inahusu taarifa yake ya mwaka huu, kama ilivyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia hoja hii. Sitawataja kama maelekezo ya kanuni zetu yanavyotaka, lakini wametusaaidia sana, na wote ambao wamegusa Kamati ya Bajeti wamesema vizuri tu, wametoa ushauri mzuri tu wa kujenga.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ni mpya. Tunaendelea kujifunza kila siku na tutaendelea kufanya hivyo. Lakini tumeyachukua mengi mazuri ambayo yatatuimarisha.

La kwanza, ni hili la kuwa na Ofisi ya Bajeti ya Bunge. Niishukuru sana, nimepewa taarifa kutoka kwa Ofisi ya Katibu wa Bunge kwamba zoezi hili linakwenda vizuri sana. Tunakushukuru wewe Spika kwamba tutaweza kupata Ofisi hii na wataalam wenye ujuzi na uzoefu wa masuala ya bajeti, ambao utawezesha sasa Kamati iweze kufanya kazi yake ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana, tunaishukuru sana Ofisi ya Katibu wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumesema humu kwenye taarifa, na tulisema kwenye taarifa ya Kamati ya Bajeti wakati tunapitia mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa letu kwa mwaka ujao wa fedha; eneo la mapato ya Serikali bado siyo la kuridhisha. Ni lazima tukubali kwamba sehemu kubwa ya bajeti ya Serikali, matumizi ya Serikali hayalingani na uwezo wetu wa mapato ya ndani. Maana yake ni kwamba kuna mjomba anatulisha. Hii kwa Taifa, siyo kitu kizuri, lazima *dependence syndrome* lazima tuanze kuipunguza; na tufanye kwa kasi. Tukienda kwa *speed* hii ambayo ipo, hatutaweza kujinasua mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashauri na tunaendelea kushauri kwamba tujielekeze katika maeneo mapya ya mapato. Mapendekezo ya *Chenge One Report* yapo, na tunaendelea kuishauri Serikali. Tumewapeni muda wa kutosha kuyapitia hayo, tuone ni wapi tunaweza tukaanza na maeneo mapya ya vyanzo vya mapato. Hili ni la msingi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

sana, na haitapendeza kila mwaka Serikali inakuja hapa na mapendekezo ya kuanzisha kodi mpya au kuongeza viwango vya kodi. Lakini hata katika kodi ambazo zipo, makusanyo yake bado hayapatikani kwa ufanisi. Hii ndiyo hoja tunayoisema, na tutaendelea kuisema ili kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Naibu Mawaziri wawili kwa maelezo waliyoyatoa katika maeneo mbalimbali ambayo yaliguswa na taarifa, lakini pia yaliguswa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Nitakuja kuyasemea mengine machache tu.

Mheshimiwa Spika, kwenye makusanyo ya mapato, sisi tunaamini kabisa kwamba yapo maeneo ambayo tukiyafanya kwa haraka, tunaweza tukaongeza mapato. Nimelisema kwenye Kamati, mapendekezo yale yamo. Suala la Vitambulisho vya Taifa, tunaamini kabisa kwamba zoezi hili likikamilika na kila Mtanzania akapata kitambulisho, tutajua anafanya nini; na lazima Serikali itapata haki yake kwa kile ambacho anakifanya kihalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna huu mpango wa Serikali wa kuanzisha *one stop boarder post* – Holili, Horohoro, Namanga, Sirari, Tunduma, Kabanga, Rusumo, Mtukula; yote haya tunajua, tukipunguza urasimu katika usafirishaji wa mizigo wakati wa *transit*, tutapata mapato mazuri tu. Tutekeleze hili tumalize. Nashukuru ya Bandari ya Dar es Salaam yanayoendelea kuhusu *one stop centre* wameishaanza, wanakaa sehemu moja, lakini limechukua muda mrefu sana. Haya tunajua yakifanyika, yataweza kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati kuu ni eneo la kuvuna tu. Ni kweli, ni shamba la bibi. Zile meli zinavua tu, lakini tunaweza tukapata mapato. Tunataka safari hii Serikali ije na mapendekezo ambayo yanawapa faraja Watanzania kwamba tunaanza kutumia rasilimali zetu zilizopo. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, Shirika letu la Petroli, kwa niaba ya Serikali, mikataba hii ya *production sharing agreement* tuliyonayo katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, inaipa haki ya kushiriki TPDC kwa kiwango kwa kutegemea upatikanaji wa mafuta hayo nchi kavu au katika bahari kuu. Mfano mzuri ni pale *Mnazi Bay*. TPDC imeshatoa *notice* ya kushiriki (ku-*participate*) katika eneo hilo. Maana unaposhiriki ni lazima uwekeze, na wamewaambia, ukiwekeza hapa, lazima kama unataka kutumia haki yako ya mkataba, sasa hivi gharama zetu ambazo zinakutaka wewe kwa kiwango unachotaka kushiriki, weka hela za kimarekani milioni 35. Zitakuwa zimeongezeka kidogo sasa hivi; lakini tunajuliza Kamati, tatizo liko wapi? Mikataba hii tunayo mingi, na inataka tushiriki.

Mheshimiwa Spika, nawaambia Watanzania wote kupitia Bunge hili, mikataba hii inawezesha Shirika la Petroli Tanzania kwa niaba ya Watanzania kuweza kushiriki kikamilifu katika haya maeneo ya gesi na mafuta. Sasa kama tunasuasua; tulielewa sisi mwanzoni kwamba labda Serikali inajipanga vizuri. Milioni 35 kuzipata kwa mara moja inaweza kuwa ngumu. Lakini tunaingia mwaka wa tatu, hakuna linalofanyika. Tunaiomba Serikali, kama hamwezi, mkakope pesa hizi ambazo mnakopa, mzielekeze TPDC iweze kushiriki iwe inapata mapato makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili linaungana na la kwanza la *Budget Office*. Tunachukua maelekezo yako, tumeisubiri sana Serikali kuleta Muswada wa Sheria ya Bajeti. Tunaambiwa bado wanafikiri wazee mle ndani. Nadhani wazee wataendelea kufikiri, hatutaipata hiyo sheria mapema.

Mheshimiwa Spika, tunayachukua haya maelekezo yako, na Kamati itaanza kufanya maandalizi ya Muswada huu mapema iwezekanavyo ili tunapofika mwisho wa mwaka huu wa fedha, tuwe na rasimu ambayo Wabunge wataweza kuiona, na kama ni kuiboresha, sawa. Lakini pia hatufanyi kazi ya kukinzana, tutaipa na Serikali nafasi ya kutosha na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

wenyewe waweze kuiona. Hatufanyi kazi gizani kama Waganga wa Kienyeji, hapana. Lengo letu ni moja, tunalotaka tishirikiane, lakini muda sasa haupo na sisi. Kwa hiyo, niliseme kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu. Huu mzunguko mpya wa bajeti hautakuwa na maana iwapo hatutaweza kujibu upatikanaji wa fedha, hasa fedha za maendeleo katika *quarter* ya kwanza ya mwaka wa fedha - Julai 1 mpaka tarehe 30 Septemba.

Mheshimiwa Spika, nimesikia maneno pembeni siyo rasmi, wanasema unaweza ukaharibu *the micro economic stability*. Itakuwaje? Pesa hizi zimekuwa *appropriated* kupitia ile Sheria ya *Appropriation* na Bunge lako. Ila tunasema haziji kwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, tunachoshauri ni kwamba Serikali ijiandae ikakope, zipatikane kwa upande wa maendeleo ili miradi ya maendeleo ambayo mtiririko wa mahitaji ya fedha yaani ile *cash flow requirement*, wanajua, isiweze kuathirika. Ugumu uko wapi? Mimi naiuliza Serikali, ugumu uko wapi? Tusipotatua tukapata jawabu, na siyo jibu; tusipopata jawabu katika eneo hili, mimi nasema kubadilisha *circle* ya bajeti ya Serikali haitakuwa na maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limesemwa vizuri sana, Naibu wa Fedha amelielezea. Tunafahamu miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa sasa kuna mkono wa Tume (Ofisi ya Rais – Tume ya Mipango), tunakubali kabisa. Lakini tunachosema, mtiririko wa mahitaji ya fedha, ile *cash flow requirement* inafahamika kwa kila mradi. Sasa unataka tu ujipange vizuri kwamba lazima pesa hii itoke kwa wakati, na isitoke kiduchu; itoke kwa mahitaji kama ilivyooombwa. Vinginevyo, miradi hii itaendelea kuumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Naibu Waziri ametoa takwimu tamu sana, ni tamu! Tunaongelea Tanzania Shillings, ni kweli zimetoka, lakini *component* ya nje, fedha ya kutoka nje kwa miradi hiyo, ukiangalia taarifa ambayo tuliitoa,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

haijatoka. Hiyo ndiyo hoja! Kwa hiyo, narudi la kwanza. Tusipojibu hoja na *dependency syndrome*, tatizo ni hilo. Miradi hii itaendelea kuumia kwa sababu zile za mjomba haziji kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la nne tumegusia katika taarifa hii kuhusu ukomo kwa mikopo ya kibiashara. Ukomo umefungwa na mapatano yetu kati ya Serikali yetu na Shirika la Fedha la Kimataifa kupitia *Policy Support Instrument*, kwa sasa imewekwa ni Dola milioni 700 kwa mwaka. Sawa, tuna mapendekezo mawili.

La kwanza, tunashauri kwamba majadiliano kati ya Serikali kwa maana ya Benki Kuu, Wizara ya Fedha yenyewe na Taasisi zake katika kupata mikopo hii, yaanze mapema kabla ya mwaka wa fedha unaofuata ambapo zinaombwa fedha hizi ili kuruhusu fedha hizi kupatikana *immediately*. Sio utaratibu wa sasa, mwaka wa fedha unaanza ndiyo wanaanza kufikiria wapi tukatafute fedha hii? *By the time* unapata hiyo mikopo, muda umekwenda. Sasa tunasema la kwanza, waanze majadiliano mapema, nadhani hilo siyo gumu.

La pili, tuchukue hata mfano huu, tulitoa taarifa humu Bungeni mwezi Oktoba, 2013 kwamba hata katika hizi milioni 700 tumechukua Dola milioni 118. Sasa ndiyo nakuuliza, mahitaji yako ni makubwa kwa miradi ya maendeleo, kwa nini uchukue tu milioni 118, si uchukue angalau robo ya kwanza? Ugumu ni nini? Maana mkopo umeishaupata milioni hizo; *quarter* ya kwanza chukua zote; na ya pili hivyo hivyo. Ukiweza, chukua yote, toa. Ndiyo tunapendekeza hivyo. (Makofi)

La pili, kubwa, tunasema ni vyema *ceiling* hii iangaliwe upya, ipandishwe. Maadam deni letu la Taifa tunasema linahimilika, na vigezo vyote vinaonyesha hivyo, basi tukubali tufanye hivyo. Tuliongeze kwa kiwango gani, watalaam wa Benki wa Kuu na Wizara ya Fedha, mtajua katika mazungumzo na wahusika. Lakini ipandishe. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

Mheshimiwa Spika, tunapokopa kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wengi; Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Ndassa na wengine walisema, pesa hizi na sisi kwenye taarifa hii ndiyo tunachosema kwanza fedha tunazokopa katika masharti ya biashara zielekezwe katika maeneo ya vipaumbele, maeneo ya kimkakati, siyo kwa ulaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Hamad Rashid, kwa aliyoyasema; ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Vile vile namshukuru sana Mheshimiwa Saleh Pamba, nilimsikia asubuhi. Wamesema hoja zipo ndani humu ni za kujenga. Lakini naichukua hii ya Mheshimiwa Hamad Rashid kwa namna ya pekee kwa sababu sisi kama nchi, tumezoea sana kwenda kwenye *traditional sources* za *funding*; vyombo vya fedha vya Kimataifa. Lakini sasa hivi yapo maeneo mengine sana mapya ya kuweza ku-*access* fedha za masharti tena nafuu ya kibiashara. Lakini tusipobadilika *mind set* tutaendelea na haya haya tu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha alipokuwa analielezea suala hili, wanavyochagua. Lakini nasema twende nje *box*; *thinking* yetu sasa lazima tutoke nje ya sanduku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo tumelisemea sana siyo humu, lakini pia linajitokeza katika Miradi ya Mkakati, ni Reli ya Kati. Reli ya Kati, tunaweza tukalia humu ndani. Upembuzi yakinifu wa Reli hii ya Kati ulianza mwaka 2006! *Is the longest feasibility study* ambayo imeweza kufanyika katika *Region* hii. (Makofi)

Ya kwanza imefanywa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, ikafanywa na Kampuni ya Kihandisi ya Ujerumani *DBI*, ikamalizika. Wanasema italipa. Awamu ya kwanza ni kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka kilomita 977, italipa. Wakaja ya pili, Serikali ya Marekani ikatoa fedha ikafanyika tena *Ballington Northern Santafee* wakafanya hiyo *feasibility study* nyingine ikaonesha inalipa. Ya mwisho, kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI]

WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

ufadhili tena wa Benki ya Maendeleo ya Afrika imefanywa na Shirika la Reli la Canada, *Cana Rail* inaonesha inalipa. Lakini miaka sita na nusu bado Watanzania tunafanya upembezi yakinifu, usanifu yakinifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu wakati tunafanya hii wanachukua muda mfupi tu; Mombasa – Nairobi – Kampala - Kigali. Lakini sisi haya maneno ni nini? Tatizo ni nini? *Phase* ya kwanza ya reli hii ipo, wataalam wamefanya uchambuzi mpana sana. Naiuliza Serikali, tatizo ni nini? Tusitafute mchawi nje ya Tanzania! Mchawi yupo ndani ya Tanzania! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu misamaha ya kodi limeelezwa vizuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, namshukuru sana, na huo ndiyo mwono wa Kamati ya Bajeti. Tunasema hatukatai faida ya misamaha ya kodi na kila nchi duniani zinafanya hivyo. Tunachosema, tubaki na maeneo ya misamaha ya kodi yenye tija na elekezwe hiyo misamaha kwenye uwekezaji mkubwa katika sekta za uchumi za kimkakati. Ndiyo *concept* tuliyonayo kwenye Kamati ya Bajeti, na Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono katika hilo na Serikali ije na sura hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sitasemea Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa sababu imekuwa ni kichekesho. Serikali imo humu humu, tumelisema, tumelisema, tumelisema; sasa niseme nini? Sina la kusema. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu nidhamu ya matumizi, limesemwa sana hili, mmelisema Waheshimiwa Wabunge nyinyi wenyewe. Matumizi lukuki, mapato kidogo. Lakini mipango ya kupunguza matumizi ya Serikali sisi tunapongeza. Unafahamu mimi huwa sipendi kukejeli kejeli mazuri yanayofanyika. Yapo tunayaona ambayo yanafanyika, lakini tunasema bado eneo hili bado halijakaa vizuri. Serikali inaweza ikafanya vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda mimi nasema *just* kwa kufikiria tu nilikuwa nafikiria tu, wala siyo wazo la Kamati la Bajeti, mimi ni mtundu tu, huwa nafikiria. Sasa kama mwaka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

huu matumizi ya kawaida ya Serikali ni Shilingi trilioni 12, ndiyo kwenye Bajeti hii, si ndiyo ukweli! Lakini mapato Shilingi trilioni nane. Sasa nasema tu, hali hii ukiona na wewe unataka kutuambia kwamba mwaka kesho unataka bajeti ya matumizi ifike Shilingi trilioni 19.8, naogopa sana! Mimi naogopa sana! Mimi ningesema, *okay*, hizo ni shughuli zipi ambazo zinatufanya tupanuke namna hiyo katika kipindi kifupi hiki? Je, hatuwezi tukasema, matumizi ya mwaka kesho yasizidi asilimia 10 ya matumizi ya mwaka huu? Eeh, *rough!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tutaumia katika maeneo mengine ni afadhali tukaumia, kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu na kwa faida ya watoto wetu. Lazima tufanye *business unusual*. Mimi nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tulielewe hili. Tukienda namna hii mimi nasema matumizi haya ya kawaida yanatisha.

Deni la Taifa na mishahara, maana watu tulionao unaweza kuchukua uamuzi kwamba wasitishwe mikataba yao ya kazi. Sawa! Unaweza kuamua kama Serikalii! Lakini mimi sishauri hilo. Unaweza ukasema tupunguze ajira isipokuwa katika maeneo ambayo ni muhimu sana.

Wananiambia huko; nasikia sana! Wanasema, sasa mbona umekubali Mkoa wa Simiyu kuanzishwa? Ndiyo, nimekubali Mkoa wa Simiyu kuanzishwa kwa sababu Mkoa wa Shinyanga ulivyokuwa, ulikuwa mkubwa mno! Eeh, tunapeleka huduma karibu na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huo. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana hilo. Eeh! Lakini nawasikia wanasema Simiyu, Simiyu; ndiyo! Simiyu, Katavi, Njombe na Geita; hongereni sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huo. Lakini hiyo haifanyi kwanza tuwe na matumizi makubwa ya Serikali kiasi hicho, halafu hatuoneshi njia za wazi za namna ya kuyapunguza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze kuhusu nidhamu. Namshukuru tena Mheshimiwa Hamad Rashid. Kama kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

watu ambao wameumia; nimeumia kimya kimya na kama Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe. Sisi tulitoa mapendekezo kwa Serikali kwamba yapo maeneo ambayo tungeweza kuanza nayo. Mojawapo ilikuwa upande wa Simu za Mkononi. Sasa haya ni mapendekezo. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna chombo chochote kinachoweza kuanzisha kodi isipokuwa kwa idhini ya Mheshimiwa Rais. Anayeanzisha kwa mujibu wa Katiba ni Mheshimiwa Rais kupitia Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, sasa hiyo hadithi na maneno mengi ya kusema kwamba, ni Kamati ya Bajeti. Kamati ya Bajeti ndiyo ilikuja Bungeni kupitia Sheria ya Muswada wa Fedha? Mimi naliuliza Bunge hili! Lakini kwa sababu sisi ni waoga *to stand in the heat gets out of the hot kitchen*, tunakimbia. Hapana!

Mheshimiwa Spika, lazima tukubali kutetea hoja zetu. Hoja hii ni ya Serikali! Sisi tupo tayari kushirikiana na Serikali na ninawashukuru sana Serikali walipoliona hili wakakaa na wadau. Lakini la kushangaza, wadau na Serikali wamekaa wakapendekeza namna ya kwenda mbele. Mapendekezo haya yamekaa na Serikali tangu tarehe 1 Agosti, 2013 na hatupati senti moja ya mapato. Sisi ndio tuko kwenye Kamati ya Bajeti, *we are concerned* kama mliyvyo nyinyi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu fedha hiyo ni fedha ya umeme vijijini, na fedha ya maji vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unafahamu sisi tumekulia vijijini kama wewe. Yale majogoo ya kienyeji huwa yakipigana yakachoka, yanaanza kutazamana hivi. Hatuwezi kufanya biashara hiyo! Sisi lazima tutafute njia ya kwenda mbele. Tunaomba Serikali kwa upande wa kodi ya simu, kwa upande wa *money transfer* wala tusiingize Kanuni za Bunge zinakataza. Sheria ya Fedha *the Finance Act*, kama zilivyo Sheria nyingine zote za nchi hii zinatawaliwa na Sura ya Kwanza ya Sheria za Tanzania. Unaweza ukapitisha sasa hivi, Rais hata kabla hawajafanya hivyo, lakini akasema nakubali. Kesho yake asubuhi mkarudi Bungeni. Hakuna kinachokataza! (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. J. CHENGE - MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI]

Mheshimiwa Spika, lakini nimesikia maneno kwamba, unajua haiwezi ikaletwa tena Bungeni, hapana. Inawezekana! *We have the opportunity* ya kuyarekebisha haya na tunaweza kama Bunge kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, kwenye maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu mapendekezo ya Mpango, tullelezea na tunaendelea kushauri...!

*(Hapa kengele ya pili illia kuashiri kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. ANDREW J. CHENGE: Ni kengele ya kwanza?

SPIKA: Kengele ya pili.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Ohoo!

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2013 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. HAMAD RASHID MOHEMAD: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Taarifa ya Kamati ya Bajeti imepitishwa na Bunge pamoja na mapendekezo waliyotoa. *(Makofi)*

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali -Mheshimiwa Filikunjombe.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru sana wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie kidogo taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali pamoja na hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu maudhui ya taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wale waliochangia taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali na kwa niaba ya Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Zitto Kabwe ambaye hayupo humu ndani sasa hivi kutokana na changamoto mbalimbali zinazomkabili kwenye Chama chake huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa michango yenu yote tumeipokea kwa mikono miwili. Sisi kama Kamati tunaitambua na tumeifanyia kazi. Natambua kwamba michango yenu mingi imelenga katika kukosoa matumizi mabaya ya fedha za umma na kushauri Serikali juu ya hatua mbalimbali katika kuboresha hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, nawashukuruni wote; CAG na Waheshimiwa Wabunge. Ukisoma ripoti ya CAG inayoishia tarehe 30 Juni, 2012, jambo moja lipo bayana kwamba bado tuna shida kwenye matumizi ya fedha. Ripoti ya CAG inaonesha kuwa bado kuna matumizi mabaya katika fedha za Umma. Fedha za Umma zinatumika vibaya, fedha za Umma zinatafunwa, fedha za Umma zinaliwa na sisi kama Wabunge hali iliyopo hapa mbele sasa hivi tunataka bajeti na fedha ziongezwe. Lakini ukweli ni kwamba hata kile kidogo tunachokipata sasa hivi, hatukitumii vizuri. Tumekuwa wepesi wa kuwalaumu Hazina na Wizara ya Fedha, kwamba *disbursement* ni ndogo, fedha hazipelekwi kwenye Mawizara na kwenye maeneo husika, lakini ukweli ni kwamba maji yanavuja.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba hata tukizidi kuongeza fedha, hata tungefika trilioni kadhaa, kama hatuwezi kuziba hii ndoo ya maji inayovuja, bado hatuwezi kuwa na ufanisi. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. H. FILIKUNJOMBE - MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI]

Mheshimiwa Spika, kwenye ripoti yetu tumependekeza mapendekezo kadhaa ya kuziba matundu hayo ili tuweze kufanikiwa, lakini kwenye ripoti ya CAG Kamati imebaini kwamba fedha za ndani zitafunwa na fedha za nje nchi zinaliwa.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda kwenye Shirika moja sisi kama PAC Mamlaka ya Bandari (TPA), tulikuta kwa mfano kwa mwaka mmoja Waheshimiwa Wabunge, Mamlaka ya Bandari wametumia bilioni tisa kwa *Master Workers Council*. Sasa tukawauliza hawa *Master Workers Council*, kwanza mlifanyia wapi? Hapa hapa ndani. Wako wangapi? Wako 180. Mmelipanje mpaka inafika Shilingi bilioni tisa?

Huko huko Mamlaka ya Bandari wamekutwa wametumia Shilingi bilioni tisa kwa matangazo. Sasa tukauliza, haya matangazo mmetangaza wapi? Nje au ndani? Kwasababu kama ni nje, labda. Kama ni ndani ya Tanzania matangazo ya Shilingi bilioni tisa, kila mmoja leo hii hata mtu ambaye yupo tumboni angejua TPA.

Sasa kama Kamati, tunawapa tu Taarifa kwamba matumizi ya fedha siyo mazuri kwenye Serikali na kwenye Mashirika ya Umma. Tumeagiza, tumemwomba CAG akafanye *Forensic Audit* tujiridhishe na haya matumizi ya Shilingi bilioni tisa kwa matangazo na Shilingi bilioni tisa kwa *Master Workers Cancel*. Jimboni kwangu Ludewa, Shilingi bilioni tatu na nusu ni fedha ya maendeleo ya mwaka mzima. Sasa hii fedha ingeweza kufanya maendeleo katika maeneo mbalimbali. Serikali kama Kamati tunapendekeza lazima ichukue hatua kuziba mianya ya matumizi mabaya ya fedha.

Sisi kama Wabunge Tubadilisha Sheria. Mimi nimemsikia Mheshimiwa Hawa Ghasia akisema Wabunge wanamtuhumu kwamba ni mwizi. Mimi niseme, hakuna aliyesema Mheshimiwa Hawa Ghasia ni mwizi, hapana. Lakini wale walio chini yako, chini ya Wizara fulani, wanapofanya vibaya, mwenye dhamana ya Wizara ni Waziri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. H. FILIKUNJOMBE - MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI]

Sasa kuna baadhi ya Sheria tumetunga, tunalaumu kwamba Watumishi wa Umma Sheria zao zinawalinda sana. Lakini Sheria za Utumishi nyingine tumetunga wenyewe Mheshimiwa Ghasia akishiriki. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hata jitihada zinazofanywa na Serikali unaona siyo za wazi za kutaka kupokea mapendekezo na maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 tumepitia Sheria hapa kwenye mfuko ambayo tulisema kabisa kwamba *CAG* akileta ripoti, Serikali nayo itawasilisha majibu *simultaneously, concurrently*. Ie sheria haijafanya kitu, ilikuwa ni Sheria ya kuwalinda wezi ile. Mimi ningeomba Serikali ilete Sheria za kuisaidia Serikali isiwatete Watendaji wachache au watumishi wachache, kwa sababu tunafika mahali humu ndani tunasema maoni ya *CAG* siyo *final*. Lakini majibu ya Serikali lazima upeleke kwa *CAG a-verify* ndiyo yaje hapa. Mkituletea majibu bila *CAG* kupitisha sisi hatuwezi kuyapokea. Maoni ya *CAG* ni *verified Opinion, ni technical opinion*, na sisi Waheshimiwa Wabunge tuna imani na Ofisi ya *CAG*. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, kwakuwa maeneo mengi ya Taarifa ya Kamati yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge, niende moja kwa moja kwenye baadhi ya mapendekezo. Waheshimiwa Wabunge walipochangia humu ndani wengi wamechangia kwenye eneo linalohusu ruzuku ya fedha ya Umma kwenye Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, kutoka mwaka 2009 mpaka 2012 Vyama vya Siasa ambavyo vimechukuwa zaidi ya Shilingi bilioni 68 havijakaguliwa hesabu zake. Ni maadili mema kwa sisi wanasiasa tulioko humu ndani tunapoinyoshea mkono Serikali na sisi tu-*practice* haya tunayoyasema, tunayoyahubiri. Shilingi bilioni 68 ni fedha nyingi, zingeweza kuleta maendeleo kwenye Wilaya 19 kwa mwaka mmoja, sisi tumezitumia, tinalumbana. Nataka niseme bayana kwamba haya ni maoni ya Kamati, ni msimamo wa Kamati kwamba tumemwagiza *CAG* aende akakague hesabu za Vyama vyote, kutoka mwaka 2009 mpaka 2012 na tumempa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. D. H. FILIKUNJOMBE - MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI]*

mwezi; tulimpa miezi mitatu mpaka Januari 30, 2014; hesabu zilizokuwa zimewasilishwa kwake zilikuwa za Vyama vinne tu; CUF, NCCR-Mageuzi, TLP na CCM. Tumevitaka na Vyama vingine vilivyosalia navyo vipeleke hesabu zao kwa CAG. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili Suala siyo la malumbano. CAG anatupa ukweli. Aakizikagua mwezi Januari, zitakuja kwenye Kamati ya PAC, tutazipitia. Nami kwenye hili niseme bayana kwamba mimi kama mbunge wa Chama cha Mapinduzi, nitatenda haki kwa wote, nitatenda haki kwa Vyama vyote. Msije mkaja CCM kwa Filikunjombe na kuniambia kwanini kwenye suala hili la hesabu zetu chafu hukututonya mapema? Hapana. Maadili ya Kamati yetu, kwa maadili ya utendaji ni lazima tusimame katikati.

Kwa hiyo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge msiwe na papara, CAG atafanya kazi yake, tumempa mpaka Januari, aje. Fedha hizi ni mali ya Umma, yule ambaye hataki kuisikia PAC, yule ambaye hataki kumsikia Filikunjombe, asipokee fedha za ruzuku; kama hutaki kumsikia Zitto Kabwe, usipokee fedha za Umma. Kama kuna Chama chako hakitaki kusikia PAC, usipokee fedha za Umma. Wanaotoa fedha hizi wengine hawana hata Vyama. Fedha hizi ni mali za Umma, ni lazima zikaguliwe, na sisi kama Kamati tutalisimamia hili, tutatenda haki na maoni yanayotolewa hapa siyo ya kwangu ni maoni ya Kamati wala siyo maoni ya Zitto Kabwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeongelea pia udhibiti wa misamaha ya kodi. Mheshimiwa Waziri amefafanua. Lakini katika hili Kamati inaitaka Serikali kwamba Sheria ya Taifa ya Ukaguzi ifanyiwe marekebisho upya ili kumpa nguvu CAG uwezo wa kukagua wa kisheria misamaha ya kodi. Naomba ieleweke hapa kwamba sisi kama Kamati hatupingi misamaha ya kodi. Kuna baadhi ya maeneo yanafanya vizuri. Lengo la pendekezo hili ni kubaini ufanisi wa tija ya misamaha inayotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililosemewa na Kamati na kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. H. FILIKUNJOMBE - MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI]

ni kuhusu uamuzi wa Mamlaka ya Bandari kusitisha matumizi ya *flow meters*. Kusitishwa kwa matumizi ya *meters* hizi ni hasara kwa Serikali kutokana na gharama kubwa za ununuzi wa *meters* hizo na uwezekano mkubwa kwamba Serikali inapoteza mapato kwa *meters* hizo kutotumika. Sisi kama Kamati tumeamua kwamba tutaunda Kamati ndogo ya kiuchunguzi ili ikachunguze na kujua ukweli juu ya kusitishwa kwa *flow meters* katika bandari yetu ya Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu ambalo Kamati tunaliwekea msisitizo ni kuhusu mapato katika Sekta ya Mawasiliano. Tulichobaini kama Kamati ni kwamba hakuna mawasiliano mazuri kati ya *TCRA* na *TRA*. Takwimu walizonazo *TCRA* ziko juu, takwimu za Mamlaka ya mapato zipo chini. Tumeziagiza Mamlaka hizi mbili zikae pamoja na zishirikiane. Haiwezekani Taasisi mbili za Serikali kila mmoja ana takwimu zake mfukoni mwake, amejifungia nyumbani kwake. Lakini kwa kuboresha mapato, na hili tumelisema toka tukiwa *POAC* kwamba *TCRA* iharakishe ufungaji na utumiaji mtambo maalum wa kukokotoa miamala ya simu na kuboresha sheria zote zinazosimamia misamaha ya kodi katika eneo hili. Kwenye hili tunasisitiza tena, *TCRA* na *TRA* ni lazima wafanye kazi pamoja, kuna fedha tunazipoteza bila sababu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya *PAC* pia imebainisha kuwa *PSPF* inaidai Serikali deni kubwa sana. Deni hili ni kubwa na ulipaji wake hauridhishi. Nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri akitoa ufafanuzi kwamba wanalipa Shilingi bilioni 50, wamelipa Shilingi bilioni 60, lakini makubaliano kati ya Serikali, Bunge na Taasisi husika, ilikuwa ni kwamba Serikali italipa Shilingi bilioni 71 kila mwaka kwa miaka kumi.

Sasa Serikali ilipokuwa inapiga chenga, labda Mheshimiwa Waziri asimame na kusema hapa kwamba yeye hatazeeka au watumishi wake, Makatibu Wakuu hawatazeeka na hivyo hawahitaji *pension*. Wastaafu wanapata shida, wanahangaika. Kwa hiyo, sisi kama Kamati, kuinusuru hali hiyo, tunaiagiza Serikali kuhakikisha kwamba inailipa *PSPF* kama tulivyokubaliana, kiasi cha Shilingi bilioni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. H. FILIKUNJOMBE - MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI]

71 kila mwaka ili kunusuru Mfuko huo na wazee wetu wastaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye mamlaka hiyo hiyo, Kamati pia inaitaka Mamlaka ya Usimamizi na Usimamizi wa Sekta Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) iwe makini katika kusimamia kiwango cha uwekezaji na mikopo yote inayotolewa na Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kwamba kiwe kinalingana na uwezo wa Mfuko. Tumegundua baadhi ya Mifuko inawekeza, inazidi kuwekeza na uwekezaji wake unakuwa hauna tija kwenye baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, kama Kamati tunapendekeza kwamba *SSRA* watoe maelekezo kwamba *SSRA* wasimamie uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashirika ya umma Serikali imekuwa mhanga katika hasara zitokanazo na Mikataba mibovu ikiwa ni pamoja na mkataba ulioingiwa na *ATCL* chini ya udhamini wa Serikali ambao mpaka sasa deni lake limefikia kiasi cha Shilingi bilioni 47.12. Kamati inaiomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba Serikali ivunje Mkataba huo mbovu usio na tija uliongia chini ya udhamani wa Serikali na uvunjwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inamuwomba pia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) afanye Ukaguzi wa nyaraka za madeni ya Serikali yaliyotokana na mali zilizouzwa ili kubaini wadaiwa na kiasi cha fedha zinazodaiwa na kisha kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili madeni hayo yakusanywe au kuvunjwa mikataba husika na kuzirejesha mali hizo zilizouzwa mikononi mwa Serikali. *CHC* ilipofanya utengefu wa baadhi ya madeni hayo ilikuta yana zaidi ya thamani Shilingi bilioni 83. Fedha hizi ni nyingi na bila kufanya uhakiki hali hii inaweza kusababisha ugumu wakati wa kukusanya deni hilo.

Mheshimiwa Spika, yaliyosemwa yapo mengi, lakini kwa kifupi nilitaka tu kusema kwamba kuna baadhi ya Wizara zinafanya vizuri, kuna baadhi ya Taasisi zinafanya vizuri na ziko Wizara ambazo hazifanyi vizuri kwenye usimamizi wa fedha na kwenye usimamizi wa mali za Umma.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. H. FILIKUNJOMBE - MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI]

Mheshimiwa Spika, kwakuwa kama Kamati tumebaini kwamba bado kuna upotevu wa fedha za Umma katika Wizara na Taasisi mbalimbali; kama Kamati tunapendekeza kwamba wale Mawaziri ambao wamekuwa mizigo na Wizara zao au Taasisi zao zimekuwa zikifanya vibaya; wajipime, wajitafakari wao wenyewe kama wanaweza kwenda na kasi ya *Big Results Now* katika kuwaletea maendeleo Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha hoja.

SPIKA: Naomba uisome hoja yako kama ilivyo. Hoja yako inasemaji?

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee Taarifa ya Kamati na ikubali mapendekezo yake yote kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali
kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati hiyo
kwa mwaka 2013 ilipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wenyeviti wa Kamati zote tatu na Waheshiwa Wabunge wote kwa sababu hizi Kamati ndiyo zinaongozwa na Kambi ya Upinzani, lakini ni Kamati za Bunge. Hii tuliipitisha wenyewe kwenye kanuni zetu kwamba Kamati hizi ambazo tunasema ni *watch dog committee* zitaongozwa na Kambi ya Upinzani. Hiyo ilikuwa ni kwa makusudi tu kusudi kuwepo na utaratibu mzima wa kuangalia, lakini wameshirikiana wote. Kama tunavyosema siku zote, siku za mbele tutaziangalia namna ya kuziandika Taarifa hizi kusudi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

mapendekezo yao yawe bayana. Tunapoamua kitu kinakuwa bayana; tunapendekeza nini kufuatana na Kamati na siyo kusambaza mapendekezo kwenye Taarifa nzima. Kwa hiyo, inakuwa hata mlichuamua inakuwa pengine siyo bayana. Kwa hiyo, tutaendelea kusimamia namna ya kuziandika Taarifa hizi vizuri zaidi, kusudi mapendekezo yale yawe bayana.

Halafu wengine tumefanya kazi kubwa ya kuendelea kuwapa mafunzo Kamati hizi zote. Wengine wamekwenda kwenye *Westminster* kwenye semina yao ya *Public Accounts Committee* ya Uingereza. Hatuwezi kusambaa Wizara zote na mashirika yote mwisho wake Taarifa inakuwa *weak*. Lakini kama mnajua kabisa eneo hili ndilo lenye udhaifu mkubwa, mnaenda pale pale mnazamia, tukifika hapa tunatoa mapendekezo yenye msingi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mnakwenda katika maeneo ambayo ni nyeti, tusema *strategic* ukiweza kuwafikia hao wenye *strategic*, tunafika mahali sisi wenyewe wengine wanakuwa lazima wafuate. Lakini ya kusambaa kote, *HaImasha* uri zote, Wizara zote, mwisho wake *weakness* ya zile Taarifa zenu zote zinabeba uzito ule ule wakati kuna maeneo ambayo sisi tuna *interest* nayo.

Kwa hiyo, hii ndiyo *training* nadhani waliyoipata Kamati ya *PAC* juzi kwenye *Westminster* na mimi nilikwenda *Westminster* miezi miwili kusomea nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ya *Public Accounts Committee*. Kwa hiyo, tunataka tu-*spot* maeneo tunayofikiri ni *key*. Pale ndiyo mnazamia kweli kweli! Mkitoa Taarifa zenu hapa, kila mtu anazikubali na hata hatua mnazozipendekeza zinakuwa rahisi. Lakini ya kwenda jumla tu, inakuwa ni jumla mno. Kwa hiyo, tutaangalia hiyo.

Kama nilivyosema, bado Serikali itabidi ijibu yale majibu ya *Control* na *Auditor General* kiutaalamu na hiyo Taarifa itawasilishwa hapa, ndiyo inaitwa *treasury observation ministries* ambazo zitaeleza kabisa wamefanya nini kwa hoja gani na nani anawajibika? Huo ndiyo utaratibu unaotakiwa ufanyike. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa mtindo ambao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

tutakaa pamoja na wote tuangalie utaratibu mpya na mzuri zaidi wa kusimamia Serikali kwa maeneo haya ya matumizi ya fedha tunaweza pata jibu ambalo lina maana zaidi. Kwasababu hakika tunataka discipline kwenye mambo ya fedha.

Discipline ya mambo ya fedha ni ya lazima vinginevyo, siyo nchi. Kwa hiyo, hayo nashukuru. Nashukuru pia Mheshimiwa Keissy, maana kama nilivyosema jana, muhimili wetu kama huu wa kwetu lazima uwe na nidhamu. Huwezi kuanza kuonesha vidole kwa watu wakati vitatu vinakuja kwako. Ni lazima sisi tukiwa na nidhamu, hii kazi tutaiweza. Kwa hiyo, mimi nafurahi kama mmeanza kukosoana wenyewe ni vizuri na mwendeleo kukosoana kusudi mweze kuonekana vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kesho tunaendelea na Taarifa za Kamati ya Katiba na Sheria halafu tutakuwa na Kamati ya Katiba Sheria na Utawala halafu na Kamati ya Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, tutakuwa na mjadala wa siku moja Kamati mbili.

Kama nilivyosema, tunalo tatizo la *time*, kwa sababu lazima tumalize tarehe 20 kusudi maandalizi ya Bunge la Katiba yaanze humu ndani. Kwa hiyo, nategemea...

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mwongozo Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Sijamaliza, unasema Mwongozo, ni adabu za wapi?

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tutajitahidi sana tuweze kwenda mjadili vitu; acheni siasa kwenye kujadili Taarifa za Kamati. Acheni! Zungumzeni yaliyopo ndiyo yanayowasaidia Watanzania. Mkianza Vyama vyenu, haisaidii kitu!

Waheshimiwa Wabunge, tafadhali mjifunze. Ni Bunge peke yake linaendelea na siasa ndani humu. Tuzungumze

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Taarifa na utendaji wa Serikali hapa! Hii ni kwa mujibu wa Katiba kabisa kifungu cha 63. Tuache kuzungumza habari za siasa, tunawachanganya wananchi, haina maana yoyote. Tutakuta muda wetu ni mfupi, mkitumia vizuri tunaweza kufanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naombeni mfanye hivyo. Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa naomba mwongozo wako juu ya jambo ambalo lilitokea wakati Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha za Serikali Kuu anafanya majumuisho yake.

Mheshimiwa Spika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya PAC katika majumuisho ameonesha na kwa kauli yake kwamba kuna Vyama ambavyo Hesabu zao hazijakaguliwa na kwa maneno amesema kama hivyo Vyama hazitaki kukaguliwa, basi visipate fedha za ruzuku. Nafikiri mimi namuunga mkono kwenye hilo, isipokuwa naomba nisome tu kauli ya Taarifa Kamati ya PAC kuhusu jambo hili, iko kwenye ukurasa wa 32 wa Taarifa ya Kamati ambayo inazungumzia kwanini Hesabu za Vyama hazijakaguliwa? inasema hivi: "Kwenye mapendekezo ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali Kuu 4.2.1 Msajili wa Vyama vya Siasa kutotangaza kwenye Gazeti la Serikali Hesabu zilizokaguliwa kwenye Vyama vya Siasa kwa miaka minne iliyopita."

Wanasema: "kwakuwa Kamati ilibaini kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa tangu mwaka 2009 hakuweza kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Hesabu zilizokaguliwa za Vyama vya Siasa kutokana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kukagua Hesabu za Vyama vya Siasa 19 isipokuwa Vyama viwili tu vya Siasa; CCM na TLP kwasababu ya kukosa fedha za kufanya Ukaguzi na ndiyo maana katika mapendekezo ya Kamati, pendekezo hili linasema:

SPIKA: Hoja ni nini?

WABUNGE FULANI: Aaah!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Siyo aaah!

MBUNGE FULANI: Siyo kweli!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Bunge kwa miaka ijayo ya fedha iwe inatenga fedha za kutosha kwenye Fungu la 45 - Ofisi ya Taifa ya ukaguzi ili Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweze kufanya ukaguzi wa Hesabu za Vyama vya Siasa bila vikwazo.

Mheshimiwa Spika, naomba utupe mwongozo, kama ni sawasawa, kwa Makamu Mwenyekiti wa PAC kulaumu Vyama vya Siasa kwamba vinakataa kukaguliwa wakati Taarifa ya Kamati inasema wazi kwamba CAG AMESHINIDWA kukagua Hesabu hizo kwasababu hana fedha. Hajatengewa fedha. Kwanini Vyama vinalalamikiwa kwa jambo ambalo haliko kwenye mamlaka yao?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

SPIKA: Mwongozo ni kwamba Vyama vikaguliwe, na CAG atoe fedha, basi yamekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine, naahirisha shughuli za Bunge, mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.40 Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi,
Tarehe 12 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*